Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project

Published on *Books on Islam and Muslims* | *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Imam Mahdi katika Usunni Na Ushia

Al-Mahdi Fi 's-Sunnah

Author(s):

Sayyid Sadiq al-Husaini al-Shirazi [3]

Publisher(s):

Al Itrah Foundation [4]

Kwa Waislamu, imani ya kuja kwa Mahdi (Muhudi) karibu ya mwisho wa dunia ni imani ambayo ina asili katika dini. Waislamu wote bila kujali tofauti za madhehebu zao wanakubaliana juu ya imani hii kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.) alisema: "Hata iwe imebakia siku moja tu kwa dunia hii kufikia mwisho wake Allah atairefusha siku hiyo ili kumwezesha Imam huyo kutawala na kuujaza ulimwengu huu uadilifu, amani na utulivu wakati ambapo ulikuwa umejaa ufisadi na dhulma." Kitu cha kuvutia ni kwamba imani hii haiko kwa Waislamu tu bali hata katika dini nyingine wana imani kama hii kwamba atatokea mtu wakati wa mwisho ambaye ataondoa dhulma na ufisadi na kuujaza ulimwengu huu uadilifu, amani na utulivu.

Translator(s):

Abdul Karim Juma [5]

Category:

Imam al-Mahdi – Imamu wa Kumi na Mbili [6]

Topic Tags:

Sunna [7]

Historia [8]

Imani [9]

Person Tags:

Imam al-Mahdi (as) [10]
Ahlul Bayt (as) [11]
Mtume Muhammad (s.a.w) [12]

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni mkusanyo wa tarjuma ya vitabu viwili vya Kiarabu. Cha kwanza ni, *al-Imam al-Mahdiyyu fii Riwayati Ahli's-Sunnah,* kilichoandikwa na Sayyid Abdul Rahim al-Musawi. Sisi tumekiita, *Imam Mahdi katika Riwaya za Sunni*. Na cha pili ni: *al- Mahdawiyyah 'Inda Ahli 'l-Bait* kilichoandikwa na Sheikh Abdul Karim al-Bahbahani . Sisi tumekiita: *Umahdia katika Ahlul Bait.* Tumevikusanya pamoja kwa vile tumeona maudhui yao yanafanana.

Vitabu hivi ni matokea ya utafiti wa kielimu pamoja na hoja zenye nguvu na utumiaji sahihi wa akili uliofanywa na wanachuoni wandishi wa vitabu hivi.

Kwa Waislamu, imani ya kuja kwa Mahdi (Muhudi) karibu ya mwisho wa dunia ni imani ambayo ina asili katika dini. Waislamu wote bila kujali tofauti za madhehebu zao wanakubaliana juu ya imani hii kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.) alisema: “Hata iwe imebakia siku moja tu kwa dunia hii kufikia mwisho wake Allah atairefusha siku hiyo ili kumwezesha Imam huyo kutawala na kuujaza ulimwengu huu uadilifu, amani na utulivu wakati ambapo ulikuwa umejaa ufisadi na dhulma.”

Kitu cha kuvutia ni kwamba imani hii haiko kwa Waislamu tu bali hata katika dini nyingine wana imani kama hii kwamba atatokea mtu wakati wa mwisho ambaye ataondoa dhulma na ufisadi na kuujaza ulimwengu huu uadilifu, amani na utulivu.

Mkusanyo wa vitabu hivi ni wenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kuvichapisha vitabu hivi kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya kidini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Hemedi Lubumba Selemani kwa kukubali jukumu hili la kuvitarjumi vitabu hivi. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Mchapishaji:

Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.

Neno La Jumuiya

Hakika mirathi ya Ahlul-Bait ambayo imehifadhiwa na kambi yao na wafuasi wao dhidi ya upotovu inaonyesha kambi iliyokusanya aina mbal- imbali za taaluma za kiislamu.

Kambi hii imeweza kulea nafsi mbalimbali zilizo tayari kunywa kutoka kwenye chemchemu hiyo, na kuupa umma wa kiislamu wanavyuoni wakubwa wenye kufuata nyayo za ujumbe wa Ahlul-Bait.

Wanavyuoni waliokusanya vidodosa na maswali mbalimbali ya madhehe- bu na mitazamo tofauti ya kifikira kuanzia ndani ya desturi ya kiisilamu hadi nje ya desturi hiyo, huku wao wakitoa majibu na utatuzi makini juu ya maswali hayo ndani ya karne zote.

Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul-Bait imefanya hima kutetea tukufu za ujumbe wa Uislamu na ukweli wake ambao umechafuliwa na makundi, madhehebu na wanaharakati mbalimbali wenye chuki na Uislamu.

Jumuiya imefuata nyayo za Ahlul-Bait na za wafuasi wa kambi yao njema ambayo imefanya hima kujibu madai yenye kuendelea na daima ikajaribu kubaki ndani ya msitari wa mapambano kwa kiwango kinachohitajika ndani ya kila zama.

Hakika uzoefu ambao umehifadhiwa ndani ya vitabu vya wanavyuoni wa kambi ya Ahlul-Bait katika dhamira hii ni wa aina ya pekee, kwa sababu una akiba ya kielimu inayotegemea akili na hoja, huku ukijiepusha na matamanio na upendeleo uliokatazwa.

Unazungumza na wasomi na wanafikra wenye fani maalumu, mazungum- zo ambayo yanakubalika kiakili na yanapokewa na maumbile yaliyo sala- ma.

Jaribio hili la Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul-Bait limekuja kuwapa watafu- ta ukweli hatua mpya ya uzoefu wa thamani katika ulingo wa mazungum- zo na maswali na kujibu hoja za utata zilizotolewa zama zilizopita au zina- zotolewa leo kwa njia ya Tovuti, na hasa kwa kupewa nguvu na baadhi ya duru zenye chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Ikijiepusha na uchochezi uliokatazwa, na ni yenye kuhangaikia kuzishau- ri akili zenye kufikiria na nafsi zenye kutafuta haki, ili ziweze kufikia kwenye haki ambayo inatolewa na Kambi ya Ahlul-Bayt ulimwengu mzima, ndani ya zama ambazo akili inaerevuka na nafsi na roho zinabore- ka kwa kasi ya pekee.

Ni lazima tugusie kuwa mfululizo huu wa tafiti hizi umeandaliwa na Kamati maalumu toka jopo la wanavyuoni watukufu, hivyo tunatoa shuku- rani njema kwa hawa wote na kwa wasomi na wahakiki kwa kila mmoja miongoni mwao kupitia sehemu ya tafiti hizi na kutoa mchango wao wa thamani kuhusu tafiti hizi.

Na sote tunategemea na kutaraji kuwa tutakuwa tumetoa kile tulichoki- weza katika juhudi za kutekeleza baadhi ya wajibu tulionao mbele ya ujumbe wa mtukufu Mola wetu Mlezi ambaye alimtuma Mtume Wake na uongofu na dini ya haki ili aipe ushindi dhidi ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.

Jumuiya ya kimataifa ya Ahlu-Bait
Kitengo cha utamaduni

Imam Mahdi Ndani Ya Riwaya Za Kisunni

Utangulizi

Imani ya ulazima wa kudhihiri suluhisho la ulimwengu huu na kusi- mamisha dola yake ni imani isiyohusu watu wa dini tu, bali inayajumuisha hata makundi ya kitheolojia na kifilosofia yasiyokuwa ya kidini. Kwa mfano kundi la wapagani wajulikanao kwa jina la Al-Jadliyyah ambalo limefasiri historia kwa kigezo cha kutokuwepo uwiano kinaamini kuwa ipo siku iliyoahidiwa mpishano huo utatoweka na nafasi yake kuchukuliwa na uwiano na amani.1

Kama pia tunavyowakuta baadhi ya wanafikra wasiokuwa wanadini waki- amini ulazima huu, kwa mfano mwanafikra mashuhuri wa kiingereza Bertrand Russell anasema: “Hakika ulimwengu unalingojea suluhisho litakaloukusanya chini ya bendera moja na tamko moja.”2

Na kauli yenye maana hii hii ameisema mfizikia maarufu Albert Einstein kwa kusema: “Hakika haiko mbali siku ambayo ulimwengu wote utatawaliwa na amani na usafi na watu kuwa katika hali ya kupendana na undugu.”3

Ama mwanafikra wa kiayalandi Bernard Shaw yeye katamka wazi mno na kwa undani kuliko uwazi na undani wa hawa wiwili, katika kutoa wasifu wa suluhisho na kuelezea ulazima wa umri wake kuwa mrefu kabla ya kudhihiri kwake amesema: “Hakika yeye ni mwanadamu hai mwenye mwili wenye afya bora na nguvu ya kiakili isiyokuwa ya kawaida. Ni mwanadamu wa hali ya juu kiasi kwamba mwanadamu huyu wa chini anamfikia baada ya juhudi za muda mrefu. Na hakika umri wake utarefu- ka mpaka avuke miaka mia tatu, na anaweza kunufaika na yale aliyoyaku- sanya ndani ya muda wote wa uhai wake mrefu.”4

Ama upande wa dini za kimungu zenyewe zimeashiria ulazima wa kudhi- hiri suluhisho la ulimwengu, na atakayefuatilia utabiri wa kimungu ndani ya vitabu vya biblia atavikuta vinaelekeza kwa huyu Mahdi ambaye ndiye anaaminiwa na madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.), kama ulivyothibitisha hilo uchambuzi mbalimbali unaohusu maelezo ya nukuu hizo za utabiri.5

Al-Qadhi As-Sabatwiy amezungumzia moja ya utabiri unaopatikana ndani ya kitabu cha Yoshua kutoka ndani ya Agano la kale ndani ya biblia unaoli- husu suluhisho la ulimwengu, akasema: "Maelezo haya yanamzungumzia Mahdi (a.s.)." Akaendelea mpaka akasema: "Shia Imamiyya wamesema: Yeye ndiye Muhammad bin Hasan Al-Askari ambaye alizaliwa mwaka mia mbili na hamsini na tano na mjakazi wa Hasani Al-Askari aitwaye Nargis huko Samrau zama za mtawala Al-Muutamid, kisha akaenda ghaibu muda wa mwaka mmoja6, kisha akadhihiri na kisha akaenda tena ghaibu na hiyo ndio ghaibu kubwa, na baada ya hapo harejei ila pindi Mwenyezi Mungu atakapotaka.

Na kwa kuwa kauli yao iko karibu mno na kile kinachozungumziwa na maelezo haya, na kwa kuwa lengo langu ni kuutetea umma wa Muhammad (s.a.w.w.) bila kujali upendeleo wa kimadhehebu ndio maana nimek- wambia kuwa lile wanalodai Shia Imamiyya ndilo lenye kuoana na maele- zo haya (ya agano la kale)."7

Pia Allamah Muhammad Ridha Fakhrul-Islam ambaye mwanzo alikuwa mkiristo kisha akawa mwislamu na kujiunga na madhehebu ya Ahlul-Bayti naye amefikia kwenye natija hii ambayo aliifikia As-Sabatwiy. Na ame- andika kitabu cha maarifa "*Anisul-Aalam*" akiwajibu mayahudi na wakris- to, na katika uchambuzi wake amezungumzia utabiri mbalimbali, na mwisho akahitimisha kuwa unaoana na Mahdi bin Hasan Al-Askari (a.s.).8

Hivyo anayechunguza kwa makini ndani ya maelezo hayo ya utabiri anakuta yanatoa wasifu wa suluhisho la ulimwengu usiyooana na mwingine asiyekuwa Mahdi mwenye kungojewa kwa mujibu wa imani ya kambi ya Ahlul-Bayt (a.s.). Hivyo asiyekubali imani hii hawezi kupata mfano halisi unaozungumziwa na utabiri huo, kama tunavyolishuhudia hilo kwenye kauli za wafafanuzi wa Injili wanapozungumzia msitari wa kwanza mpaka wa kumi na saba wa kitabu cha ufunuo wa Yohana sura ya kumi na mbili, wao wametamka wazi kuwa mtu anayezungumziwa na utabiri huu uliyomo ndani ya mistari hii bado hajazaliwa, na hivyo tafsiri yake ya uwazi na maana yake dhahiri imeachwa mpaka mbele na muda usiojulikana ambao ndani yake atadhihiri."9

Na kuna baadhi ya wanavyuoni wa kisunni wanaamini uchunguzi huo na natija hiyo, kwa mfano ustadhi Said Ayyub ameongoka kwa kusema kuwa mfano halisi unaozungumziwa na misitari iliyotangulia ya kitabu cha ufun- uo wa Yohana ni ule mfano halisi unaoaminiwa na kambi ya Ahlul-Bayt, akasema: "Imeandikwa ndani ya vitabu vya manabii kuwa Mahdi katika matendo yake hamna dosari." Kisha maelezo haya akayaongezea kwa kusema: "Nakiri hakika mimi nimeyakuta hivyo hivyo ndani ya vitabu vya watu wa kitabu, hakika watu wa kitabu wamefuatilia habari za Mahdi kama walivyofatilia habari za babu yake (s.a.w.w.), na hivyo habari za kitabu cha ufunuo wa Yohana zikaelekeza kwa mwanamke ambaye ndani ya mgongo wake kutatoka wanaume kumi na wawili." Kisha akaashiria mwanamke

mwingine, yaani ambaye atazaa mwanaume wa mwisho ambaye yeye ni kutoka kwenye mgongo wa babu yake. Kitabu kimesema: “Hakika mwanamke huyu atazingirwa na hatari, na alama ya hatari ni kwa jina la “At-Tanin” (joka kubwa). Na ikasema: “At-Tanin alisimama mbele ya mwanamke mwenye kujiandaa kujifungua ili ammeze mtoto pindi tu atakapojifungua.”10

Maana yake ni kuwa utawala ulikuwa unataka kumuua kijana huyu, lakini baada ya mtoto kuzaliwa; Barkel anasema ndani ya ufafanuzi wake kuwa: “Pindi hatari ilipomshambulia, Mwenyezi Mungu alimnyakua mwanawe na kumuhifadhi.” Na maelezo “Mwenyezi Mungu alimnyakua mwanawe.”11 Maana yake ni: “Hakika Mwenyezi Mungu alimpeleka ghaibu mtoto huyu.” Kama ilivyo ndani ya kauli ya Barkel: “Kitabu kime- sema kuwa: “Hakika ghaibu ya kijana itakuwa siku elfu moja na mia mbili na sitini.12” Nao ndio muda wake na alama yake kwa watu wa kitabu.”

Kisha Barkel akasema kuhusu kizazi cha mwanamke wa kwanza kwa ujumla: “Hakika At-Tanin atafanya vita kali pamoja na kizazi cha mwanamke, kama alivyosema ndani ya kitabu: “At-Tanin akamkasirikia mwanamke na akaenda kuweka vita pamoja na kizazi chake kingine, ambao wanahifadhi usia wa Mwenyezi Mungu.”13

Baada ya maelezo hayo yaliyotangulia, ustadh Abu Said Ayyub akasema: “Huu ndio wasifu wa Mahdi na ndio ule ule wasifu wake kwa Shia Imamiyya wafuasi wa Maimamu kumi na wawili.14

Na akaipa nguvu kauli yake kwa maelezo aliyoyaweka pambizoni yaki- husu uonaji wa wasifu wa Mahdi na Mahdi wa nyumba ya Mtukufu Mtume.15

Hivyo uchunguzi mwingi umesisitiza kuwa utabiri unamwashiria Mahdi Al-Muntadhir mwenyewe anayeaminiwa na madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.). Hebu sasa tuelekee kwenye riwaya za kambi ya Sunni ambazo zime- toka zikimzungumzia Imamu na kitambulisho chake, ili tuone je, zenyewe zimevuka kutoka kwenye anuani mpaka zikafika kuzungumzia utu wake baada ya riwaya za kudhihiri kwake kuwa nyingi mno, au ziliishia kwenye anuani tu?

Jibu ni: Inajulikana wazi kuwa anayeamini kudhihiri na ana yakini kabisa kuwa atatokea lakini hajapambanukiwa ni nani Mahdi aliyeahidiwa zama za mwisho, hatohesabiwa kuwa anamwamini Mahdi kama utakavyo Uislamu, kwa sababu anamwamini Mahdi kama anuani tu, lakini hamwamini mlengwa mwenyewe, ilihali kitendo cha kutofautisha kati ya kumwamini Imam mlengwa na kuamini kudhihiri kwake kinaharibu imani ya Mahdi, ni mfano wa imani ya mtu anayeamini wajibu wa Swala lakini yeye hajui nguzo zake.

Hivyo ili tufikie kumjua Imam Mahdi mwenyewe aliyelengwa na aliye hal- isi kwa kupitia riwaya za kisunni tutalazimika kuugawa uchambuzi katika mambo mbalimbali:

---

1. Buhuth Hawlal-Mahd cha As-Sayyid As-Shahid Muhammad Baqir As-Sadri: 87.
2. Al-Mahdi Al-Maw’uud wadaf ’ush-Shubhati An’hu cha As-Sayyid Abdur-Ridha As-Shuhrustaniy: 6.

3. Al-Mahdi Al-Maw'uud wadaf 'ush-Shubhati An'hu cha As-Sayyid Abdur-Ridha As-Shuhrustaniy: 6.
4. Bernadisho: Abbas Mahmuud Al-Uqad: 124 – 125.
5. Rejea kitabu Basharati Ahadayni cha Shaikh As-Sadiqiy, kimetafsiriwa kwa kiarabu kwa jina la "Al-Basharatu Wal-Muqaranatu".
6. Kilichothibiti ni kuwa ghaibu ya Imam Mahdi baada ya kifo cha baba yake ilien-
delea mpaka mwaka wa 69 A.H.
7. Al-Barahin As-Sabtwiyyah: Imenukuliwa kutoka kwenye kitabu Kashful-Astar
cha Al-Mirza An-Nuriyyu: 84.
8. Basharati Ahadayni cha Muhammad As-Sadiqiy: 232.
9. Basharati Ahadayni cha Muhammad As-Sadiqiy: 232.
10. Ufunuo wa Yohana 12: 3.
11. Ufunuo wa Yohana 12: 5.
12. Muda wake umepatikana ndani ya kiebrania kwa kusema: "Atakwenda ghaibu
dhidi ya At-Tanin zama moja, zama mbili na nusu zama." Rejea Basharati Al- Ahadayn: 263.
13. Ufunuo wa Yohana 12: 13.
14. Al-Masih Ad-Dajjal: Said Ayyub 379 – 380 imenukuliwa kutoka kwenye Al- Mahdi Al-Muntadhar Fil-Fikri Al-Islamiy: Imetolewa na Markazi Ar-Risalah: 13 – 14.
15. Rejea Al-Imam Al-Mahdi Dhimnu Silsilatu Aalamul-Hidayah cha Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul-Bayt: 9 – 24.

Jambo La Kwanza: Wanavyuoni wa madhehebu ya Sunni wamekiri kuwa Imam Mahdi (a.s.) ameshazaliwa

Kuna matamko mengi ya kukiri kuwa Imam Mahdi (a.s.) ameshazaliwa ambayo Sunni wameyasajili kwa kalamu zao. Na baadhi wamefanya kazi ya kuchunguza kukiri huku katika uchambuzi hasa unaojitegemea, hivyo uchunguzi huu ulikuwa unafuatana zama kwa zama kiasi kwamba haishindikani mwenye kukiri sasa kuhusu kuzaliwa kwa Mahdi kukutana na aliyekiri zama zilizotangulia, na hilo ni kuanzia zama za ghaibu fupi ya Imam Mahdi (a.s.) (260 – 329 A.H.) Na mpaka zama zetu hizi.

Sisi tutafupisha kwa kuwataja baadhi yao, ama atakayetaka kwa urefu na upana ni juu yake kurejea uchunguzi uliotangulia kuhusu kukiri huko,1 na hao baadhi ni:

1. Ibnul-Athir Al-Jazariy Izud-Din aliyefariki mwaka 360 A.H. Amesema ndani ya kitabu chake *Al-Kamil fit-Tarikh* kwenye mlango wa matukio ya mwaka 260 A.H. kuwa: "Ndani ya mwaka huo alifariki Abu Muhammad Al-Alawi Al-Askari, naye ni mmoja wa Maimamu kumi na wawili wa madhahebu ya Imamiyya, na yeye ndiye mzazi wa Muhammad ambaye wanamwamini kuwa ndiye anayengojewa."2

2. Ibnu Khallakan aliyefariki mwaka 681 A.H. Amesema ndani ya kitabu *Wafayatul-Aayan*: "Abu Qasim

Muhammad bin Hasan Al-Askari bin Ali Al-Hadiy bin Muhammad Al-Jawwad aliyetajwa kabla ni Imam wa kumi na mbili kwa mujibu wa imani ya Shia Imamiyya maarufu kwa sifa ya Hujah….mazazi yake yalikuwa siku ya Ijumaa nusu ya Shabani mwaka mia mbili hamsini na tano." Kisha akanukuu kutoka kwa mwanahistoria Ar-Rahalah Ibnul-Azraqu Al-Fariqiy aliyefariki mwaka 577 A.H. kuwa amesema ndani ya kitabu *Tarikh Mayyafariqina* kuwa: "Hakika Hujjah aliyetajwa amezaliwa Mfunguo sita mwaka mia mbili hamsini na nane, na imesemekana kuwa ni mwezi nane Shabani mwaka hamsini na sita, na ndio kauli sahihi mno."3

Nasema: Kauli sahihi kuhusu siku ya kuzaliwa kwake (a.s.) ni ile aliyoise- ma mwanzo Ibnu Khallakan, nayo ni siku ya ijumaa nusu ya mwezi wa Shaban mwaka mia mbili hamsini na tano, kauli hiyo wameafikiana Shia wote. Wametoa riwaya nyingi sahihi kuhusu hilo huku wanavyuoni wao waliotangulia wakithibitisha hilo, hakika Sheikh Al-Kulayni aliyeishi zama za ghaibu ndogo ameitoa tarehe hii kwa ukamilifu, kutoa kulikosal- imika na akaitanguliza kabla ya riwaya zinazoikhalifu tarehe hiyo. Amesema kwenye mlango unaohusu kuzaliwa kwake (a.s.): "Amezaliwa (a.s.) nusu ya Shaban mwaka mia mbili hamsini na tano."4

As-Saduq aliyefariki mwaka 381 A.H. Amepokea kutoka kwa Sheikh wake Muhammad bin Muhammad bin Iswam Al-Kulayniy kutoka kwa Muhammad bin Yaqub Al-Kulayniy kutoka kwa Ali bin Muhammad bin Bandari amesema: "Imam wa zama hizi (a.s.) alizaliwa nusu ya Shaban mwaka mia mbili hamsini na tano."5 Na Al-Kulayniy hajanasibisha kauli yake kwa Ali bin Muhammad kwa sababu ya umashuhuri wake na kuwe- po itifaki juu yake.

3. Ad-Dhahabiy aliyefariki mwaka 747 A.H. Amekiri ndani ya vitabu vyake vitatu kuwa Mahdi (a.s.) ameshazaliwa, na hatujafuatilia vitabu vyake vingine. Amesema ndani ya kitabu chake *Al-Ibaru*: "Na ndani ya mwaka huo (yaani ndani ya mwaka 256 A.H.) alizaliwa Muhammad bin Hasan bin Ali Al-Had bin Muhammad Al-Jawwad bin Ali Ar-Ridha bin Musa Al-Kadhim bin Jafar As-Sadiq Al-Alawi Al-Husayniy, Abu Qasim ambaye Shia walimpa lakabu ya Al-Khalafu Al-Hujjah, wakampa pia lak- abu ya Al-Mahdi na Al-Mantadhar, na wakampa lakabu ya Sahibuz-Zaman na yeye ndiye hitimisho la Maimamu kumi na wawili."6

Na amesema kwenye kitabu *Tarikh Duwalil-Islam* katika wasifu wa Hasan Al-Askari kuwa: "Hasan bin Ali bin Muhammad bin Ali Ar-Ridha bin Musa bin Jafar As-Sadiq, Abu Muhammad Al-Hashimiy Al-Husayniy ni mmoja wa Maimamu ambao Shia wanadai utakaso wao, na huitwa Hasani Al-Askari kwa kuwa aliishi Samrau, kwani eneo hilo huitwa Al-Askari, na yeye ndiye mzazi wa yule anayengojewa na Shia. Alifariki huko Samrau mwezi nane mfunguo sita mwaka mia mbili na sitini na akazikwa ubavuni mwa mzazi wake.

Ama mwanaye Muhammad bin Hasan ambaye Shia wanamwita Al-Qaim Al-Khalafu Al-Hujjah yeye alizaliwa mwaka wa hamsini na nane, na inase- mekana ni mwaka hamsini na sita."7

Na amesema ndani ya kitabu *Siru Aalamin-Nubalai*: "Sharifu Al- Muntadhar Abu Qasim Muhammad bin

Hasan Al–Askari bin Ali Al–Hadiy bin Muhammad Al–Jawwad bin Ali Ar–Ridha bin Musa Al–Kadhim bin Jafar As–Sadiq bin Muhammad Al–Baqir Ibnu Zaynul–Abidina Ali bin Husein As–Shahidu Ibnu Imam Ali bin Abi Talib Al–Alawi Al–Husayni ni hitimisho la mabwana kumi na wawili."[8]

Nasema: Kinachotuhusu sisi katika rai ya Ad–Dhahabiy kuhusu kuzaliwa kwa Mahdi tayari tumeshakifafanua. Ama kuhusu imani yake juu ya Mahdi ni kuwa yeye ni kama katika kauli zake zote nyingine bado alikuwa anan– gojea sirabi, kama tulivyoweka wazi hilo kuhusu mtu anayeamini kuwa Mahdi ni Muhammad bin Abdullah.

4. Ibnu Al–Wardiy aliyefariki mwaka 749 A.H. mwishoni mwa muhtasari ujulikanao kwa jina la *Tarikh Ibnul–Wardiy*: "Muhammad bin Hasan Al– Khalisu alizaliwa mwaka mia mbili hamsini na tano."[9]

5. Ahmad bin Hajar Al–Haythamiy Ash–Shafiy aliyefariki mwaka 974 A.H. amesema kwa maelezo haya ndani ya kitabu chake *As–Sawaiqul–Muhriqah* mwishoni mwa sura ya tatu ya mlango wa kumi na moja: "Abu Muhammad Hasan Al–Khalisu, na Ibnu Khallakani amemfanya huyu kuwa ndio Al–Askari, alizaliwa mwaka mia mbili thelathini na mbili.....alifia huko Samrau na alizikwa karibu na baba yake na ami yake akiwa na umri wa miaka ishirini na minane, na inasemekana kuwa alipewa sumu, na wala hakumwacha ila mwanae wa kiume Abu Qasim Al–Hujah, na alikuwa na umri wa miaka mitano baba yake alipofariki. Lakini Mwenyezi Mungu alimpa hekima na anaitwa Al–Qaim Al–Muntadhar. Imesemekena ni kwa kuwa alifichwa huko Madina na akatoweka na haikujulikana amekwenda wapi."[10]

6– As–Shabrawiy Ash–Shafiy aliyefariki mwaka 1171 A.H. ametamka wazi ndani ya kitabu chake *Al–Ittihafu* kuwa: "Imam Mahdi Muhammad bin Hasan Al–Askari (a.s.) amezaliwa usiku wa nusu ya Shaban mwaka mia mbili hamsini na tano hijiriya.[11]

7. Muumin bin Hasan As–Shablanjiy aliyefariki mwaka 1308 A.H. Ndani ya kitabu chake *Nurul–Absar* amekiri ndani ya maneno mengi kuwepo jina Imam Mahdi na nasaba yake tukufu toharifu, na kuniya yake na lakabu zake, mpaka akasema: "Na yeye ndiye Imam wa mwisho katika maimamu kumi na wawili kwa mujibu wa imani ya Shia Imamiyya."[12]

8'. Khayrud–Dini Az–Zarkiliy aliyefariki mwaka 1396 A.H. Amesema ndani ya kitabu chake *Al–Aalam* katika wasifu wa Imam Mahdi Al– Muntadhar: "Muhammad bin Hasan Al–Askari Al–Khalisu bin Ali Al–Hadiy Abu Qasim, Imam wa mwisho kati ya maimamu kumi na mbili wa Shia Imamiyya....alizaliwa Samrau na baba yake alifariki yeye akiwa na umri wa miaka mitano....Na katika tarehe ya kuzaliwa kwake inasemekana kuwa ni nusu ya Shaban mwaka mia mbili hamsini na tano, na katika tare– he ya kwenda ghaibu ni mwaka mia mbili sitini hijiriya."[13]

Nasema: Tarehe ya kuanza ghaibu ndogo ni mia mbili na sitini hijiriya, hiyo ni kwa itifaki ya Shia wote pamoja na wengine walioandika kuhusu ghaibu ndogo katika vitabu tulivyoviona, na huenda tarehe iliyomo ndani ya kitabu *Al–Aalam* inatokana na makosa ya chapa, kwa sababu Az– Zarkiliy hajaandika tarehe ya ghaibu kwa herufi bali kaandika kwa tarakimu, na hivyo uwezekano wa kuwepo makosa katika kuchapa tarakimu ni jambo rahisi mno. Na kuna matamko mengine mengi ya kukiri ambayo uchambuzi

hauturuhusu kuyanukuu.[14]

---

1. Rejea kitabu Al-Iman As-Sahih cha As-Sayyid Al-Qazwiniy. Kitabu Al-Imam Al-Mahdi fi Nahjul-Balagha cha Sheikh Mahdi Faqih Imaniy. Kitabu Man huwa Imamul-Mahdi cha At-Tabriziy. Kitabu Ilzamun-Naswib cha Sheikh Ali Al-Yazdiy Al-Hairiy. Kitabu Al-Imam Al-Mahdi cha ustadhi Ali Muhammad Dakhil. Kitabu Difau Anil-Kafiy cha As-Sayyid Thamir Al-Umaydiy. Ndani ya hiki cha mwisho wametajwa watu mia moja na ishirini na nane kutoka Sunni ambao wamekiri kuwa Imam Mahdi (a.s.) ameshazaliwa huku akiwapanga kulingana na karne zao, hivyo wa kwanza wao alikuwa ni Abubakri Muhammad bin Harun Ar-Riwayaniy ndani ya kitabu chake Al-Musnad aliyefariki mwaka 307 A.H. Na wa mwisho wao alikuwa ni ustadhi wa zama zetu Yunus Ahmad As-Samirai ndani ya kitabu chake Samirau fi Adabul-Qurni At-Thalithu Al-Hijiriy, kilichochapwa kwa msaada wa chuo kikuu cha Baghdadi mwaka 1968 A.D. Tazama Difau Anil-Kafiy 1: 568 – 592 chini ya anwani: Dalili ya sita: Matamko ya kukiri kwa Sunni.
2. Al-Kamil fit-Tarikh 7: 274 mwishoni mwa matukio ya mwaka 260 A.H.
3. Wafayatul-Aayan 4: 176, 562.
4. Usulul-Kafiy 1: 514, mlango wa 125.
5. Kamalud-Dini 2: 430, mlango wa 42.
6. Al-Ibaru fi Khabari Man Ghabara 3: 31.
7. Tarikhul-Islam: Juzuu ya kumi na tisa, kwenye matukio na vifo (251 – 260 A.H.): 113.
8. Siru Aalamin-Nubalai 13: 119, wasifu namba 60.
9. Nurul-Absar: 186. Hatujapata ndani ya Tarikh Ibnu Al-Wardiy ndani ya mwaka uliyotajwa, hatujui je, maelezo yaliondolewa?!!!
10. As-Sawaiq Al-Muhriqah cha Ibnu Hajar Al-Haythamiy, chapa ya kwanza: 207 na chapa ya pili: 124 na chapa ya tatu: 313 – 314.
11. Al-Ittihafu Bihubil-Ashrafi: 68.
12. Nurul-Absar: 186.
13. Al-A'alam 6: 80.
14. Rejea Al-Mahdi Al-Muntadhar fil-Fikri Al-Islamiy, kilichotolewa na Markazur-Risalah: 123 – 127.

Jambo La Pili: Jina la Imam ni lipi, na nasaba yake ni ipi?

Mwenye kufuatilia Hadithi sahihi zilizopatikana kuhusu jina na nasaba ya Mahdi ndani ya vitabu vya Sunni atazikuta nyingi mno zikisisitiza uhalisia mmoja nao ni: Nasaba ya Mahdi inarejea kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na kuwa yeye ni miongoni mwa Ahlul-Bait na miongoni mwa maimamu kumi na wawili walio watakasifu, na yeye ndiye wa mwisho wao. Naye ni Muhammad bin Hasan Al-Askari (a.s.) Ibnu Ali Al- Hadi bin Muhammad Al-Jawad bin Ali Ar-Ridha bin Musa Al-Kadhim bin Jafar As-Sadiq bin Muhammad Al-Baqir bin Ali As-Sajjad bin Husein As- Shahid wa Karbala bin Ali bin Abi Talib (a.s.).

Na ndiyo mwenye lakabu ya Al-Mahdi Al-Muntadhar anayeoana na ile imani ya Shia Imamiyya.

Zifuatazo ni riwaya zinazozungumzia jina lake na nasaba yake:

Mahdi ni: Mkinana, Mkurayshi na Hashimia

Imepokewa kutoka kwa Qatadah amesema: “Nilimwambia Said bin Al- Musayyab: Mahdi ni haki? Akasema: ‘Ndio ni haki.’ Nikamwambia: Anatokana na nani yeye? Akasema: ‘Anatokana na Kinana.’ Nikasema: Kisha kutoka kwa nani? Akasema: ‘Kutoka kwa Kurayshi.’ Nikasema: Kisha kutoka kwa nani? Akasema: ‘Kutoka kwa wana wa Hashim.”1

Hivyo kwa mujibu wa riwaya hii Mahdi ni mkinana, mkurayshi na muhashimia, na wala hakuna mgongano katika lakabu hizi, kwa sababu kila muhashimia anatokana na mkurayshi na kila mkurayshi anatokana na mkinana, kwa sababu Kurayshi ni An-Nadhar bin Kinanah, kwa itifaki ya wasomi wote wa nasaba za watu.

Mahdi ni kutoka kwa watoto wa Abdul-Muttalib

Ibnu Majah amepokea kutoka kwa Anas bin Malik amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: “Sisi ni kizazi cha Abdul-Mutwalib mabwana wa watu wa Peponi, mimi, Hamza, Ali, Jafar, Hasan, Husein na Mahdi.”2 Kwa mujibu wa riwaya hii Mahdi anakuwa miongoni mwa watoto wa Abdul-Mutwalib.

Mahdi ni kutoka kizazi cha Abu Talib

Imepokewa kutoka kwa Saif bin Umayrah amesema: Nilikuwa kwa Abu Jafar Al-Mansur akaanza kuniambia: “Ewe Saif bin Umayrah! Ni lazima atapatikana mwenye kunadi tokea mbinguni kwa jina la mtu kutoka kizazi cha Abu Talib.”

Nikamwambia: Ewe kiongozi wa waumini! Mimi ni fidia kwako; hii ni riwaya? Akasema: “Ndiyo, naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake, hakika nimeisikia kwa masikio yangu mawili.”

Nikamwambia: Ewe kiongozi wa waumini! Hakika Hadithi hii sijaisikia kabla ya muda huu. Akasema: “Ewe Saif! Hakika yenyewe ni kweli, na iki- tokea basi mimi nitakuwa wa kwanza kumkubali, kwani hakika wito ni kuelekea kwa mtu kutoka wana wa ami yetu.”

Nikamwambia: Ni mtu kutoka kizazi cha Fatima? Akasema: “Ndiyo ewe Saif, laiti nisingeisikia kutoka kwa Abu Jafar Muhammad bin Ali akiniha- dithia basi nisingeikubali kutoka kwa mtu yeyote hata kama wangenisimu- lia watu wote wa aridhini, lakini aliyenisimulia ni Muhammad bin Ali.”3

Na Hadithi hii inasisitiza kuwa Mahdi ni kutoka kizazi cha Abu Talib.

Mahdi ni kutoka Ahlul-Bayt (a.s.)

Imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-Khudri amesema: Mtume wa
Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: “Kiyama hakitosimama mpaka ardhi ijae dhuluma na uadui.” Akasema: “Kisha atokee mtu kutoka ndani ya kizazi changu au watu wa nyumba yangu atakayeijaza usawa na uadilifu kama ilivyojaa dhuluma na uadui.”4

Na mfano wake ni ile iliyotoka kwa Abdullah kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Kiyama hakitosimama mpaka aje mtu miongoni mwa watu wa nyumba yangu, jina lake linalingana na jina langu.”5

Imepokewa kutoka kwa Ali kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amese- ma: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): “Mahdi ni kutoka kwetu sisi Ahlul-Bayt, Mwenyezi Mungu atamleta ndani ya usiku mmoja.”6

Mahdi ni kutoka kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)

Kutoka kwa Ibnu Umar amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): “Zama za mwisho atatokea mtu kutoka kwenye kizazi changu, jina lake ni jina langu, kuniya yake ni kuniya yangu, ataijaza ardhi uadili- fu kama itakavyokuwa imejaa ujeuri, na huyo ndiye Mahdi.”7

Mahdi ni kutoka kizazi cha Fatima (a.s.)

1- Imepokewa kutoka kwa Ummu Salamah mke wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): “Mahdi ni kweli na yeye ni kutoka kizazi cha Fatima.”8

2- Kutoka kwa Ummu Salamah amesema: “Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akisema: “Mahdi ni kutoka ndani ya kizazi changu kutoka kwenye kizazi cha Fatima.”9

Mahdi ni kutoka kizazi cha Husein (a.s.)

Imepokewa kutoka kwa Hudhayfah bin Al-Yamani (r.a.) amesema: “Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alituhutubia, basi Mtume wa Mwenyezi Mungu akatutajia yatakayotokea, kisha akasema: “Hata kama dunia itabakiwa na siku moja, basi Mwenyezi Mungu ataire- fusha siku hiyo mpaka amlete mtu kutoka ndani ya kizazi changu, jina lake ni jina langu.”

Salman Al-Farsi (r.a.) akasema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni kutoka kwa mwanao yupi? Akasema: “Ni kutoka kwa huyu.” Akawa amempiga Husein (a.s.) kwa mkono wake.10

Imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-Khudri amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu aliugua ugonjwa

ambao ulimdhoofisha, basi Fatima (a.s.) akaingia kumtembelea na mimi nikiwa nimeketi kuliani kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.w.w.), basi alipoona udhaifu alio nao Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alianza kulia mpaka machozi yakafika mashavuni. Ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu akamwambia: “Ewe Fatima! Kitu gani chakuliza? Hivi hujui kuwa Mwenyezi Mungu aliitazama ardhi yote mara moja akamchagua baba yako kutoka humo na kumfanya nabii, kisha akaitazama mara ya pili akamchagua mume wako, ndipo akanifunulia na nikakuoza kwake na nikamfanya wasii. Hivi hujui kuwa wewe uko katika heshima ya Mwenyezi Mungu kwa kuwa baba yako alikuoza kwa mtu mwenye elimu mno zaidi yao, mvumilivu mno kuliko wao na wa kwanza wao kuukubali Uislamu.”

Ndipo Fatima akacheka na kufurahi. Mtume wa Mwenyezi Mungu akata- ka kumuongezea nyongeza ya kheri ambayo Mwenyezi Mungu aliigawa kwa Muhammad na kizazi cha Muhammad, akamwambia: “Ewe Fatima! Ali ana fadhila nane: Kumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hekima yake, mke wake, watoto wake Hasan na Husein, kuamrisha kwake mema na kukataza kwake maovu.

“Ewe Fatima! Sisi Ahlul-Bayt tumepewa vitu sita, ambavyo hajapewa yeyote vitu hivyo kati ya watu waliotangulia kabla yetu na wala hatovipa- ta yeyote atakayekuja baada yetu asiyekuwa Ahlul-Bayt: nabii wetu ndiye mbora wa manabii, naye ni baba yako. Wasii wetu ndiye mbora wa mawasii, naye ni mume wako. Shahidi wetu ndiye mbora wa mashahidi, naye ni Hamza ami ya baba yako. Na wajukuu wawili wa umma huu wana- toka kwetu, nao ni wanao wawili.

“Na Mahdi wa umma huu ambaye Isa ataswali nyuma yake anatoka kwetu.” Kisha akapiga mkono wake juu ya bega la Husein (a.s.) na kuse- ma: “Mahdi wa umma huu atatoka kwa huyu.”11

Jina la mzazi wa kike wa Mahdi na kuwa Mahdi ni kutoka kizazi cha As-Sadiq (a.s.)

Imepokewa kutoka kwa mfafanuzi wa lugha ajulikanaye kwa jina la Ibnul-Khashabu, amesema: Alinisimulia Abu Qasim At-Tahir bin Harun bin Musa Al-Kadhim kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake, amesema: Bwana wangu Jafar bin Muhammad alisema: “Mrithi mwema ni kutoka kizazi changu naye ni Mahdi, jina lake ni Muhammad na kuniya yake ni Abu Qasim, atatokea zama za mwisho, mama yake ataitwa Nargis na juu ya kichwa chake (a.s.) kutakuwa na wingu likimkinga na jua, litazunguka pamoja naye popote atakapokwenda huku likinadi kwa sauti fasaha huyu ndiye Mahdi mfuateni.”12

Mahdi ni kutoka kizazi cha Ar-Ridha (a.s.)

Imepokewa kutoka kwa Hasan bin Khalid, amesema: Ali bin Musa Ar- Ridhaa alisema: “Hana dini asiyekuwa na ujidhibiti, na hakika mbora wenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni mcha Mungu kuliko nyinyi.” Kisha akase- ma: “Hakika mtu wa nne kutoka katika kizazi changu ni mwana wa bibi wa watumwa, kupitia yeye Mwenyezi Mungu atatoharisha ardhi dhidi ya kila ujeuri na dhuluma….”13

Jina la mzazi wa kiume wa Imam Mahdi (a.s.)

Ar-Riwayyaniy na At-Tabaraniy na wengineo wametoa: “Mahdi ni kutoka kizazi changu, uso wake ni kama nyota ing’aayo, rangi yake ni rangi ya kiarabu, na kiwiliwili cha kiisraeli – yaani mrefu – ataijaza ardhi uadilifu kama itakavyokuwa imejaa dhulma. Watu wa mbinguni na ardhini watarid- hia ukhalifa wake.”

Pia katika kitabu chake *Al-Hilyatu* imepatikana: “Yeye ni kijana mwenye macho yenye wanja, mwenye nyusi laini zilizolala kwa urefu, mwenye pua nyembamba yenye mwinuko, mwenye ndevu fupi zilizosokotana, na juu ya shavu lake la kulia kuna weusi.”

Sheikh Al-Qutub Al-Ghawthiy Sayyidiy Muhyid-Din Ibnul-Arabiy amese- ma ndani ya kitabu *Al-Futuhati*: “Fahamuni kuwa ni lazima atatokeza Mahdi, lakini hatoki mpaka ardhi ijae ukatili na dhuluma na ndipo aje kui- jaza uadilifu na usawa, na yeye ni kutoka kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kutoka kizazi cha Fatima Mola awe radhi naye, babu yake ni Husein bin Ali bin Abu Talib na mzazi wake wa kiume ni Hasan Al-Askari mwana wa Imam Ali An-Naqiy mwana wa Imam Muhammad At-Taqiy mwana wa Imam Ali Ar-Ridhaa mwana wa Imam Musa Al- Kadhim mwana wa Imam Ja’far As-Sadiq mwana wa Imam Muhammad Al-Baqir mwana wa Imam Zaynul-Abidina mwana wa Imam Husein mwana wa Imam Ali bin Abu Talib, Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote.

“Jina lake linaoana na jina la Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), waislamu watampa kiapo cha utii eneo la kati ya Ruknu na Maqam. Anafanana na Mtume wa Mwenyezi Mungu katika maumbile na anakarib- iana naye katika maadili, watu wema kupitia yeye ni watu wa Kufa, ata- gawa mali kwa usawa, atafanya uadilifu kwa raia na maisha bora yatakuwa mikononi mwake.”14

---

1. Uqadud-Durari: 42 – 44, mlango wa kwanza. Mustadrak Al-Hakim 4: 553. Maj’mauz

2. Sunanu Ibnu Majah 2: 1368, Hadithi ya 4087, mlango wa kutokeza kwa Mahdi.
Mustadrak Al-Hakim 3: 211. Maj’maul-Jawamiu cha As-Suyuti 1: 851.

3. Uqadu Ad-Durar cha Al-Muqaddasiy As-Shafiiy: 149 – 150, mlango wa nne.

4. Musnad Ahmad 3: 424, Hadithi ya 10920. Musnad Abu Yaala 2: 274, Hadithi ya 987. Al- Mustadrak 4: 577. Uqadu Ad-Durar: 36, mlango wa 1. Mawaridu Ad-Dham’ani: 464, Hadithi ya 1879 na 1880. Muqadimah cha Ibnu Khalduni: 250, sura ya 53. Jam’ul-Jawamiu
1: 902. Kanzul-ummal 14: 271, Hadithi 38691. Yanabiul-Mawaddah 433, mlango wa 73.

5. Musnadul-Bazzaz 1: 281. Musnad Ahmad: 3761. Sunan At-Tirmidhiy 4: 505, mlango wa
52, Hadithi ya 2230. Al-Muujam Al-Kabir 10: 135, Hadithi ya 10221 ikiwa na tofauti kido- go. Tarikh Baghdad 4: 388. Uqad Ad-Durar: 38, mlango wa 3. Matwalibu As-Suul 2: 81. Al-Bayan fi Akhbari Swahibuz-Zaman cha Muhammad An-Nawfaliy Al-Qurayshiy Al- Kunjiy As-Shafiiy: 91. Faraidu As-Samtwayn 2: 327, Hadithi ya 576. Ad-Durul-Manthur 6:58. Jam’ul-Jawamiu 1:903. Kanzul-ummal 14: 271, Hadithi ya 38692. Burhanul-Muttaqiy: 90, mlango wa 2, Hadithi ya 4.

6. Ibnu Abu Shayba 8: 678, Hadithi 190. Futunu Ibnu Hammad. Musnad Ahmad 1: 84. Tarikh Al-Bukhari 1: 371, Hadithi ya 994. Sunan Ibnu Majah 2: 1367, mlango wa 34, Hadithi ya 4085. Musnad Abu Yaala 1: 359, Hadithi ya 465. Hilyatul-Awliyai 3: 177. Al- Kamil cha Ibnu Adiy 7: 2643. Al-Firdawsu 4: 222, Hadithi ya 6619. Al-Bayani fi Akhbari Swahibuz-Zaman cha Al-Kunjiy As-Shafiiy: 100. Uqadu Ad-Durar: 183, mlango wa 6. Al- Ilalu Al-Mutanahiyah 2: 2856, Hadithi ya 1432. Faraidu

As-Samtwayni 2: 331, Hadithi ya 583. Mizanul-Iitidal 4: 359, Hadithi ya 9444. Muqadimah Ibnu Khalduni 1: 396, mlango 53. Tahdhibu At-Tahdhibu 11: 152, Hadithi ya 294. Urufus-Suyutiy Al-Hawiy 2: 213. Ad- Durul-Manthur 6: 58. Jam'ul-Jawamiu 1: 449. Al-Jamiu As-Saghir 2: 672, Hadithi ya 9243. As-Sawaiq cha Ibnu Hajar: 163, mlango wa 511, sura ya 1. Kanzul-ummal 14: 264, Hadithi ya 38664. Burhanul-Muttaqiy: 87, mlango wa 1, Hadithi ya 43, na ukurasa wa 89, mlango wa 2, Hadithi ya 1. Mirqatul-Mafatihi 9: 349 humo mna tofauti kidogo. Faydhul-Qadir 6: 278, Hadithi ya 9243.

7. Tadhkiratul-Khawwas: 363, Uqadu Ad-Durar: 43, mlango wa 1. Minihajus- Sunnah cha Ibnu Taymiyah 4: 86 – 87.

8. Tarikh Bukhari 3: 364. Al-Muujam Al-Kabir 23: 267, Hadithi ya 566. Mustadak Al-Hakim 4: 557.

9. Sunan Abu Dawdi 4: 104, Hadithi ya 4284. Sunan Ibnu Majah 2: 1368, mlan- go wa 34, Hadithi ya 4086. Al-Firdawsu 4: 497, Hadithi ya 6943. Maswabihul- Baghawi 3: 492, mlango wa 3, Hadithi ya 4211. Jamiul-Usul 5: 343. Matwalibu As-Suul: 8. Uqadu Ad-Durar: 36, mlango wa 1. Mizanul-Iiitidal 2: 87. Mishkatul- Maswabihi 3: 24, sura ya 2, Hadithi ya 5453. Tuhfatul-Ashraf 13: 7, Hadithi ya 18153. Al-Jamiu As-Saghir 2: 672, Hadithi ya 9241. Ad-Durul-Manthur 6: 57. Jam'ul-Jawamiu 1: 449. As-Swawaiq cha Ibnu Hajar: 141, mlango wa 11, sura ya 1. Kanzul-ummal 14: 264, Hadithi ya 38662. Mirqatul-Mafatihi 9: 350. Is'afur- Raghibina: 145. Faydhul-Qadir 6: 277, Hadithi ya 9241. At-Taju Al-Jamiu Lil- Usul 5: 343.

10. Al-Manaru Al-Munifu cha Ibnul-Qayyim: 148, 329, sura ya 50, kutoka kwa At- Tabaraniy ndani ya kitabu Al-Awsatu. Uqadu Ad-Durar: 45, mlango wa kwanza, humo mna: "Ameitoa Al-Hafidhu Abu Nua'im katika sifa ya Mahdi.". Dhakhairul-Uqba cha Al-Muhibu At-Tabari: 136, humo mna: "Maelezo yasiyoainishi yanatafsiriwa na haya yaliyoainishi." Faraidu As-Samtwayni 2: 325, 575, mlango wa 61. Al-Qawlu Al-Mukhtasar cha Ibnu Hajar 7: 37, mlango wa 1. Faraidu Fawaidul-Fikri: 2, mlango wa 1. As-Siratul-Halbiyah 1: 193. Yanabiul- Mawaddah 3: 63, mlango wa 94. Na kuna Hadithi nyingine zenye kuelezea sifa hizi mahususi ndani ya kitabu Maqtalul-Imam Al-Husayn cha Al-Khawarazamiy Al-Hanafiy 1: 196. Faraidu As-Samtwayn 2: 310 – 315, Hadithi za 561 – 569. Yanabiul-Mawadah 3: 170: 212, mlango wa 93 na mlango wa 94.

11. Al-Bayanu: 120, mlango 9. Al-Fusulul-Muhimmah: 286, chapa ya Darul- Adh'wai, sura ya 12. Yanabiul-Mawadah: 490 na 493, mlango wa 94, japokuwa kuna tofauti kidogo.

12. Yanabiul-Mawaddah: 491 kutoka kwenye kitabu Al-Arbauni cha Al-Hafidhu Abu Naim Al-Isbihaniy.

13. Yanabiul-Mawaddah: 448 na 489, imenukuliwa kutoka kitabu Faraidu As- Samtwayni.

14. Mashariqul-An'wari Fifawzi Ahlil-Iitibar cha Sheikh Hasan Al-Adawi Al- Hamzawiy Al-Misriy: 476 – 477, sura inayohusu Mahdi. Yawaqitul-Jawahir 562, mlango unaohusu alama zote za Kiyama, imenukuliwa kutoka kwenye kitabu Al-

Jambo La Tatu: Sifa za Imam Mahdi

Baada ya kubainika jina la Imam Mahdi na nasaba yake, basi katika jambo hili tutazungumzia riwaya zilizopatikana ndani ya vitabu vya Sunni zina- zohusu sifa za kimaumbile za Imam (a.s), kuanzia sifa ya uso, rangi yake, nywele na mfano wa hayo. Tutabainisha hayo ndani ya riwaya mbalimbali.

1- Imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-Khudri, kutoka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kuwa alisema: "Mahdi wa kutoka kwangu ni mwenye paji bapa na pua nyembamba yenye mwinuko, ataijaza ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa ukatili na dhuluma..."1

2 - Imepokewa kutoka kwa Hudhayfa amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: "Mahdi ni mtu kutoka ndani ya kizazi changu, uso wake ni kama mwezi ung'aao, rangi yake ni rangi ya kiarabu, kiwili- wili chake ni kiwiliwili cha kiisraeli, ataijaza ardhi uadilifu, kama itakavyokuwa imejaa

dhulma. Wataridhia ukhalifa wake watu wa mbingu- ni na aridhini na ndege wa angani...." 2

3- Imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-Khudri kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kuwa alisema: "Mahdi ni kutoka kwetu Ahlul-Bayt, ni mwenye pua nyembamba yenye mwinuko ulionyooka, mwenye paji bapa, ataijaza ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa ukatili na dhuluma. Ataishi hivi." Akawa amefungua mkono wake wa kushoto na vidole viwili – kidolegumba na kidoleshahada – vya mkono wa kulia na akawa amefumba vitatu vilivyobaki.3

4- Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Al-Harthu amesema: "Mahdi ata- jitokeza akiwa na miaka arubaini kama mtu kutoka kizazi cha Israil."4

5- Imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Jubayri amesema: "Mahdi ni mwenye nyusi laini zilizolala kwa urefu, paji bapa na macho meusi mno, atakuja kutokea Hijazi na kutulia juu ya mimbari ya Damascus akiwa kijana wa miaka kumi na minane."5

6- Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Bashir kutoka kwa Kaab amese- ma: "Mahdi ni mnyenyekevu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama unyenyekevu wa mbawa za furukombe."6

7- Imepokewa kutoka kwa Ibnu Abbas amesema: "Mahdi ni kijana kutoka kwetu Ahlul-Bait."7

8- Imepokewa kutoka kwa Abdur-Rahmani bin Awfi kutoka kwa baba yake amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: "Hakika Mwenyezi Mungu atamleta mtu kutoka ndani ya kizazi changu, ana mwanya na paji bapa, ataijaza ardhi usawa na uadilifu na ataimwagia mali nyingi."8

9- Imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Ja'far kutoka kwa Ali bin Abu Talib (a.s.) amesema: "Hakika mwana wa huyu ni bwana kama alivy- omwita Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na Mwenyezi Mungu ata- toa kwenye mgongo wake mtu mwenye jina la nabii wenu, anafanana naye kwa maumbile na tabia, atatoka wakati ambao watu watakuwa katika mghafala, wakiifisha haki na kudhihirisha dhulma. Wallahi laiti angekuwa hatokei basi ningemkata shingo yake. Kwa kutokeza kwake watafurahia watu wa mbinguni na wakazi wake, na yeye ni mtu mwenye paji bapa, pua nyembemba yenye mwinuko, tumbo pana, mwenye matege huku paja lake la kulia likiwa na weusi na ni mwenye mwanya, ataijaza ardhi uadilifu kama itakavyokuwa imejaa dhuluma na ukatili."9

10- Imepokewa kutoka kwa Sulayman bin Habib amesema: "Nilimsikia Abu Umamah Al-Bahiliy akisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: "Kati yenu na Rum kutakuwa na vituo vinne vya kupumzika kwa siku, cha nne atakifungua mikononi mwa mtu kutoka jamaa wa mteule na atadumu miaka saba." Basi mtu mmoja kutoka ukoo wa Abdul-Qaysi aliyekuwa akiitwa Al-Mustawradu bin Ghaylan aka- muuliza: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nani atakuwa Imam wa watu zama hizo? Akasema: "Mahdi kutoka ndani ya kizazi changu, mwenye miaka arubaini, uso wake kama nyota ing'aayo huku kwenye shavu lake la kulia kukiwa na weusi...."10

11- Imepokewa kutoka kwa Al-Haytham bin Abdur-Rahman kutoka kwa Ali bin Abu Talib (a.s.)

amesema: “Mahdi sehemu ya kuzaliwa kwake ni Madina, ni kutoka Ahlul-Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), jina lake ni jina la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), eneo atakalohamia ni Baytul-Maqdas, ana ndevu za msokotano, mwenye macho ya wanja, meno yake ya mbele ni yenye kung’aa, usoni mwake ana weusi, mwenye pua nyembamba yenye mwinuko, mwenye paji bapa, begani kwake kuna alama ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). bendera yake inatokana na kitambaa kisichoshonwa yenye utande wa nyuzinyuzi, ni nyeusi ya pembe nne na imekunjwakun- jwa, haijapepea tangu afariki Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na haitopeperush- wa mpaka atokeze Mahdi (a.s.). Mwenyezi Mungu atampa msaada kwa Malaika elfu tatu watakaowapiga mbele na nyuma wale waliowakhalifu.”11

---

1. Sunan Abi Dawdi 4: 107, Hadithi ya 428. Mustadrak Al-Hakim 4: 557, japo ina tofauti kidogo. Maalimus-Sunan 4: 344. Maswabihul-Bahgawi 3: 492, Hadithi ya 4212. Al-Ilalu Al-Mutanahiyah 2: 859, Hadithi ya 1443. Jamiul-Usul 5: 343, mlango 7. Matalibus-Su’ul 2: 80, mlango wa 12. Al-Bayan: 117. Uqadu Ad-Durar: 59, mlango wa 3. Mishkatul-Maswabihi 3: 171, mlango wa 2, sura ya 2, Hadithi ya 5454. Al-Jamiu As-Swaghir 2: 672, Hadithi ya 9244. Jam’ul-Jawamiu 1: 449. Kanzul-ummal 14: 264, Hadithi ya 38665. Mirqatul-Mafatihu 9: 351, Hadithi ya 5454. Faydhul-Qadir 6: 278, Hadithi ya 9244. At-Taju Al-Jamiu Lil-Usul 5: 34, mlango wa 7.

2. Al-Firdawsu 4: 496, Hadithi ya 6940. Al-Ilalu Al-Mutanahiyah 2: 858, Hadithi ya 1439. Al-Bayan: 118, mlango wa 8. Dhakhairul-Uqba: 136. Uqadu Ad-Durar:
60, mlango wa 3, humo mna “Kama nyota ing’aayo.”. Mizanul-Iitidal 3: 449. Lisanul-Mizan 5: 24. Al-Fussul Al-Muhimmah: 284. Al-Jamiu As-Swaghir 2: 672, Hadithi ya 9245. As-Sawaiq cha Ibnu Hajar: 164, mlango wa 11, sura ya 1. Kanzul-ummal 14: 264, Hadithi ya 38666. Mirqatul-Mafatihi 9: 350. Lawaihus-Safawiniy 2: 4. Is’afur-Raghibina: 146. Nurul-Absar: 187. Faydhul-Qadir 6: 279, Hadithi ya 9245.

3. Mustadrak Al-Hakim 4: 558. Uqad Ad-Durar: 60, mlango wa 3, japo mna tofauti kidogo. Faraidu As-Samtwayni 2: 330, Hadithi ya 580. Burhanul-Muttaqiy: 98, mlango wa 2, Hadithi ya 28 na 99, mlango wa 3, Hadithi ya 3. Yanabiul-Mawaddah: 488, mlango wa 94.

4. Futunu Ibnu Hammad: 258, Hadithi ya 1008. Urufu As-Suyuti Al-Hawiy 2:232. Burhanul-Muttaqiy: 99, mlango wa 3, Hadithi ya 2. Kanzul-ummal 14: 586, Hadithi ya 39660.

5. Burhanul-Muttaqiy: 100, mlango wa 3, Hadithi ya 5. Uqadu Ad-Durar: 64, mlango wa 3. Urufus-Suyuti Al-Hawi 2: 232. Faraidu Fawaidul-Fikri: 4, mlango 2.

6. Ibnu Hammad: 258. Uqad Ad-Durar: 65, mlango wa 3. Urufus-Suyuti Al-Hawi 2: 232. Al-Qawlu Al-Mukhtasar: 98, mlango wa 3, Hadithi ya 29. Burhanul- Muttaqiy 101, mlango wa 3, Hadithi ya 10.

7. Ibnu Hammad: 102. Urufus-Suyuti Al-Hawi 2: 232. Burhanul-Muttaqiy 98,
mlango wa 2, Hadithi ya 26 na 27. Kanzul-ummal 14: 585, Hadithi ya 39658, japo kuna tofauti kidogo. Faraidu Fawaidul-Fikri: 2, mlango 1.

8. Al-Bayanu: 139, mlango wa 19. Uqadu Ad-Durar: 37, mlango wa 1. Faraidu As-Samtwayni 2: 331, Hadithi ya 582, japo mna tofauti kidogo. Urufus-Suyuti Al- Hawi 2: 220. As-Sawaiq cha Ibnu Hajar: 164, mlango wa 11, sura ya 1. Al-Qawlu Al-Mukhtasar: 43, mlango wa 1, Hadithi ya 33. Burhanul-Muttaqiy: 84, mlango wa 1, Hadithi ya 32. Is’afur-Raghibina: 146. Yanabiul-Mawaddah: 433, na 436, mlango wa73, sura ya 2. Faraidu Fawaidul-Fikri: 4, mlango 2.

9. Sunan Ibnu Dawdi 6: 162, Hadithi ya 4121. Uqadu Ad-Durar: 45, mlango wa 1. Futunu Ibnu Kathir 1: 38. Muqaddimatu Ibnu Khaliduni: 391, sura ya 53. Urufus-Suyuti Al-Hawi 2: 214. Ad-Durrul-Manthur 6: 39, mwishoni mwa Aya ya 8. Jam’ul-Jawamiu 2:35. Kanzul-ummal 13: 647, Hadithi ya 37636. Mirqatul- Mafatihu 9: 363, Hadithi ya 5462. Yanabiul-Mawaddah: 432, mlango wa72. At- Taju Al-Jamiu Lil-Usul 5: 343, Hadithi ya 10.

10. Al-Bayan: 137–138, mlango wa 18, kutoka kwenye Al-Muujam Al-Kabir na
Manaqib Al-Mahdawi cha Abu Nua’im.

11. Al-Bayan: 140, kutoka kwenye Al-Muujam Al-Kabir cha At-Tabaraniy na
Manaqib Al-Mahdawi cha Abu Nua’im.

Jambo La Nne: Nafasi ya Imam Mahdi (a.s.) mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu

Baada ya kuwa tumejua jina la Imam Mahdi na sifa zake, basi ndani ya kifungu hiki tutazungumzia hadhi ya kiroho aliyonayo Imam Mahdi na nafasi yake mbele ya Mola ambayo humsukuma kutekeleza jukumu lake, na kuwa yeye ni khalifa wa Mwenyezi Mungu tuliyeahidiwa, ambaye ni wajibu kumtii kwa amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Tutazungumzia hilo ndani ya riwaya mbalimbali.

1- Imepokewa kutoka kwa Anas bin Malik amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akisema: "Sisi kizazi cha Abdul-Muttalib ni mabwana wa watu wa Peponi, mimi Hamza, Ali, Ja'far, Hasan, Husein na Mahdi."1

2- Imepokewa kutoka kwa Ibnu Abbas kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Mahdi ni tausi wa watu wa Peponi."2

3- Imepokewa kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Umma huu utakuwa na khalifa, Abubakri na Umar si bora kuliko yeye."3

4- Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Umar amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Mahdi atatokeza huku juu ya kichwa chake kukiwa na wingu. Na kuna mnadi atakayenadi: Huyu ndiye Mahdi khalifa wa Mwenyezi Mungu mfuateni."4

5- Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Amru kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Atatokeza Mahdi huku juu ya kichwa chake kukiwa na Malaika akinadi: Hakika huyu ndiye Mahdi mfuateni."5

---

1. Sunan Ibnu Majah 2: 1368, mlango wa 34, Hadithi ya 4087. Mustadrak Al- Hakim 3: 211. Tarikh Baghdad 9: 434, Hadithi ya 5050. Matwalibus-Suul 2: 81, mlango wa 12. Al-Bayan: 101, mlango 3. Dhakhairul-Uqba: 15 na 89. Ar-Riyadh An-Nadhirah 3: 4 na 182, sura ya 8. Uqad Ad-Durar: 194, mlango wa 7. Faraidu As-Samtwayn 2: 32, mlango 7, Hadithi ya 380. Muqaddimati Ibnu Khalduni: 398, mlango wa 53. Al-Fusulu Al-Muhimmah: 284, chapa ya Darul-Adh'wai, sura ya 12. Jam'ul-Jawamiu 1: 851. As-Sawaiq cha Ibnu Hajar: 160, mlango wa 11, sura ya 1 na ukurasa wa 187, mlango wa 11, sura ya 2, Hadithi ya 19. Burhanul- Muttaqiy: 89, mlango wa 2, Hadithi ya 3. Is'afur-Raghibina: 124. Urufus-Suyutiy Al-Hawi 2: 214.

2. Al-Firdawsu 4: 222, Hadithi ya 6668. Al-Bayanu: 118, mlango wa 8. Uqad Ad- Durar: 199, mlango wa 7. Al-Fusul Al-Muhimmah: 284, sura ya 12. Burhanul- Muttaqiy: 171, mlango wa 12, Hadithi 2. Kunuzud-Daqaiq: 152. Nurul-Absar: 187. Yanabiul-Mawaddah: 181, mlango wa 56.

3. Ibnu Abi Shaybah 15: 198, Hadithi ya 19496. Al-Kamil cha Ibnu Adiy 6: 2433. Uqad Ad-Durar: 199, malngo wa 7. Burhanul-Muttaqiy: 172, mlango wa 12, Hadithi ya 6.

4. Al-Bayan: 132, mlango wa 15. Uqad Ad-Durar: 183, mlango wa 6. Faraidu As- Samtwayni 2: 316, mlango 61, Hadithi ya 566 – 569. Al-Fusul Al-Muhimmah: 298, sura ya 12. Urufus-Suyutiy Al-Hawi 2: 217. Tarikhul-Khamis 2: 288. Nurul-Absar:

5. Takhlisul–Mutashabihi 1: 417. Al–Bayan: 133, mlango wa 16. Faraidu As– Samtwayni 2: 316, mlango 61, Hadithi ya 569. Urufus–Suyutiy Al–Hawi 2: 217. Al– Qawlu Al–Mukhtasar: 39, mlango wa 1, Hadithi ya 24. Burhanul–Muttaqiy: 72, mlango wa 1, Hadithi ya 2. Yanabiul–Mawaddah: 447, mlango wa 78.

Jambo La Tano: Mahdi (a.s.) khalifa wa Mwenyezi Mungu na hitimisho la maimamu (a.s.)

Ikiwa Imam Mahdi tuliyeahidiwa ndiye Muhammad bin Hasan Al–Askari (a.s.), na nafasi yake kwa Mwenyezi Mungu ni khalifa wa haki ambaye ni lazima kumtii. Basi tunajiuliza: Je, kuna Imam mwingine atakuja baada yake? Au yeye ndiye khalifa wa mwisho kutoka Ahlul–Bayt (a.s.) na hitimisho lao, kama wanavyoamini Shia Imamiyya na kumngojea?

Riwaya zifuatazo ambazo ni kutoka kwenye vitabu vya Sunni zinazungumza kuwa Mahdi tuliyeahidiwa ndiye Imam wa mwisho na hitimisho la makhalifa (a.s.).

1– Kutoka kwa Thawbani amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Watatu watagombana kwenye hazina yenu wote wakigombania ukhalifa, kisha hakuna hata mmoja miongoni mwao atakayeupata, kisha zitatokeza bendera nyeusi upande wa Mashariki na kuwauwa mauaji yasiyowahi kufanywa na kaumu yoyote.” – kisha akase– ma jambo ambalo silikumbuki – Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: “Mkimuona basi mpeni kiapo cha utii angalau kwa kutambaa juu ya thelu–ji, kwani hakika yeye ni Mahdi khalifa wa Mwenyezi Mungu.”1

2– Imepokewa kutoka kwa Ali bin Abu Talib (a.s.) amesema: “Nilimwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mahdi ni kutoka kwetu sisi maimamu wa uongofu au ni kutoka kwa asiye sisi? Akasema: “Bali ni kutoka kwetu, dini inahitimishwa kupitia kwetu kama ilivyofun– guliwa kupitia kwetu, na kupitia kwetu wataokolewa dhidi ya upotovu wa fitina kama walivyookolewa dhidi ya upotovu wa shirki. Kupitia kwetu Mwenyezi Mungu ataunganisha kati ya nyoyo zao ndani ya dini baada ya uadui wa fitina kama alivyounganisha nyoyo zao na dini Yake baada ya uadui wa shirki.”2

3– Ibnu Hajar Al–Haythamiy aliyefariki mwaka 974 A.H. Amesema: “Abu Hasan Al–Abiriy amesema: Zimekuwa nyingi mno habari na zikazidi kwa uwingi wa wapokezi wake kutoka kwa Al–Mustafa (s.a.w.w.) kuhusu kutokeza kwake – Mahdi – na kuwa yeye ni kutoka ndani ya Ahlul–Bayt wake, na kuwa ataijaza ardhi uadilifu, na kuwa yeye atatoka pamoja na Isa (a.s.) na hivyo atamsaidia katika kumuuwa Dajjal huko kwenye mlango wa Ludi kwenye ardhi ya Palestina, na kuwa yeye atasalisha umma huu akiwa Imam na Isa ataswali nyuma yake.”3

4– Sheikh As–Swabbani aliyefariki mwaka 1206 A.H. Amesema: “Zimekuwa nyingi mno habari kutoka

kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu kutokeza kwake – Mahdi – na kuwa yeye ni kutoka ndani ya Ahlul- Bayt wake, na kuwa ataijaza ardhi uadilifu, na kuwa yeye atamsaidia Isa (a.s.) katika kumuuwa Dajjal huko kwenye mlango wa Ludi kwenye ardhi ya Palestina, na kuwa yeye atasalisha umma huu akiwa Imam na Isa atasali nyuma yake."4

5- Hadithi ya Abu Saidi Al-Khudri: "Ardhi itajaa ukatili na dhuluma, ndipo atatokeza mtu kutoka ndani ya kizazi changu..."5

---

1. Al-Bayan: 104, mlango wa 3. Sunan Ibnu Majah: 2 / 1367, Hadithi ya 4084. Al- Mustadrak: 4 / 463. Talkhisul-Mustadrak: 4 / 463 na 464. Musnad Ahmad bin Hanbal: 5 / 277, japo kuna tofauti kidogo.
2. Al-Muujamu Al-Awsatu 1: 136, Hadithi ya 157. Al-Bayan: 125, mlango wa 11. Uqadu Ad-Durar: 192, mlango wa 7. Majmauz-Zawaidi 7: 316 – 317. Muqaddimati Ibnu Khalduni: 396 na 397, mlango wa 53. Al-Fusul Al-Muhimmah: 288, japo kuna tofauti kidogo, sura ya 12. Urufus-Suyutiy Al-Hawi 2: 217. Jam'ul- Jawamiu 2: 67. As-Sawaiq cha Ibnu Hajar: 163, mlango wa 11, sura 1. Kanzul- ummal 14: 598, Hadithi ya 39682. Burhanul-Muttaqiy: 91, mlango wa 2, Hadithi ya 7 na 8. Faraidu Fawaidul-Fikri: 3, mlango 1. Nurul-Absar: 188.
3. As-Sawaiq Al-Muhriqah cha Ibnu Hajar: 165, chapa ya Misri.
4. Is'afur-Raghibina cha As-Swaban: 140.
5. Mustadrak Al-Hakim 4: 558.

Jambo La Sita: Mahdi (a.s.) atamswalisha Nabii Isa (a.s.)

Ikiwa dalili za nukuu zilizomo ndani ya *Sahih Sita* na vitabu vingine zina- sisitiza ukweli wa Imam Mahdi, kuanzia utu wake, jina lake, nasaba yake hadi sifa zake nyingine, hivi je, muislamu wa zama atakazodhihiri ame- ongezewa alama nyingine zitakazoimarisha imani yake kwake na utiifu kwa huyu mtu aliye Imam mwenyewe, na kumwepusha na mafuriko nyuma ya madai na mkondo wa upotovu?

Hakika riwaya zifuatazo zinasisitiza ukweli huu wa kihistoria nao ni kuwa, Nabii Isa (a.s.) atateremka kutoka mbinguni na kusali nyuma ya Imam Mahdi mwana wa Hasan Al-Askari (a.s.).

1- Ile aliyoitoa Ibnu Shaybah ndani ya kitabu *Al-Muswannaf*, kutoka kwa Ibnu Sirini amesema: "Mahdi ni kutoka ndani ya umma huu, na yeye ndiye atakayemsalisha Isa bin Maryam."1

2- Ile aliyoitoa Abu Nua'im kutoka kwa Abdullah bin Amru amesema: "Mahdi atateremkiwa na Isa bin Maryam, na Isa atasali nyuma yake."2

3- Ile aliyoisema Al-Munawi katika kufafanua Hadithi: "Ni kutoka kwetu yule ambaye Isa bin Maryam

atasali nyuma yake.” Akasema: “Kutoka kwetu” yaani sisi Ahlul–Bayt. “Ambaye” yaani mtu ambaye. “Isa bin Maryam atasali” yaani Ruhullah pindi atakapoteremka kutoka mbinguni zama za mwisho pindi Dajjal atakapodhihiri. “Nyuma yake” yaani atateremka wakati wa swala ya Asubuhi juu ya mnara mweupe Mashariki mwa Damascus, na kumkuta Imam Mahdi akitaka kusali, hivyo atamuhisi na hapo atarudi nyuma ili (Isa) atangulie, lakini Isa atamtanguliza na kusali nyuma yake. Na hapo umma huu utapata fadhila na sharafu kubwa kupitia kwake.”3

4– Aliyoisema Ibnu Burhani As–Shafiy kuhusu kuteremka kwa Isa (a.s.): “Kuteremka kwake kutakuwa wakati wa swala ya Alfajiri, atasali nyuma ya Mahdi baada ya Mahdi kumwambia: “Tangulia ewe Ruhullah” naye ata– jibu: Tangulia imekimiwa kwa ajili yako.”

Akaendelea mpaka akasema: “Hakika Mahdi atatokeza pamoja na Isa na hivyo kumsaidia kumuua Dajjal. Na imepokewa kuwa Mahdi ni kutoka kizazi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kupitia kizazi cha Fatima.”4

5– Ile iliyokuja ndani ya kitabu *Fat'hul–Bari*: “Abu Hasani Al–Khasaiy Al–Abadiy5 ndani ya kitabu *Manaqib Ash–Shafiiy* amesema: Zimekuwa nyin– gi mno habari kuwa Mahdi ni kutoka ndani ya umma huu na kuwa Isa ataswali nyuma yake. Amelitaja hilo ikiwa ni kujibu Hadithi ambayo ime– tolewa na Ibnu Majah kutoka kwa Anas isemayo: “Hakuna Mahdi ila ndiye Isa mwenyewe.” Kisha akajibu kauli ya At–Twibiy isemayo kuwa maana yake ni: “Isa atawasalisha akiwa ndani ya dini yenu.” Akajibu kwa kuse– ma: “Inabatilishwa na kauli yake iliyomo kwenye Hadithi nyingine ya Muslim: “Ataambiwa tusalishe. Atasema hapana, hakika wao kwa wao ni viongozi kwa ajili ya kuupa heshima umma huu.”

Kisha akanukuu kutoka kwa Ibnu Al–Jawziy kauli yake: “Laiti Isa ange– tangulia kama Imam basi nafsi ingeingiwa na utata, na ingesemwa: Unaona ametangulia kama naibu au nabii mpya kisheria? Hivyo ataswali kama maamuma ili asichafuliwe na vumbi za utata kutokana na kauli ya (s.a.w.w.): “Hakuna nabii yeyote baada yangu.”

Kisha akasema: “Isa kusali nyuma ya mtu wa kutoka ndani ya umma huu ilihali ikiwa ni zama za mwisho, na ile kukaribia Kiyama ni dalili zithibitishazo usahihi wa kauli zisemazo: Hakika ardhi haikosi khalifa wa Mwenyezi Mungu aliye hoja.” Na Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye zaidi.6

6– Aliyoitoa Ibnu Abu Shaybah kutoka kwa Ibnu Sirin: “Mahdi ni kutoka ndani ya umma huu na yeye ndiye atakayemswalisha Isa mwana wa Maryam.”7

---

1. Al–Muswannaf cha Ibnu Abu Shaybah 15: 198: 19495
2. Al–Hawi Lil–Fatawa cha As–Suyutiy 2: 78.
3. Faydhul–Qadir cha Al–Munawi 6: 17
4. As–Siratu Al–Halbiyah cha Ibnu Burhani As–Shafiy 1: 226 – 227.
5. Hivyo ndivyo ilivyo, na sahihi ni Al–Abariy. Baadhi wamemwita kwa kuniya ya Abu Husein, na sahihi ni Abu Hasani. Alifariki mwaka 363 A.H. Kama ilivyo ndani ya wasifu wake.

6. Fat'hul–Bari Bisharhi Sahih Bukhar cha Ibnu Hajar Al–Asqalaniy 6: 383 – 385.
7. Al–Muswannaf cha Ibnu Abu Shaybah 15: 198, 19495.

Jambo La Saba: Bendera ya Mahdi (a.s.)

Na miongoni mwa alama alizoongezewa mwislamu wa zama za kudhihiri kwake (a.s.) ili ajikinge na asiweze kuingia ndani ya mikondo ya upotovu ni wasifu wa bendera ya Imam Mahdi na wito wake unaosubiriwa. Kwani bendera yake (a.s.) ina alama itakayowaongoza wenye kungojea kudhihiri kwake, basi hebu tuzitazame riwaya hizi mbili zifuatazo:

1– Kutoka kwa Abdullah bin Sharik, amesema: "Mahdi atakuwa na ben– dera ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) iliyohukumiwa kushinda. Natamani ningekutana naye ilhali nikiwa ni mwenye nguvu mno."1

2– Kutoka kwa Abu Is'haqa kutoka kwa Nufu Al–Bukaiy: "Bendera ya Mahdi imeandikwa: Kiapo cha utii ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu."2

---

1. Ibnu Hammad: 249, Hadithi ya 972. Al–Qawlu Al–Mukhtasar: 100, mlango wa 3, Hadithi ya 35. Burhanul–Muttaqiy: 152, mlango wa 7, Hadithi ya 24.
2. Ibnu Hammad: 249, Hadithi ya 973. Uqad Ad–Durar: 274, mlango wa 9. Al– Qawlu Al–Mukhtasar: 101, mlango wa 3, Hadithi ya 36. Burhanul–Muttaqiy: 152, mlango wa 7, Hadithi ya 25. Faraidu Fawaidul–Fikri: 8, mlango wa 4. Yanabiul–Mawaddah: 435, mlango wa 73.

Jambo La Nane: Atoacho Imam Mahdi (a.s.)

Miongoni mwa mambo yasiyo na shaka kabisa ni kuwa uadilifu kwa maana yake yote utatimia chini ya utawala wa Mahdi (a.s.), ardhi na mbin– gu zitamwaga kheri zake na dola yake itakuwa ni dola ya mfano bora tuliyoahidiwa na Mola, dola ambayo ndani yake mwanadamu atakuwa mwema kwani hakutokuwa na dhuluma, unyang'anyi, ufakiri wala ufisadi. Hakika maelezo ya riwaya zifuatazo yanaashiria ukweli huu halisi:

1– Kutoka kwa Abu Said Al–Khudri (r.a.) kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Umma wangu utaneemeka zama za Mahdi kwa neema ambayo katu hawajawahi kuneemeka kwa mfano wake, watatumi– wa mvua nyingi na ardhi haitoacha mmea wowote ila itauotesha, na mali yenye kulundikana,

itakuwa mtu anasimama na kusema: Ewe Mahdi nipe, naye anamjibu chukua."1

2- Kutoka kwa Abu Said Al-Khudri (r.a.) amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Ndani ya umma wangu atakuwemo Mahdi, ikipungua ni miaka saba na kama si hivyo ni miaka tisa, ndani ya muda huo umma wangu utaneemeshwa kwa neema ambazo katu haujaneemeshwa kwa mfano wake. Ardhi itapatwa na mazao yake na wala hawatowekeza chochote. Kipindi hicho mali itakuwa imelundikana na hivyo mtu anasi- mama na kusema: Ewe Mahdi nipe, naye anamwambia chukua."2

3- Kutoka kwa Abu Said Al-Khudri (r.a.) amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Hakika ndani ya umma wangu yumo Mahdi, atatokeza na kuishi mitano au saba au tisa." Amesema: Tukasema ni nini hiyo? Akasema: "Miaka." Akasema: "Atakuwa anajiwa na mtu na kusema: Nipe, nipe." Akasema: "Ndipo anapomjazia nguo yake kwa kadiri atakavy- oweza kubeba."3

4- Kutoka kwa Jabir bin Abdullah Al-Ansariy kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: "Zama za mwisho atakuwepo khal- ifa anawajazia mali nyingi bila kuzihesabu mara kwa mara."4

5- Muslim ametoa ndani ya *Sahih* yake kutoka kwa Jabir bin Abdullah Al- Ansariy kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kuwa alise- ma: "Zama za mwisho atakuwepo khalifa anayegawa mali bila kuzihesabu."5

---

1. Ibnu Hammad: 253, Hadithi ya 992. Al-Bayan: 145, mlango wa 23. Uqad Ad- Durar: 225, mlango wa 8. Al-Fusul Al-Muhimmah: 288 na 289, sura ya 12. Nurul- Absar: 189, mlango wa 2.
2. Sunan Ibnu Majah 2: 1366 – 1367, Hadithi ya 4083. Mustadrak Al-Hakim 4:558. Burhanul-Muttaqiy: 81, mlango wa 1, Hadithi ya 25 na 82 mlango wa 1, Hadithi ya 26.
3. Sunan At-Tirmidhi 4: 439, mlango wa 53, Hadithi ya 2232. Al-Bayan: 107, mlango wa 6. Al-Ilal Al-Mutanahiyah 2: 858, Hadithi ya 1440. Mishkatul- Maswabihi 3: 24, sura ya 2, Hadithi ya 5455. Muqaddimatu Ibnu Khalduni: 393, sura 53. Urufus-Suyutiy Al-Hawi 2: 215. As-Sawaiq cha Ibnu Hajar: 164, mlango wa 11, sura 1. Kanzul-ummal 14: 262, Hadithi ya 38654. Mirqatul-Mafatihu 9:352. Mashariqul-An'war: 114, sura ya 2. Tuhfatul-Ahwadhiy 6: 404, Hadithi ya 2333. At-Taju Al-Jamiu Lil-Usul 5: 342 – 343.
4. Maswabihus-Sunnah 3: 488, Hadithi ya 4199. Pia kuna Hadithi nyingine muhimu ndani ya kitabu Muswannaf cha Abdur-Ridhaq 11: 371, Hadithi ya 20770, mlango wa Mahdi, ameitoa mwandishi wa kitabu Difau Anil-Kafiy 1: 266.
5. Sahih Muslim ufafanuzi wa An-Nawawiy 18: 39.

Jambo La Tisa: Miujiza ya Imam Mahdi (a.s.)

Ikiwa Mahdi tuliyeahidiwa ndiye mmoja kati ya maimamu watakasifu, kwa mujibu wa imani ya Shia Imamiyya ni lazima Imam huyu atakuwa na vipaji kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kama vile elimu pana

na uwezo wake wa kufanya miujiza ambayo ataitoa kwa watu ili kuhimiza uimamu wake na ukhalifa wake wa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), kama vitendo vya nguvu ya ghaibu vilivyokuwa vikitoka kwa baba zake, kwani baba zake kumi na moja watakasifu walikuwa na miujiza na karama mbalimbali iliyosisitiza hadhi yao mbele ya Mola. Maelezo ya riwaya zifuatazo yanaashiria ukweli huu halisi:

1- Kutoka kwa kiongozi wa waumini Ali bin Abu Twalib (a.s.) amesema: "Mahdi atakuwa anamwashiria ndege na kuanguka mikononi mwake, na atakuwa anapanda mti sehemu ndogo ya ardhi basi unastawi na kutoa majani."1

2- Kutoka kwa kiongozi wa waumini Ali bin Abu Twalib (a.s.) amesema: "Bendera tatu zitatofautiana: Bendera ya Morocco na bendera ya Uarabuni na bendera ya Sham, fitina itadumu mwaka mzima kati yao." Kisha akazungumzia kutokeza kwa As-Sufyaniy na dhuluma na ujeuri atakao- fanya, kisha akazungumzia kutokeza kwa Mahdi na kupewa kiapo cha utii eneo la kati ya Ruknu na Maqam, kisha akasema: "Atakwenda na jeshi kubwa mpaka afike kwenye mabonde ya vijiji kwa utulivu na upole, na huko mwana wa ami yake Al-Hasaniy ataungana naye akiwa na wapanda farasi elfu moja na kumwambia: Ewe mwana wa ami yangu! Mimi nina haki zaidi na jeshi hili kuliko wewe, mimi ni mwana wa Hasan na mimi ndiye Mahdi. Basi Mahdi (a.s.) atamjibu: "Bali mimi ndiye Mahdi." Hapo Al-Hasaniy atamwambia: "Je, una muujiza wowote nikupe kiapo cha utii? Ndipo Mahdi ataashiria kwenye ndege na kudondoka mikononi mwake, na atapanda mti sehemu ndogo ya ardhi na ndipo utastawi na kutoa majani. Hapo Al-Hasaniy atamwambia: Ewe mwana wa ami yangu hili (jeshi) lenyewe ni la kwako."2

Muhtasari

Kutokana na uchambuzi imebainika kuwa imani ya ulazima wa kudhihiri suluhisho la ulimwengu zama za mwisho si imani ya watu wa dini tu, bali inajumuisha hata makundi ya kitheolojia na kifilosofia yasiyokuwa ya kidini. Pamoja na dini kukiri ulazima wa kudhihiri suluhisho hili vilevile uchambuzi wa kielimu umeongeza utabiri mbalimbali uliopatikana ndani ya vitabu vya zama mbili kwa namna ya kipekee kuwa suluhisho hili ndiye Mahdi (a.s.).

Wanavyuoni bila kujali madhehebu yao ya kiisilamu wamesajili matamko ya kukiri kuzaliwa kwa Imam Mahdi (a.s.) kuanzia mwaka 260 A.H. mpaka wakati tulio nao. Hivyo basi, kulichunguza kundi la Hadithi za Mahdi (a.s.) zinazopatikana ndani ya vitabu vya Waisilamu kunatosha kuleta yakini kuwa zimetoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa wingi bila shaka yoyote ile.

Kwa muhtasari ni kuwa uwingi wake umethibiti ndani ya vitabu vya Sunni3 ambazo wanavyuoni na wasimulizi wamezitoa ndani ya vitabu vyao vingi.4 Wanavyuoni mbalimbali wametamka wazi hilo akiwemo At- Tirmidhiy aliyefariki mwaka 297 A.H.5, Al-Hafidhu Abu Jafar Al-Aqiliy aliyefariki mwaka 322 A.H6, Al-Hakim An-Nisaburi aliyefariki mwaka
405 A.H.7, Imam Al-Bayhaqiy aliyefariki mwaka 458 A.H.8, Imam Al- Baghawi aliyefariki mwaka 510 A.H.9, Ibnu Al-Athir aliyefariki mwaka

606 A.H[10]., Al–Qurtubiy Al–Malikiy aliyefariki mwaka 671 A.H.[11], Ibnu Taymiyya aliyefariki mwaka 728 A.H.[12], Al–Hafidhu Ad–Dhahabiy aliye– fariki mwaka 748 A.H.[13], Al–Kunjiy As–Shafiy aliyefariki mwaka 658
A.H.[14], Al–Hafidhu Ibnu Al–Qayyim aliyefariki mwaka 751 A.H.[15], na wengineo waliokiri usahihi wa Hadithi za Mahdi kama vinavyoeleza vitabu vyao.

Pia kundi lingine la wanavyuoni wa kisuni limetamka wazi uwingi wa Hadithi za Mahdi, na sisi hapa tutafupisha kwa kutaja baadhi yao akiwemo Al–Barbahariy aliyefariki mwaka 329 A.H.[16], Muhammad bin Hasan Al–Abariy As–Shafiy aliyefariki mwaka 363 A.H., hili limenukuliwa na Al– Qurtubiy Al–Malikiy[17] kutoka kwake. Na Al–Qurtubiy Al–Malikiy aliye– fariki mwaka 671 A.H.[18], Al–Hafidhu Al–Mutqinu Jamalud–Dini Al– Mazniy aliyefariki mwaka 742 A.H.[19], Ibnu Al–Qayyim aliyefariki mwaka 751 A.H.[20], Ibnu Hajar Al–Asqalaniy aliyefariki mwaka 751 A.H.[21], na wengineo.

Na nyongeza ya habari zinazounga mkono uwingi wa Hadithi zake ni zile zinazotoa wasifu wake, umbile lake na vitendo vyake, na habari zina– zozungumzia jina lake, nasaba yake, jina la mama yake na jina la baba yake.

Na tunamuainisha kutoka kwenye habari zisizoainisha kwa kupitia habari zinazozungumzia utu wake kama zile zinazosema kuwa Mahdi ni kutoka wana wa Abdul–Mutwalib, na kuwa yeye ni kutoka kizazi cha Abu Talib, na kuwa ni kutoka Ahlul–Bayt (a.s.) na kuwa ni kutoka kizazi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na kuwa ni kutoka kizazi cha Fatima, na kuwa ni kutoka kizazi cha Husein na kuwa ni kutoka kizazi cha As–Swadiq na kuwa ni kutoka kizazi cha Ar–Ridha (a.s.), na kuwa yeye ni khalifa wa Mwenyezi Mungu na hitimisho la maimamu, na kuwa yeye atamsalisha Nabii Isa (a.s.).

Maelezo haya yote ambayo yanamuainisha na kumbainisha Imam Mahdi tuliyeahidiwa ambaye hitimisho la Mitume, Muhammad (s.a.w.w.) alibashiri kudhihiri kwake zama za mwisho yanaonyesha kuwa yeye ni Muhammad bin Hasan Al–Askari bin Ali Al–Hadiy bin Muhammad Al– Jawaad bin Ali Ar–Ridha.

Na hivyo inabainika waziwazi kuwa Mahdi tuliyeahidiwa amezaliwa nusu ya pili ya karne ya tatu ya hijiriya na yeye yuko hai anaendelea kuruzuki– wa. Ama kitendo cha sifa zake kuelezwa kwa ufafanuzi zaidi kwa kutilia umuhimu sifa zake za kimwili, kiroho na kimaadili ni uthibitisho wa kweli jinsi gani sheria ilivyotilia umuhimu uainishaji wa mtu huyu kiongozi wa kiulimwengu tuliyeahidiwa na mfano halisi wa mtu huyo ambaye ni Imam Mahdi (a.s.) ili asifanane na mwingine na ili wapotoshaji wasitumie fursa hii kuwapotosha watu. Na zaidi ya hapo uainishaji huu unamzidishia mtafi– ti imani na yakini kuhusu suala la kiulimwengu la Imam Mahdi (a.s.) kupi– tia wasifu wake uliotolewa na Uislam.

Na mwisho wa dua zetu ni kushukuru kuwa kila sifa njema ni ya
Mwenyezi Mungu.

---

1. Burhanul–Muttaqiy: 76, mlango wa 1, Hadithi ya 14.

2. Burhanul–Muttaqiy: 76, mlango wa 1, Hadithi ya 15.
3. Rejea Ibrazul–Wahmi Al–Maknuni: 437.
4. Ameviorodhesha Ustadh Muhammad Ali Dakhil ndani ya kitabu chake Al– Imam Al–Mahdi: 259 – 365, mpaka kafikisha vitabu thelathini vya kisuni.
5. As–Sunan At–Tirmidhiy 4: 505, 2230, 2231 na 4: 506, 2233.
6. Ad–Dhuafau Al–Kabir cha Al–Aqiliy 3: 253 na 1257.
7. Mustadrak Al–Hakim: 4 / 429 na 465 na 553 na 558.
8. Al–Itiqad Wal–Hidayatu Ilas–Sabilir–Rashadi cha Al–Bayhaqiy: 127.
9. Maswabihus–Sunnah: 492 – 493 / 4210 – 4213 na 4215.
10. An–Nihayatu Figharibil–Hadithi Wal–Athar cha Ibnu Al–Athir 5: 254.
11. At–Tadhkiratu cha Al–Qurtubiy: 704, mlango wa yanayomhusu Mahdi.
12. Minihajus–Sunnah cha Ibnu Taymiya 4: 211.
13. Talkhisul–Mustadrak cha Ad–Dhahabiy 4: 553 na 558.
14. Al–Bayanu Fi–Akhbar Swahibuz–Zaman: 500.
15. Al–Manaru Al–Munif cha Ibnu Al–Qayyim: 130 – 135/ 326 na 327 na 39 na 331.
16. Al–Ihtijaju Bil–Athari Ala Man An'kara Al–Mahdi Al–Muntadhar: 28.
17. At–Tadhkirah 1: 7. Tahdhibul–Kamal cha Al–Mazniy 25: 146 / 5181.
18. At–Tadhkirah 1: 701.
19. Tahdhibul–Kamal 25: 146, 5181.
20. Al–Manaru Al–Munif: 135.
21. Tahdhibut–Tahdhibu 9: 125, 201.

Mahdi Wa Ahlul–Bait

Kimeandikwa na:
Sheikh Abdul Karim al–Bahbahani
Kimetarjumiwa na:
Hemedi Lubumba Selemani

Neno La Jumuiya

Hakika mirathi ya Ahlul–Bait ambayo imehifadhiwa na madhehebu yao na wafuasi wao dhidi ya upotovu inaonyesha madhehebu iliyokusanya aina mbalimbali za taaluma za kiislamu.

Kambi hii imeweza kulea nafsi mbalimbali zilizo tayari kunywa kutoka kwenye chemchemu hiyo, na kuupa umma wa kiislamu Wanachuoni wakubwa wenye kufuata nyayo za ujumbe wa Ahlul–Bait.

Wanachuoni waliyokusanya vidodosa na maswali mbalimbali ya madhe– hebu na mitazamo tofauti ya kifikira kuanzia ndani ya desturi za kiisilamu hadi nje ya desturi hizo, huku wao wakitoa majibu na utatuzi

makini juu ya maswali hayo ndani ya karne zote.

Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul–Bait imefanya hima kutetea tukufu za ujumbe wa Uislamu na ukweli wake ambao umechafuliwa na makundi, madhehebu na wanaharakati mbalimbali wenye chuki na Uislamu.

Jumuiya imefuata nyayo za Ahlul–Bait na za wafuasi wa madhehebu yao njema ambayo imefanya hima kujibu madai yenye kuendelea na daima ika– jaribu kubaki ndani ya msitari wa mapambano kwa kiwango kinachohita– jika ndani ya kila zama.

Hakika uzoefu ambao umehifadhiwa ndani ya vitabu vya wanachuoni wa madhehebu ya Ahlul–Bait katika dhamira hii ni wa aina ya pekee, kwa sababu una akiba ya kielimu inayotegemea akili na hoja, huku ukijiepusha na matamanio na upendeleo uliokatazwa.

Unazungumza na wasomi na wanafikra wenye fani maalumu, mazungum– zo ambayo yanakubalika kiakili na yanapokewa na maumbile yaliyo sala– ma.

Jaribio hili la Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul–Bait limekuja kuwapa watafu– ta ukweli hatua mpya ya uzoefu wa thamani katika ulingo wa mazungum– zo na maswali na kujibu hoja za utata zilizotolewa zama zilizopita au zina– zotolewa leo kwa njia ya Tovuti, na hasa kwa kupewa nguvu na baadhi ya duru zenye chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Ikijiepusha na uchochezi uliokatazwa, na ni yenye kuhangaikia kuzishau– ri akili zenye kufikiria na nafsi zenye kutafuta haki, ili ziweze kufikia kwenye haki ambayo inatolewa na Kambi ya Ahlul–Bait ulimwengu mzima, ndani ya zama ambazo akili inaerevuka na nafsi na roho zinabore– ka kwa kasi ya pekee.

Ni lazima tugusie kuwa mfululizo huu wa tafiti hizi umeandaliwa na Kamati maalumu toka jopo la wanachuoni watukufu, hivyo tunatoa shuku– rani njema kwa hawa wote na kwa wasomi na wahakiki kwa kila mmoja miongoni mwao kwa kupitia sehemu ya tafiti hizi na kutoa mchango wao wa thamani kuhusu tafiti hizi.

Na sote tunategemea na kutaraji kuwa tutakuwa tumetoa kile tulichoki– weza katika juhudi za kutekeleza baadhi ya wajibu tulionao mbele ya ujumbe wa Mtukufu Mola Wetu Mlezi ambaye alimtuma Mtume Wake na uongofu na dini ya haki ili aipe ushindi dhidi ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.

Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlu–Bait

Kitengo cha utamaduni

Imani ya uimamu wa maimamu kumi na wawili ni msingi wa uelewa juu ya Mahdi (a.s.)

Hakika chanzo cha wazo la kudhihiri mwokozi ambaye anawakilisha msingi wa wazo la Mahdi ndani ya Uislamu ni wazo la wanadamu wote wala si la dini fulani au madhehebu mahsusi, na ukweli huu wenyewe binafsi unasaidia kuvunja hoja nne za utata juu ya suala la Mahdi wakati mmoja.

Kwanza: Wenyewe unafafanua ubatilifu wa hoja isemayo kuwa wanaoamini imani ya Mahdi ni Shia tu. Na hasa inapothibiti ijimai ya waislamu juu ya imani yake.

Pili: Unafafanua ubatilifu wa hoja ya ngano isemayo kuwa, imani kuhusu Mahdi ni ngano itokanayo na dhana isiyo na uwepo, kwani hakika ngano ni dhana tupu isiyo na uwepo wowote itokanayo na hali ya kikabila au kitaifa au kundi maalumu. Na hakuna ngano yoyote inayothaminiwa na dini zote za kimungu na zisizo za kimungu, huku ikielezea dhamira ya wanadamu wote na huku wanachuoni na wanafikra pamoja na wanafalsafa mbalimbali wakiikubali.

Tatu: Unafafanua ubatilifu wa hoja isemayo kuwa Mayahudi wana mchango mkubwa katika kupandikiza wazo la kuwepo Mahdi. Ikiwa wazo la Mahdi linaaminiwa na dini zote hata zile zisizokuwa za kimungu, basi ni kwa nini tunachukia wazo hili kuwemo ndani ya Uislamu? Kwani kwa mujibu wa akili salama na mantiki ni kuwa Uislamu unapasa uwe na wazo hili tena kwa uwelewa wa wazi zaidi na uliokamilika zaidi, kama ilivyo ndani ya madhehebu ya Ahlul–Bait (a.s.).

Hivyo basi miongoni mwa ukamilifu wa dini hii na madhehebu hii ni kule kulimiliki kwa ukamilifu wazo la kuwepo Mahdi, hivi dini za kimungu si zinashirikiana katika duru nyingi za kiimani na kisharia kama vile hija, Swaumu na Swala...? Hivi Mayahudi kuamini ibada hizi inapasa kuwa sababu ya Uislamu kuzikana? Au inapasa kuzihimiza na kuzitolea uwele– wa uliokamilika na wa hadhi ya juu mno? Hakika hoja yao hii inawaletea wenyewe upungufu na kuuletea Uislamu na Ushia ukamilifu.

Nne: Unafafanua ubatilifu wa hoja isemayo kuwa wazo la kuwepo Mahdi limetokana na mazingira ya ugandamizaji wa kisiasa ambao uliwapata Maimamu (a.s.), kwani makhawariji walikumbana na ugandamizaji usioto– fautiana na ule uliowakumba wafuasi wa Maimamu (a.s.) na kama hiyo ingekuwa ni kanuni basi ni wangapi wamedhulumiwa na kugandamizwa lakini hawaamini wazo la Mahdi. Na ni makundi mangapi na watu wan– gapi wameamini wazo hili bila ya kukumbana na dhuluma na ugan– damizaji. Na kama imani hii ingekuwa inatokana na dhuluma na ugan– damizaji kwa nini imani hii imedhihiri kwenye vizazi vilivyofuata visivyogandamizwa?

Ndiyo, tunaweza kuamini kuwa sababu za ugandamizaji na unyanyasaji zinafaa kumsukuma mtu zaidi kushikamana na wazo la Mahdi, lakini si kwamba zenyewe ndizo zinaanzisha wazo hili na kuwa msingi wa kuwepo kwa wazo hili.

Hakika dini ni maelezo kamilifu mno kuhusu uhalisia wa mwanadamu, na Uislamu ni maelezo kamilifu mno kuhusu uhalisia wa dini, na madhehebu ya Ahlul–Bait ni maelezo kamilifu mno kuhusu uhalisi wa Uislamu.

Hivyo basi, pindi dini zinapoeleza waziwazi wazo la mwokozi wa ulimwengu huwa zinafichua dhamira ya mwanadamu iliyohimizwa na huwa ni kwa namna bora mno. Na pindi Uislamu unapoelezea waziwazi wazo hili huwa unaelezea waziwazi ukweli wa kidini uliyohimizwa na huwa ni kwa namna bora zaidi kuliko ulivyoelezwa na dini zilizotangulia.

Na pindi madhehebu ya Ahlul–Bait inapoelezea waziwazi wazo hili huwa inatoa maelezo kamilifu mno kuhusu ukweli wa Uislamu katika dhamira hii.

Hivyo tofauti iliyopo kati ya uelewa wa madhehebu ya kisunni na madhe– hebu ya Ahlul–Bait kuhusu Mahdi ni tofauti kati ya madhehebu inayobain– isha kiwango cha chini cha ukweli na madhehebu inayochukua jukumu la kubainisha ukweli wa Uislamu kwa kiwango cha juu mno. Hivyo madhe– hebu ya kwanza ikadhani kuwa madhehebu ya pili imepita njia ya mapen– zi ya kupindukia na nje ya mstari.

Siri ya Ushia kuwa mashuhuri kwa wazo la Mahdi mpaka likawa kama lin– auhusu Ushia tu na si miongoni mwa imani waliyokubaliana Waisilamu wote, huenda ni ile hali ya Ushia kuhusika kwa kiwango cha ukamilifu mno katika suala la Mahdi, huku uwelewa huo kwake ukiwa na sifa za kipekee ambazo kwazo inatimia ile maana halisi inayohitajika kutoka kwenye wazo la Mahdi.

Na sifa hizi zinatoka ndani ya msingi mmoja nao ni kuwa wazo la Mahdi katika uelewa wa Ahlul–Bait si nadharia tu ya mustakabali na wala si kutoa tu habari za mustakabali mwema kwa binadamu ambao atakuwanao mwisho wa safari kama linavvyoonekana kwa madhehebu ya Makhalifa, bali lenyewe ni sehemu isiyoachana na imani ya uimamu wa Maimamu kumi na wawili ambao Mwenyezi Mungu aliamua utawale ulimwengu tokea sekunde ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mpaka sekunde za mwisho za uhai wa wanadamu. Au kwa maelezo mengine ni kuwa wazo hilo ni suala la Imam wa kumi na mbili ambaye uimamu wake umeanza tangu mwaka 260 A.H. ukaendelea mpaka sasa na utazidi kuendelea mpaka atakapodhihiri mwishoni mwa historia ya mwanadamu.

Sisi tunapochambua suala la Mahdi katika uwelewa wa Ahlul–Bait (a.s.) ni lazima tuhimize msingi huu wa kiimani, na tutazame tena upande wa dalili na hoja kwa lengo la kuthibitisha, na mara nyingine tutazame matokeo ya

imani hiyo, na mara ya tatu tutazame upande wa hadhi ya kiimani iliyon– ayo matokeo hayo, hivyo kuna hatua tatu za uchambuzi na kila hatua tutai– weka kwenye sura yenye kujitegemea.

Sura Ya Kwanza

Uthibitisho wa kiimani juu ya uwelewa wa wazo la

Mahdi upande wa Ahlul-Bait (a.s.)

Dalili ya kiimani juu ya wazo hili inapatikana ndani ya mamia ya riwaya zilizopatikana kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)1 ambazo zinamwainisha Mahdi kuwa ni miongoni mwa Ahlul-Bait (a.s.)2.... Na kuwa ni kutoka kizazi cha Fatima3... Na ni kutoka kizazi cha Husein4.... Na kuwa ni wa tisa kutoka kizazi cha Husein5....

Na kuwa ni Khalifa wa kumi na mbili.6

Haya ni makundi matano ya riwaya zinazoshindana katika kubainisha uwelewa wa wazo la Mahdi na kumwainisha Imam Mahdi, na yule atakayezichunguza atazikuta zinakwenda hatua kwa hatua zikianzia kwenye anuani kuu mpaka kwenye kifungu kidogo mpaka zinafika kumwainisha mhusika mwenyewe.

Sayyid Shahid Muhammad Baqir As-Swadri (q.s.) amebainisha kuwa: "Zimefikia kiwango cha juu cha uwingi na kuenea licha ya kuwa Maimamu (a.s.) walijizuia na kuchukua tahadhari katika kueneza fikira hii kwa watu wote, walifanya hivyo kwa ajili ya kumlinda mrithi mwema (a.s.) dhidi ya njama mbaya zinazolenga kuutoa uhai wake haraka iwezekanavyo.7 Wala uwingi wa idadi ya wapokezi wake sio kigezo pekee cha msingi cha kuzikubali, bali zaidi ya hapo ni sifa na vielelezo vinavyothibitisha usahihi wake.

Hivyo baadhi ya waandishi wamehesabu riwaya za Mtukufu Mtume kuhusu Maimamu au Makhalifa au Watawala baada yake, na kuwa wao ni Maimamu au Makhalifa au Watawala kumi na wawili wakazikuta ni zaidi ya riwaya mia mbili na sabini8**,** huku zikiwa zimechukuliwa kutoka kwenye vitabu mashuhuri vya Shia na Sunni, vikiwemo *Bukhari*9, *Muslim*10*, Tirmidhi*11**,** *Abu Dawdi*12**,** *Musnad Ahmad*13 na *Mustdrakul-Hakim Alas-Sahihayni*14.

Hapa tunakuta kuwa Bukhari ambaye amenukuu Hadithi hii aliishi zama za Imam Al-Jawwad na maimamu wawili Al-Hadiy na Al-Askari, hilo lina makusudio makubwa; kwa sababu hilo linathibitisha kuwa Hadithi hii ilisajiliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kabla ya madhumuni yake kutimia kivitendo ambayo ni fikira ya maimamu kumi na wawili. Hii inamaanisha kuwa hakuna shaka yoyote kuwa unakili wa Hadithi hii ume- tokana na ukweli wa wazo la uimamu wa maimamu kumi na wawili; kwa sababu Hadithi za uzushi ambazo zinanasibishwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni matukio au uhalalishaji wa hali iliyochelewa, Hadithi ambazo hazijaitangulia hali hiyo katika kudhihiri kwake na kusajiliwa ndani ya vitabu vya Hadithi.

Maadamu tumemiliki dalili ya kimaada kuwa Hadithi iliyotajwa ilitangu- lia kabla ya mfululizo wa kihistoria wa maimamu kumi na wawili, na ikad- hibitiwa ndani ya vitabu kabla ya kutimia maimamu kumi na wawili, basi tunaweza tukazidi kuamini kuwa Hadithi hii haitokani na hali hiyo bali yenyewe ni maelezo ya uhalisia kutoka kwa Mola ambayo ilielezwa na yule asiyetamka kwa matamanio yake,[15] akasema: “Makhalifa baada yangu ni kumi na wawili.”[16] Na hali halisi ya maimamu kumi na wawili ikaanzia kwa Imam Ali na kukomea kwa Mahdi (a.s.) ili iwe ni uoanishaji wa pekee wa Hadithi hiyo tukufu[17] wenye kukubalika kiakili.”[18]

Muslim ametoa ndani ya Sahih yake kwa njia ya Qutaybah bin Said kuto- ka kwa Jabir Ibnu Samara, amesema: “Niliingia na baba yangu kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) nikamsikia akisema: “Jambo hili halitotoweka mpaka litawaliwe na makhalifa kumi na wawili.” Kisha akasema: Akazungumza maneno ambayo sikuyasikia, nikamwambia baba yangu: Amesema nini? Akasema: “Wote ni kutoka kwa makurayshi.”[19]

Kisha ameitoa kutoka kwa Ibnu Abu Umar, kutoka kwa Hudabu bin Khalid kutoka kwa Nasru bin Ali Al- Jahdhamiy kutoka kwa Muhammad bin Rafiu wote kwa njia moja. Na ameitoa kutoka kwa Abubakr bin Abu Shayba kwa njia wawili. Na kutoka kwa Qutaybah bin Said kwa njia wawili nyingine. Hizi ni njia tisa za Hadithi hii ndani ya kitabu Sahih Muslim tu, tusikwambie njia zake nyingine nyingi ndani ya vitabu vya Hadithi vya Sunni na Shia.[20]

Kambi ya Sunni yatapatapa katika tafsiri ya Hadithi hii

Swali hapa ni akina nani hawa makhalifa? Kabla hatujachagua jibu husi- ka la swali hili ni lazima kwanza tutoe dhana mbalimbali zinazotarajiwa katika maana ya Hadithi hii, na makusudio ya Mtukufu Mtume hapo. Hapa kuna dhana wawili tarajiwa na wala hakuna ya tatu, nazo ni:

1. Makusudio ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni kubainisha hali ya kisiasa itakayoupata umma baada yake, akiwa katika hali ya kufichua na kuonye- sha mustakabali ikiwa ni mfululizo wa tabiri mbalimbali zilizotoka kwa (s.a.w.w.) kuhusu masuala mbalimbali. Hivyo malengo ya Hadithi hii ni kutoa habari za hali halisi ya mustakabali wa umma. Dhana hii tuipe jina la “ufafanuzi juu ya hali ya mustakabali.”

2. Makusudio ya (s.a.w.w.) ni kutoa azimio kwa kuainisha Imam na Khalifa baada yake, hivyo malengo yake ni kuanzisha na kusimika kwa mujibu wa sharia, na si kuelezea hali halisi ya mustakabali. Dhana hii tuipe jina la “ufafanuzi juu ya imani.”

Kwa muktadha wa elimu tunawajibika kuchunguza dhana hizi wawili na mwisho tuchague ile inayoungwa mkono na dalili na hoja za kiakili na za kinukuu. Ispokuwa madhehebu ya Sunni tangu mwanzo ilipoamini sheria ya utaratibu wa ukhalifa ilikataa nadharia ya uteuzi na hatimaye theiolojia yao na fikihi yao vikajengeka juu ya msingi huu na hivyo ikajikuta mbele ya dhana moja tu bila kuwa na kiwawilio lingine, nayo ni dhana ya kwan- za, na mwisho ikalazimika kukiletea tafsiri nyingine kila kinachopingana nayo, na kulazimika kuchukua tafsiri hizi hata kama hazioani na Hadithi na ziko mbali

mno na kanuni za kiakili na za kijamii, kwa sababu ni jambo lisilokuwa na njia mbadala.

Kambi hii ilitakiwa iichunguze Hadithi hii kwa uchunguzi wa kielimu huru usioegemea fikira yoyote ili iweze kupata uhakika wa ubovu wa tafsiri ya “dhana ya ufafanuzi juu ya hali ya mustakbali”. Kwani ikiwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) lengo lake ni kutoa hali itakayotokea basi ni sababu ipi iliyopelekea kuweka kikomo cha idadi ya makhalifa kumi na wawili ilihali mustakabali bado unaendelea zaidi ya hapo?

Ikiwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alilenga ukhalifa sahihi unaooana na vip– imo vya sharia basi jua hakika madhehebu ya Sunni haiamini na wala hai– jakongamana ila kwa makhalifa wanne. Na kuanzia hapa ndipo mitazamo yao ikatapatapa katika kuainisha watu maalumu walio makhalifa kumi na wawili.

Kwa Ibnu Kathir makhalifa kumi na wawili ni wale wanne pamoja na Umar bin Abdul–Aziz na baadhi ya wana wa Abbas, na akadhihirisha kuwa Mahdi ni miongoni mwao.21

Kwa Kadhi Ad–Damashqiy makhalifa kumi na wawili ni wale wanne pamoja na Muawiya, Yazid bin Muawiya, Abdul–Malik bin Mar’wan na wanae wanne: Al–Walid, Sulayman, Yazid na Hisham. Na wa mwisho ni Umar bin Abdul–Aziz.22

Kwa Waliyullah msimulizi kwenye viburudisho vya macho mawili, kama ilivyokuja ndani ya kitabu ‘Awnul–Maabud’ makhalifa kumi na wawili ni wale wanne pamoja na Muawiya, Abdul–Malik bin Mar’wan na wanae wanne na Umar bin Abdul–Aziz na Walid bin Yazid bin Abdul–Malik. Kisha akanukuu kutoka kwa Malik bin Anas kuwa yeye alimjumuisha Abdullah bin Zubayr katika orodha hiyo, lakini mwandishi akaikataa kauli ya Malik akitoa dalili kupitia riwaya iliyopokewa kutoka kwa Umar na Uthman kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) inayoonyesha kuwa kutawala kwa Ibnu Zubayri kulikuwa ni miongoni mwa misiba mikubwa ya umma huu. Kisha akampinga yule aliyemjumuisha Yazid katika orodha hiyo huku akitamka waziwazi kuwa alikuwa na mwenendo mbaya mno.23

Ibnul–Qayyim Al–Jawziyy amesema: “Ama kuhusu makhalifa kumi na wawili ni kuwa jamaa akiwemo Abu Hatim na Ibnu Habban na wengineo wamesema: Wa mwisho wao ni Umar bin Abdul–Aziz, hivyo wakawataja makhalifa wanne kisha Muawiya kisha mwanae Yazid, kisha Muawiya bin Yazid kisha Mar’wan bin Al–Hakam, kisha Abdul–Malik na mwanae, kisha Al–Walid Ibnu Abdul–Malik kisha Sulayman bin Abdul–Malik kisha Umar bin Abdul–Aziz na kifo chake kilikuwa mwishoni mwa mwaka wa mia moja, nayo ndio karne iliyofadhilishwa ambayo ndio karne bora, na dini katika karne hii ilikuwa katika kilele cha utukufu kisha ndipo yakatokea
yaliyotokea.”24

An–Nur Bashtiy amesema: “Njia katika Hadithi hii na inayofatia katika maana hii, hutafsiriwa kuwa inawalenga waadilifu miongoni mwao, kwani wao ndio wanaostahiki jina la Khalifa kwa maana yake halisi, na wala hailazimu wawe ni watawala. Na hata kama ikikadiriwa kuwa wao ni watawala basi hakika makusudio ni wale wanaoitwa hivyo kwa kinaya, na ndio hali hiyo hiyo kwa waasi.”25

Kwa Al–Muqriziy makhalifa kumi na wawili ni wale wanne kisha Imam Hasan (a.s.), amesema: “Kwake

yeye (a.s.) ndiko kulikomalizikia siku za makhalifa waongozaji." Yeye hajamjumuisha yeyote miongoni mwa wana wa Umayya, kwani ametamka waziwazi kuwa baada yake ukhalifa uligeu- ka ufalme wenye kung'ang'aniwa.

Amesema: "Yaani kulikwa na nguvu na dhuluma!!" Pia hajamjumuisha yeyote miongoni mwa wana wa Abbas akitamka waziwazi kuwa ukhalifa wao "ulifarakisha nguvu ya Uislamu na jina la waarabu likatoweka ndani ya shajara, wakaingizwa waturuki ndani ya shajara hiyo, wakaimarika madaylum kisha waturuki, hatimaye wakawa na dola kubwa mno na tawala za ardhi zikagawika sehemu mbalimbali na kila eneo likawa na mtawala anawaendesha watu kwa dhuluma na kuwatawala kwa nguvu."

Inaonekana waziwazi jinsi gani madhehebu ya Sunni inavyotapatapa kati- ka kutafsiri Hadithi hii na kuingia kwenye tope ambazo inashindikana kuji- nasua maadamu tu bado inang'ang'ania maana ya tafsiri ya 'ufafanuzi wa hali ya mustakabali'.

As-Suyutiy amesema ndani ya kitabu Al-Hawi: "Mpaka leo bado hawa- japatikana kumi na wawili ambao umma wote umekongamana juu ya kila mmoja miongoni mwao."26

Laiti tafsiri ya 'ufafanuzi wa hali ya mustakabali' yenyewe binafsi ingekuwa ni sahihi na inakubalika basi maswahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wangeiamini kabla ya mwingine yeyote na imani hiyo ingeonekana kupitia ndimi za makhalifa wenyewe, na wa kwanza wao angesema: Mimi ndiye wa kwanza kati ya makhalifa kumi na wawili, na wa pili na wa tatu mpaka wa kumi na wawili wote wangesema mfano wa maneno hayo, na dai kama hili lingekuwa ni fahari kwao na ushahidi tosha wenye kusaidia kuthibitisha uhalali wa kila mmoja miongoni mwao. Lakini historia haijasajili dai la namna hiyo kutoka kwa yeyote miongoni mwa majina hayo yaliyotajwa katika orodha ya makhalifa kumi na wawili wa bandia.

Hakika Hadithi inaonyesha kuwa kipindi cha uimamu wa maimamu kumi na wawili kitajumuisha umri mzima wa Uislamu mpaka mwisho wake kiasi kwamba baada yao ardhi haitokuwa na mtu yeyote. Sunni wame- pokea kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwa alisema: "Dini hii itaendelea kusimama mpaka watimie kumi na wawili wote kutoka kwa makurayshi, wakitoweka basi ardhi haitokuwa na mtu."27

Ardhi haikutoweka wakazi wake baada ya kifo cha Umar bin Abdul-Aziz, bali kuenea kwa elimu mbalimbali za dini kama vile elimu ya sharia, Hadithi na tafsiri kuliimarika ndani ya karne wawili za hijiriya, ya tatu na ya nne, mpaka elimu za dini zikafikia kilele cha ubora katika kuenea ikiwa ni baada ya kufariki hawa makhalifa kumi na wawili wa Sunni, wakati ili- takiwa ardhi isiwe na wakazi wake!

Pia wamepokea kutoka kwa Jabir bin Samra kuwa: "Umma huu utaende- lea kuimarika katika jambo lake, ukiwa na nguvu juu ya adui wake mpaka watimie makhalifa kumi na wawili miongoni mwao, wote ni kutoka kwa makurayshi, kisha ndipo itapatikana *'maraji*.'"28**28**

Ikiwa makusudio ya neno "*maraji*" ni moyo kuuma, msukosuko na utata basi inapasa kusema kuwa

hakikutokea kitu kama hicho hata mpaka zama za Umar bin Abdul–Aziz. Lakini historia haijui fitina kubwa ambayo mau– mivu ya moyo yalizidi, msukosuko uliongezeka na utata kati ya haki na batili ulikuwa ila ni ile ya Muawiya na kitendo chake cha kutoka kwenda kumpiga Khalifa wa waisilamu.

Hii inaonyesha kuwa muradi wa neno "*maraji*" ni kitu kikubwa zaidi kuliko maumivu ya moyo, msukosuko na utata, na huenda muradi ikawa ni kitendo cha kuachwa dini yote, na hili halijatokea ila litatokea Kiyama kitakapokaribia, Kiyama ambacho kitatanguliwa na udhihiri wa Imam Mahdi na matukio mengine yatakayotokea baada ya kufariki kwake.

Kisha akinamaanisha nini kitendo cha kuwajumuisha wafalme kwenye orodha ya makhalifa?! Bila shaka Sunni wamepokea kutoka kwa Saad bin Abu Waqqas mmoja wa kumi waliobashiriwa, na mmoja wa wajumbe wa kamati aliyoiteua Umar, kuwa aliingia kwa Muawiya huku akiwa amekataa kumpa kiapo cha utii, akasema: "Amani iwe juu yako ewe mfalme." Akamjibu: "Je, hakuna jingine lisilokuwa hilo? Ninyi ni waumini na mimi ni kiongozi wenu." Akasema: "Ndiyo, iwapo tukikupa uongozi." Katika tamko lingine: "Sisi ni waumini na hatujakupa uongozi."

Aisha alimkanusha Muawiya juu ya dai lake la ukhalifa, kama ambavyo pia Ibnu Abbas alikanusha dai hilo, na hata Imam Hasan (a.s,) aliendelea kukanusha hata baada ya suluhu29, hivyo yeye ni miongoni mwa waovu kwa itifaki ya wote kwa mujibu wa Hadithi: "Ewe Ammar litakuuwa kundi ovu." Sasa sijui vipi imesihi muovu aliyetoka kumpiga Khalifa halali kuwa Khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu juu ya waumini!

Kinamaanisha nini kitendo cha kumjumuisha Yazid muovu kwenye orod– ha ya makhalifa?! Ambaye alikuwa akidhihirisha waziwazi ufasiki wake na uvunjaji wa heshima ya Mwenyezi Mungu, na kweli hili ni ajabu ya maajabu! Vipi inasihi kwa mwislamu amfanye kuwa Khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) mtu ambaye anamwaga damu za watu wa nyumba ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), mtu ambaye jeshi lake linalivamia Jiji la Madina na kuwaua maelfu ya wakazi wake kiasi kwam– ba baada ya tukio hilo hakubaki hai sahaba yeyote yule aliyepigana vita vitukufu vya Badri!

Na ndio hali hiyo hiyo kwa wafalme toka mti uliolaniwa na Qur'an tuku– fu, bila shaka Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) aliwaona usingizini, na kama ujuavyo ndoto ya Mtume ni kweli, aliwaona wakichezea mimbari yake kama wachezavyo ngedere (tumbir). Hilo ni kwa mujibu wa itifaki ya wafasiri wengi wa Qur'an wa kisunni pindi wanapoifasiri Aya ya sitini ya Sura Al–Israi, wala hatuna haja ya kunukuu maneno yao.

Hivyo kwa uwazi kabisa yanadhihiri matokeo matatu:

1. Kufeli kwa tafsiri ya "ufafanuzi juu ya hali ya mustakabali" kwenye Hadithi ya ukhalifa wa maimamu kumi na wawili.

2. Mchango wa sababu ya kisiasa katika kuisababisha madhehebu ya Sunni ikiwawilie tafsiri hiyo.

3. Tafasiri ya kweli ya halali ya Hadithi imekomea kwenye tafsiri ya “ufafanuzi juu ya imani” ambayo inasema Hadithi iliyotajwa inaonyesha kuwekwa kwa maimamu kumi na wawili wa waisilamu, na hiyo ndiyo tafsiri iliyothibitishwa na dalili za kiakili na Aya nyingi za Qur’an ambazo zimefafanuliwa sana kwenye vitabu vya Shia Imamiya vya sasa na vya zamani, tazama hilo kwenye ulingo wa tafsiri, Hadithi, theiolojia na historia.

Inaonekana wazi kuwa historia haijataka kitu ila kuwabakisha maimamu kumi na wawili kutoka nyumba ya Mtume (a.s.) ili wawe mfano halisi pekee wa Hadithi iliyotajwa kiasi kwamba hawapingwi katika hilo hata katika kiwango cha madai. Wa kwanza wao ni kiongozi wa waumini (a.s.) na wa mwisho wao ni Imam Mahdi mwana wa Hasan Al-Askarii (a.s.), na hazihesabiki kwa wingi wake Hadithi tukufu zinazothibitisha hilo.

Hapa tutaashiria moja kati ya hizo, nayo ni ile aliyoitoa Al-Juwayniy As- Shafiy ndani ya kitabu Faraidu As-Samtwayni, kutoka kwa Ibnu Abbas kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwa yeye alisema: “Mimi ni bwana wa manabii na Ali bin Abu Talib ni bwana wa mawasii, na bila shaka mawasii wangu baada yangu ni kumi na wawili, wa kwanza wao ni Ali bin Abu Talib na wa mwisho wao ni Mahdi.”30

Kuanzia hapa ndipo baadhi ya wahakiki wakaona kuwa, huenda ndani ya jibu la baba kuna opotoshaji. Imesemwa na vitabu vya Hadithi kuwa, pindi baadhi ya maneno ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yalipokosa kusikika kwa Jabir bin Samara, na akawa amemuuliza baba yake kuhusu maneno yaliy- ofichikana kwake, baba yake alimjibu kuwa (s.a.w.w.) amesema: “Wote ni kutoka kwa makurayshi.”

Kwa sababu riwaya imetoa sababu iliyosababisha jibu lisisikike, ikasema: “Kisha jamaa wakainua sauti na kuongea.” Na “Watu wakapiga kelele.” Na “Akasema neno ambalo watu walinifanya nisilisikie.” Na “Watu wakainua sauti hivyo sikusikia alilosema.” Na “Watu wakatoa takbira na kupiga kelele.” Na “Watu wakaanza kusimama na kukaa.” Sababu zote hizi hazi- afikiani na ibara ambayo mpokezi hakuisikia, kwa sababu kuufanya ukhalifa uwe kwa makurayshi ni jambo linalowapendeza wala halipelekei fujo na kelele, na hivyo dhana inayonasibiana na hali hii iliyoelezwa ni ile ya kuwa uimamu umekabidhiwa kwa kundi maalumu na si makurayshi.

Hili ndilo alilolisema Al-Qunduz ndani ya kitabu chake Yanabiul- Mawaddah kwani amesema, ibara aliyoitamka Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ni “Wote ni kutoka kwa wana wa Hashim.”31

Baada ya kubainika kuwa upande mmoja tafsiri ya “ufafanuzi wa hali ya mustakabali” imefeli kwenye Hadithi ya uimamu wa maimamu kumi na wawili, na upande wa pili umethibiti ukweli wa tafsiri ya “ufafanuzi wa imani” na upande wa tatu limethibiti jina la Imam Mahdi ndani ya orodha ya mfululizo wa maimamu wa Ahlul-Bait na kuwa yeye ni Imam wa kumi na wawili ambaye kupitia kwake Mwenyezi Mungu ataitengeneza ardhi baada ya kuwa imejaa uharibifu, basi baada ya hapo haibaki shaka yoyote juuu ya kuthibiti wazo la imani ya uwepo wa Mahdi anayehimizwa na madhehebu ya Ahlul-Bait (a.s.).

Kwa sababu uhusiano wa ndani kati ya suala la uimamu wa maimamu kumi na wawili na suala la Mahdi unapelekea yahamishiwe kwenye suala la Mahdi matokeo matatu yaliyopatikana ndani ya uchambuzi.

Hivyo ikife- li tafsiri ya “ufafanuzi juu ya hali ya mustakabali” kwenye uimamu wa maimamu kumi na wawili maana yake ni kuwa tafsiri hii pia imefeli kwenye suala la Mahdi. Kama ambavyo ikithibiti sababu ya kisiasa katika kuzuka tafsiri hii kwenye uimamu wa maimamu kumi na wawili itamaan- isha imethibiti sababu hiyo kwenye suala la Mahdi.

Kwani madhehebu ya Sunni kama ilivyoifanya Hadithi ya ukhalifa wa makhalifa kumi na wawili kuwa ni habari juu ya hali ya mustakabali ili iwe ni sehemu ya usahihi wa nadharia ya uchaguzi wa sakifa, ukhalifa na uha- lali wake, basi ndivyo hivyo hivyo imeona dharura ya kuunga suala la Mahdi kwenye tafsiri ya “ufafanuzi juu ya hali ya mustakabali”, wame- fanya hivyo ili kukimbia imani ya uimamu wa Ahlul-Bait (a.s.) na kutosi- hi utaratibu wa ukhalifa. Kama ambavyo kuthibiti ukweli wa tafsiri ya “ufafanuzi juu ya imani” kwenye Hadithi ya uimamu wa maimamu kumi na wawili kunamaanisha ni kuthibiti ukweli kuhusu wazo la imani ya uwepo wa Mahdi.

---

1. Rejea Muujamu Ahadithil-Imam Al-Mahdiy: Juz 1 kwenye Hadithi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

2. Musnad Imam Ahmad 1: 84, Hadithi ya 646. Ibnu Abu Shaybah 8: 687, kitabu cha 40, mlango wa 2, Hadithi ya 190. Ibnu Majah na Naimu bin Hammad ndani ya Al-Futunu kutoka kwa Ali (a.s.) amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu ame- sema: “Mahdi ni kutoka kwetu Ahlul-Bait, Mwenyezi Mungu atamtoa ndani usiku mmoja.”. Rejea Sunan Ibnu Majah 2: 1367, Hadithi ya 4085. Al-Hawi Al-Fatawa cha As-Suyuti 2: 213 na 215, humo mna: “Ameitoa Ahmad na Ibnu Shaybah na Abu Daud kutoka kwa Ali kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: “Hata kama ulimwengu utabakiwa na siku moja, ni lazima Mwenyezi Mungu atamleta mtu kutoka ndani ya kizazi changu, atakeyeujaza uadilifu kama utakavyokuwa umejaa dhulma.” Rejea Sahih Sunanul-Mustafa 2: 207. Rejea Muujamu Ahadithil- Mahdi 1: 147 na unaofuata, kwani amenukuu Hadithi nyingi zenye maana hii kutoka kwenye Sahih Sita na Masanid. Rejea Mawsuatul-Imam Al-Mahdi: Usanifu wa Mahdi Faqihi Imaniy, juzuu ya kwanza, humo mna nakala halisi zili- zonukuliwa kutoka ndani ya makumi ya vitabu vya kisuni na wasimulizi wao zik- ihusu Mahdi, sifa zake na yanayomhusu, na humo mna nakala halisi ya muhadhara wa Sheikh Al-Ibad kuhusu Hadithi na athari zinazomhusu Mahdi (a.s.).

3. Al-Hawi Lil-Fatawa cha As-Suyutiy Jalalud-Dini 2: 214. Amesema: Abu Daud ametoa na Ibnu Majah na At-Tabaraniy na Al-Hakim kutoka kwa Ummu Salamah alisema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akisema: “Mahdi ni kutoka ndani ya kizazi changu kutoka kizazi cha Fatima.”. Rejea Sahih Sunanul-

4. Hadithi zinazosema kuwa Mahdi ni kutoka kizazi cha Husein (a.s.) kama ilivyo ndani ya vyanzo vifuatavyo kama ilivyonukuliwa ndani ya Muujamu Ahadithil- Mahdi, navyo ni: Al-Arbauna Haditha cha Abu Naim Al-Isfahaniy kama ilivyo ndani ya Uqad Ad-Durar cha Al-Muqadasiy As-Shafiiy. Na ameitoa At-Tabaraniy ndani ya kitabu Al-Awsat kama ilivyo ndani ya Al-Manaru Al-Munir cha Ibnu Al- Qayyim na ndani ya kitabu As-Siratu Al-Halbiyah 1: 193. Na ndani ya kitabu Al- Qawlu Al-Mukhtasar cha Ibnu Hajar Al-Haythamiy. Rejea Muntakhabul-Athar cha Shaikh Lutfullah As-Swafiy zile alizozinukuu kutoka kwenye vitabu vya Kishia. Rejea dalili za udhaifu wa riwaya isemayo kuwa yeye ni kutoka kizazi cha Imam Hasan, kitabu cha As-Sayyid Al-Amidiy Difau Anil-Kafiy 1: 296

5. Rejea riwaya ambayo inaelezea kuwa yeye ni wa tisa kutoka kizazi cha Husein (a.s.) ndani ya kitabu Yanabiul-Mawaddah cha Al-Qunduziy Al-Hanafiy: 492 na ndani ya kitabu Maqtalul-Imam Al-Husein cha Al-Khawarazamiy 1: 196. Faraidu As-Samtwayn cha Al-Jawniy As-Shafiiy 2: 310 – 315, Hadithi ya 561 – 569. Rejea Muntakhabul-Athar cha Allamah Shaikh As-Swafiy kwani yeye kazitoa kwa njia za madhehebu zote mbili.

6. Hadithi: “Makhalifa baada yangu ni kumi na wawili wote ni kutoka kwa Makurayshi.” Au “ Dini hii itaendelea kusimama mpaka itawaliwe na kumi na wawili wote kutoka kwa Makurayshi.”. Hadithi hii ni mutawatiri, imepokewa ndani ya Sahihi sita na Masanid kwa njia mbalimbali japokuwa zinatofautiana kidogo katika matamshi. Ndio wametofautiana katika tafsiri na

hivyo waka- hangaika. Rejea Sahih Bukhari 9: 101, kitabu cha hukumu, mlango wa kuacha Khalifa. Sahih Muslim 6: 4, kitabu cha alama, mlango wa kuacha Khalifa. Musnad Ahmad 5: 90, 93, 97.

7. Rejea kitabu Al-Ghaybatul-Kubra cha As-Sayyid Muhammad As-Sadri: 272 na kuendelea.

8. Rejea At-Taju Al-Jamiu Lil-Usul 3: 40, amesema: "Imepokewa na mashekhe wawili na Tirmidhi." Kuhusu uhakiki wa Hadithi, njia zake za upokezi na senten- si zake rejea kitabu Al-Imam Al-Mahdi cha Ali Muhammad Ali Dakhil.

9. Sahih Bukhar: Juzuu ya tatu 9: 101, kitabu cha hukumu, mlango wa ukhalifa, chapa ya Daru ihyaut-Turathil-Arabiy – Beirut.

10. Rejea At-Taju Al-Jamiu Lil-Usul 3: 40, ameongezea kwenye Hadithi kwa kusema: "Imepokewa na mashekhe wawili na Tirmidhi." Pembezoni akasema: "Ameipokea Abu Dawdi ndani ya kitabu cha Mahdi kwa tamko: "Dini hii itaen- delea kusimama mpaka mtawaliwe na Makhalifa kumi na wawili…."" Na rejea Sunan Abi Dawdi 2: 207.

11. Rejea At-Taju Al-Jamiu Lil-Usul 3: 40, ameongezea kwenye Hadithi kwa kusema: "Imepokewa na mashekhe wawili na Tirmidhi." Pembezoni akasema: "Ameipokea Abu Dawdi ndani ya kitabu cha Mahdi kwa tamko: "Dini hii itaen- delea kusimama mpaka mtawaliwe na Makhalifa kumi na wawili…."" Na rejea Sunan Abi Dawdi 2: 207.

12. Rejea At-Taju Al-Jamiu Lil-Usul 3: 40, ameongezea kwenye Hadithi kwa kusema: "Imepokewa na mashekhe wawili na Tirmidhi." Pembezoni akasema: "Ameipokea Abu Dawdi ndani ya kitabu cha Mahdi kwa tamko: "Dini hii itaen- delea kusimama mpaka mtawaliwe na Makhalifa kumi na wawili…."" Na rejea Sunan Abi Dawdi 2: 207.

13. Musnad Imam Ahmad 6: 99, Hadithi ya 20359.

14. Al-Mustadrak Alas-Sahihayni 3: 618.

15. Anaashiria kauli ya Mwenyezi Mungu: "Hatamki kwa matamanio.* Ila ni wahyi unaofunuliwa." Sura Najmu: 3 – 4.

16. Hadithi hii tayari tumeshaitoa huko nyuma.

17. Bahthu hawlal-Mahdi cha As-Sayyid As-Shahid As-Sadri: 105 – 107, uhaki- ki wa Dr. Abdul-Jabar Shirara.

18. Baadhi ya Wanachuoni baada ya kukongamana juu ya usahihi wake wame lazimika kuioanisha na mifano ambayo haiwezekani kuikubali, bali baadhi yake kamwe akili haiwezi kuiridhia, kama Yazid bin Muawiya fasiki wa waziwazi ambaye alitoka ndani ya dini na kukufuru, au mwingine mfano wake.

19. Sahih Muslim 6, kitabu cha alama, mlango wa watu wawafuate makurayshi.

20. Rejea Sahih Bukhar 4: 164, kitabu cha hukumu, mlango wa ukhalifa. Musnad Ahmad 6: 94, Hadithi ya 325, 20366, 20367, 20416, 20443, 20503 na 20534. Sunan Abi Dawd 4:106 / 4279 – 4280. Al-Muujam Al-Kabir cha At-Tabaran 2:238/1996. Sunan At-Tirmidhi 4: 501. Mustadrakul-Hakim 3:618. Hilyatul-Awliyai cha Abu Naim 4:333. Fat'hul-Bari 13:211. Sahih Muslim sherehe ya An- Nawawi 12:201. Al-Bidayah Wan-Nihayah cha Ibnu Kathir 1:153. Tafsir Ibnu Kathir 2:24 kwenye tafsiri ya Aya ya 12 ya Sura Maida. Kitabus-Suluki fiduwalil-Muluki cha Al-Maqrizi 1: 13 – 15, sehemu ya kwanza. Sherehe ya Sunan Abi Dawd 11: 363, iliyofanywa na Al-Hafidh Ibnu Qayyim Al-Jawziyah, sherehe ya Hadithi ya 4259. Sherehe ya Al-Aqidah At-Tawahiyah 2:736. Al-Hawi Lil-Fatawa cha As-Suyutiy 2:85. Awnul-Maabud Sharhu Sunan Abi Dawd cha Al-Adhim Abad 11:362, sherehe ya Hadithi ya 4259. Mishkatul-Maswabih cha At-Tabrizi 3:327, 5983. As-Silsilatu As-Sahiha cha Al-Abaniy, Hadithi namba 376. Kanzul-Ummal 12:32, 33848, na 12:33/33858, na 12:34/33861. Hadithi hii pia ime- tolewa na wasimulizi wa kishia akiwemo As-Saduq ndani ya kitabu chake Kamalud-Din 1:272, na Al-Khisal 2:469 na 475, ndani ya kitabu chake Ihqaqul- Haqi 13: 1 – 50 amefatilia njia za upokezi wake na maswahaba walioipokea.

21. Tafsir Ibnu Kathir 2: 34, tafsiri ya Aya 12 ya Sura Maida

22. Sherehe ya Al-Aqidah At-Tahawiyah cha Kadhi Ad-Damashqiy 2: 736.

23. Awnul-Maabud katika kusherehesha Sunan Abi Dawd 11: 246, sherehe yaHadithi ya 427, kitabu cha Mahdi, chapa ya Darul-Kutubi Al-Ilmiyah.

24. Awnul-Maabud katika kusherehesha Sunan Abi Dawd 11: 245.

25. Awnul-Maabud katika kusherehesha Sunan Abi Dawd 11: 244.

26. Al-Hawi Lil-Fatawa 2: 85.

27. Kanzul-Ummal 12: 34, Hadithi ya 33861, Ibnu An-Najar ameitoa kutoka kwa Anas.

28. Kanzul-Ummal 12: 32, Hadithi ya 33848.

29. Rejea kitabu Al-Ghadir cha Al-Allamah Al-Amin 1: 26 – 27, amelitaja hilo akiwa amelitoa kwenye vitabu vya masunni.

30. Faraidu As-Samtwayni 2:313, Hadithi ya 564.
31. Yanabiul-Mawaddah 3: 104, mlango wa 77.

Sura Ya Pili

Sifa mahususi kuhusu uwelewa wa Mahdi kwa Ahlul-Bait wenyewe (a.s.).

Baada ya kutimia uthibitisho wa kiimani juu ya uwelewa wa Mahdi kwa madhehebu ya Ahlul-Bait (a.s.) sasa tunaingia hatua mpya ya uchunguzi, nayo ni hatua ya uchunguzi juu ya sifa muhtasi zinazohusu uwelewa huu ili tuweze kuthibitisha kuwa zenyewe ni sifa halisi kivitendo na zina uwepo wa nje kihistoria na kisharia, na kuwa kuziamini sifa hizo hakupelekei kutia doa imani wala kutengana na historia. Na sifa hizo ni kama zifuata- zo:

Sifa ya kwanza: Kuzaliwa kwa Imam Mahdi kulitimia katika mazingira ya siri yaliyokuwa ni lazima kutimia.

Ukithibiti uwelewa wa wazo la Mahdi kwa mujibu wa Ahlul-Bait basi inabainika kuwa miongoni mwa sifa barizi mno za lazima za uwelewa huu ni kuzali kwa Imam wa kumi na wawili kuwe kumeambatana na siri na ufi- cho ili baada ya hapo iwezekane kwake ghaibu na kujificha mbali na macho akiwa sehemu yenye amani atakayoichagua Mwenyezi Mungu kwa ajili yake mpaka pale atakapomruhusu kudhihiri.

Hiyo ni kwa kuzingatia kuwa yeye ndiye nyota ya mwisho katika mbingu ya uimamu na Imam ambaye waisilamu hawana Imam mwingine baada yake. Hivyo maana hii inalazimu kupatikana maisha ya uficho, umri mrefu na mazazi ya siri ili nafasi ya uimamu iendelee kutumikiwa muda wote na Imam miongoni ma maimamu kumi na wawili (a.s.) aliye hai aliye ghaibu.

Basi haifai kabisa kusema kuwa: Kwa nini kuzaliwa kwa Imam na kuwe- po kwake baada ya baba yake hayakuwa ni mambo ya wazi yanayoshuhudiwa na kuguswa na kila anayetaka kusadikisha? Kwa sababu laiti ingelikuwa hivyo basi ghaibu na kujificha mbali na macho visingekuwa rahisi kwake kwa sababu yeye ndiye Imam wa kumi na waw- ili, na hatimaye maimamu wangekuwa wengi kuliko idadi hii, na suala hili linapingana na dalili zilizotoka kwa Mtume zilizotajwa mwanzo. Hivyo mazazi ya siri ni miongoni mwa mambo ya lazima yanayotokana na hali halisi ya dalili hizo.

Suala hili linabainisha kuwa kuthibitisha uwepo wa nje wa kadhia ya kuza- liwa Imam Mahdi, kuwepo kwake na maisha yake hakuwezi kukomea tu kwenye uchunguzi wa kihistoria madamu tu tunaamini tangu mwanzo kuwa kadhia hiyo imeambatana na usiri na ufichaji wa kiwango cha juu sana, bali

wenyewe ni uthibitisho wa kiakida ndani ya historia ambao ndani yake akida ina nafasi ya msingi, wakati historia yenyewe ina nafasi ya kukamilisha tu.

Kwa sababu sisi tuna yakini tangu mwanzo kuwa wapo wakanushaji wa kadhia hiyo na wenye shaka nayo maadamu tu kadhia ni ya siri iliyofich– wa, na wenye kuitambua ni watu wachache kiasi kwamba inawapa mwanya wengine kuikanusha na kuitilia shaka maadamu tu wako mbali na hali halisi iliyo ya siri iliyofichwa, hali hiyo ni hata kama watakuwa ni ukoo wa karibu na Imam na wafuasi wa dhati, kiasi kwamba lau mtu atawahoji kuhusu kuzaliwa kwa Imam Mahdi, kuwepo kwake na maisha yake wangekanusha, na wao wangewanukulia watu kuwa hawajamwona na wala hawajasikia habari za kuzaliwa na kuwepo kwake.

Hivyo sisi hatuzungumzii suala la kimaada lenye kutambulika vipengele vyake vyote kwa njia ya milango ya fahamu, linalo tutaka tufuate nukuu kamili za historia ili katika uthibitisho wake na ukanushaji wake tuwa– tegemee wanahistoria na wapokezi, hapana si hivyo, bali sisi kimsingi tunazungumzia kadhia ya ghaibu, isipokuwa tu ughaibu huo si ule usio na mipaka, bali wenyewe ni ule wenye miale yenye kutambulika kwa kupitia milango ya fahamu unaofahamika na watu maalumu waliyoteuliwa, hivyo wao wameshuhudia mazazi yake na kuyathibitisha na wameshuhudia ghaibu ndogo na wameithibitisha na wakashuhudia ghaibu kubwa kisha wakaithibitisha. Na kwa ajili hii ndio maana tukasema kuwa uwelewa wa wazo la uwepo wa Mahdi kwa mujibu wa madhehebu ya Ahlul–Bait (a.s.) ni uwelewa wa kiitikadi.

Hii ina maana kuwa kukanusha kwa wakanushaji katika kadhia ya Imam Mahdi hakuwi hoja ya kihistoria ya kimantiki inayoweza kuthibitisha kutokuwepo kwake (a.s.) maadamu tu tumeshaamini tangu mwanzo kuwa kadhia hii ni kadhia ya siri iliyofichwa. Dharura ya uchunguzi wa historia ni kuthibitisha uwepo wa yule aliyemwona Mahdi (a.s.) na akasikia habari za kuwepo kwake na akaziamini, hilo ni bila kujali ukanushaji wa wakanushaji, ukanushaji ambao ni suala la kawaida kupatikana kwenye kadhia ya siri iliyofichwa.

Basi kuanzia hapa tutazama ndani ya uchambuzi wa aina wawili: Kwanza uchambuzi juu ya ushahidi unaothibitisha kuzaliwa kwa Imam na kuende– lea kwake kuwepo. Uchambuzi mwingine ni kuzijadili dalili za wenye kumkanusha (a.s.).

Vielelezo vya kihistoria vinavyothibitisha uwepo wa Imam Mahdi (a.s.)

Upande huu ni mpana mno umejaa namba nyingi sana za vielelezo vya kihistoria, nasi tunavihariri katika nukta mbalimbali:

1. Uthibitisho wa Imam Hasan Al–Askarii (a.s.) kuhusu kuzaliwa mwanae

Imam Mahdi (a.s.):

Katika hilo kuna Hadithi nyingi zilizothibitishwa na Shia na wapokezi wake, nasi tunanukuu baadhi tu:

Hadithi iliyopokewa kutoka kwa Muhammad bin Yahya kutoka kwa Ahmad bin Is'haqa kutoka kwa Abu Hashim Al-Jafariy, amesema: "Nilimwambia Abu Muhammad (a.s.): Heshima yako inanizuia nisiku-ulize, je unaniruhusu nikuulize? Akasema: "Uliza." nikasema: Ewe bwana wangu! Je, una mtoto wa kiume? Akasema: "Ndiyo."1

Ndani ya Hadithi hii kuna njia ya upokezi na madhumuni vinavyoji- tosheleza, kwani ni hivi hapa vitabu vya wapokezi vinathibitisha heshima ya Muhammad bin Yahya Abu Jafar At-Tar Al-Qummiy ambaye kaburi lake mpaka leo bado ni maarufu na mashuhuri watu wakilizuru. Pia vinathibitisha hadhi ya juu ya Ahmad bin Is'haqa bin Abdullah bin Saad bin Malik bin Al-Ahwas Al-Ash'ari Abu Ali Al-Qummiy kwa Imam Hasan Al-Askarii (a.s.). Pia vinathibitisha nafasi ya Daud bin Al-Qasim Ibnu Is'haqa bin Abdullah bin Jafar bin Abu Talib Abu Hashim Al-Jafariy.... Kisha tazama uchache wa mtiririko wa wapokezi katika njia ya upokezi wa Hadithi hii, Hadithi ambayo inaonyesha hali ya wahusika kwa ule ufupi wa njia ya upokezi ambao unaheshimika kama ushahidi unaoipa nguvu Hadithi hii.

2. Uthibitisho wa Al-Qabilah

Yeye ni dada wa Imam na shangazi wa Imam na binti wa Imam, anatokana na ukoo wa Ali uliotoharika. Hakimah binti Muhammad Al-Jawwad ni dada wa Imam Al-Had na shangazi wa Imam Al-Askarii, yeye amethibitisha waziwazi kuwa alishuhudia kuzaliwa kwa Imam Mahdi (a.s.) ndani ya usiku aliyozaliwa2, na yeye ndiye aliyesimamia uzazi wa Nargis mama wa Imam Mahdi (a.s.) kwa kupata idhini kutoka kwa baba yake Hasan Al-Askarii (a.s.)3.

3. Uthibitisho wa watu mbalimbali waliomwona Imam (a.s.):

Hapa tuna orodha ndefu ya majina ya watu waliomwona Imam Mahdi na wakakutana naye na wakathibitisha kuwa wamemwona, orodha hiyo ime- sajiliwa na historia na baadhi ya waandishi wameisajili ndani ya vitabu vyao muhtasi, mfano kitabu *"Tabsiratul-Waliy Fiman'raa Al-Qaimu Al-Mahdiy"* cha Sayyid Hashim Al-Bahrani, humo amewataja watu sabini na tisa waliothibitisha kuwa wamemwona Imam (a.s.) utotoni mwake au kipindi cha ghaibu ndogo, na ametaja majina ya rejea alizozitegemea kati- ka hilo.

Sheikh Abutalibi At-Tajlili At-Tabrizi Zahau yeye amehesabu watu mia tatu na nne waliomwona Imam (a.s.) na wakathibitisha kumwona4.

Sheikh As-Suduq aliyefariki mwaka 381 A.H. na aliyeishi zama za ghaibu ndogo ya Imam Mahdi (a.s.) yeye amehesabu majina ya watu sitini na nne waliothibitisha kuwa wamemwona Imam (a.s.), na wengi miongoni mwao walikuwa mawakala wake5, na wenyewe ni kutoka miji mbalimbali.

Miongoni mwa mawakala wake ni: Kwa watu wa Adhribayjani ni Al- Qasim bin Al-Alau. Kwa watu wa Ahwaz ni Muhammad bin Ibrahim bin Mahziyar. Kwa watu wa Baghdad ni Hajiz Al-Balaliy, Uthman bin Said Al-Amriy, Muhammad bin Uthman bin Said Al-Amriy na Al-Atar. Kwa watu wa Kufa ni Al-Asimiy. Kwa watu wa Qum ni Ahmad bin Is'haqa. Kwa watu wa Nisabur ni Muhammad bin Shadhan. Kwa watu wa Hamdan ni Al-Basamiy, Muhammad bin Abu Abdullah Al-Kufiy Al-Asadiy na Muhammad bin Salih.

Ama wengine waliomwona wasokuwa mawakala wake miongoni mwao ni: Kutoka Isfihan ni Ibnu Bashadhalah. Kutoka Ahwaz ni Al-Huswayniy. Kutoka Baghdad ni Ahmad bin Hasan, Is'haqa mwandishi wa ukoo wa Nawbakhat, Abu Abdullah Al-Khaybariy, Abu Abdullah bin Farukh, Abu Abdullah bin Al-Kindiy, Abul Qasim bin Abu Halis, Abul Qasim bin Dabis, Masrur At-Tabakh mtumwa wa Abu Hasan (a.s.), An-Nayliy na Harun Al-Fazariy.

Kutoka Daynawar ni Ahmad mtoto wa kaka yake na Hasan bin Harun na ami wa Hasan bin Harun. Kutoka Ray ni Abu Jafar Ar-Rafau, Ali bin Muhammad, Al-Qasim bin Musa, mtoto wa Al-Qasim bin Musa, Abu Muhammad bin Harun na Muhammad bin Muhammad Al-Kulayniy.

Kutoka Kazwin ni Ali bin Ahmad na Murdasi. Kutoka Qum ni Hasani bin An-Nadhru, Husayn bin Yaaqub, Ali bin Muhammad bin Is'haq, Muhammad bin Is'haq na Muhammad bin Muhammad. Kutoka Misri ni Abu Rajai. Kutoka Nasibayn ni Abu Muhammad bin Al-Wajnau An- Naswibiy. Kutoka Hamdan ni Jafar bin Hamdan, Muhammad bin Kashmirda na Muhammad bin Harun. Kutoka Yemen ni Ibnu Al-Aajamiy, Al-Jafariy, Hasani bin Al-Fadhlu Ibnu Yazid, baba yake Al-Fadhlu bin Yazid na Shamshati. Pia amewataja waliomwona kutoka Shahruzur, Swaymara, Faris, Qabis na Murwu.

Je, akili inakubali kuwa hawa wote walikubaliana na kuafikiana juu ya kuzua uongo? Ilihali miongoni mwao wapo wasimulizi waaminifu ambao vitabu vya wapokezi wa Hadithi vimethibitisha waziwazi uaminifu wao?

4. Utawala wa koo wa Abbas ulicheza mchezo mchafu juu ya tukio hili

Bila shaka utawala wa ukoo wa Abbas baada ya kufariki Imam Hasan Al- Askarii uliamiliana na familia yake muamala unaoonyesha hofu yao dhidi ya mtoto hatari aliyefichwa dhidi yao, hivyo wakaanza kumtafuta kwa kila nguvu na njia waliyo nayo, kiasi kwamba Al-Muutamid Al-Abbasiy aliye- fariki mwaka 279 A.H alimwamuru mkuu wake wa polisi kuipekua nyum- ba ya Imam Hasan Al-Askarii msako mkali sana huku wakimsaka Imam Mahdi. Akaamuru majirani wa Abu Muhammad wawekwe rumande na familia yake ikamatwe, alifanya hivyo huku akisaidiwa na Jafar mwongo, kwa ajili hiyo watu wa karibu wa Abu Muhammad wakapatwa na kila tati- zo kuanzia kukamatwa, kuwekwa mahabusu, kutishwa, kuvunjiwa heshi- ma na kudhalilishwa.6

Haya yote yalifanywa Imam akiwa na umri wa miaka mitano, wala Al- Muutamid hakujali umri baada tu ya kujua kuwa kijana huyu ndiye Imam Mahdi atakayeangusha jukwaa la muovu kutokana na habari zilizoenea na kutapakaa kuwa Imam wa kumi na wawili wa Ahlul-Bait ataijaza dunia usawa na uadilifu

kama itakavyokuwa imejaa dhuluma na ujeuri, hivyo msimamo wake dhidi ya Mahdi ni sawa na msimamo wa Firaun dhidi ya Musa (a.s.) ambaye mama yake alimweka ndani ya mto akiwa mchanga kwa ajili ya kumuogopa Firaun.

Si Al–Muutamid pekee ndiye aliyekuwa amejua ukweli huu bali hata Al– Muutazu na Al–Muhtad waliujua kabla yake, kwa ajili hii Imam Hasan Al– Askari alikuwa katika tahadhari sana ili habari za kuzaliwa Imam Mahdi zisitapakae isipokuwa kati ya watu wateule kutoka kwa mashia wake na wafuasi wake.

Harakati za utawala zimefichua kuwa wenyewe na watu wengine wote walitambua vizuri kuwa Hadithi ya Jabir bin Samra haiwahusu wao wala yeyote aliyetangulia miongoni mwa ukoo wa Umaiya, bali mfano halisi pekee wa Hadithi hiyo ni watu wa nyumba ya utume ambao ni shukio na teremkio la ufunuo.

Kama si hivyo basi ni hatari gani kutoka kwa mtoto asiyevuka umri wa miaka mitano inatishia utawala wao? Kama si kule kuamini kuwa mtoto huyu ndiye yule Mahdi aliyezungumziwa ndani ya Hadithi mbalimbali mutawatiri!

Mmoja wa watafiti anasema: “Ingekuwa kweli hajazaliwa basi kuna maana gani kuwaweka majirani rumande na kutuma vikosi kwenda kuwapekua wanawake wajawazito na kuwapeleleza muda mrefu usiokubalika, kwani mwingine alikuwa chini ya upelelezi muda wa miaka miwili, yalifanywa yote haya huku maswahaba wa Imam Askari wakiteswa na kutumiwa majasusi ili kupeleleza habari za Mahdi (a.s.) na mara kwa mara nyumba zikivamiwa?

Kisha kwa nini utawala haukuridhika na dai la Jafar kuwa kaka yake (a.s.) amefariki bila kuacha mtoto? Hivi haikuwa inatosha kumpa haki yake ya mirathi na mambo yote yaishe kuliko harakati hizi za kipumbavu ambazo zinaonyesha jinsi ulivyokuwa na woga na hofu dhidi ya mwana wa Hasan (a.l.f.s.)?!!

Ndiyo, inaweza kusemwa kuwa nia ya utawala ilikuwa ni kumpa kila mwenye haki haki yake na hiyo ndiyo sababu iliyoupelekea kufuatilia ili kujua uwepo wa mtoto wa kiume ili Jafar asimiliki mirathi peke yake kwa ushahidi wake tu.

Tunasema: Haikufaa kwa utawala wa zama hizo kufatilia jambo hili kwa vitendo hivi vyenye kutia shaka, bali ilipasa Khalifa wa ukoo wa Abbas aliache dai hilo la Jafar mwongo mikononi mwa makadhi, na hasa ukizinga– tia kuwa suala lenyewe ni mirathi, suala ambalo hutokea kila siku mara nyingi, na hapo ingekuwa ni jukumu la kadhi muhusika kufungua mlango wa kuletwa shahidi wa kuthibitisha, kwa mfano angeitwa shangazi yake na Imam Hasan Askari (a.s.) na mama yake na watu wa ukoo wa Hashimu walio karibu na Hasan Askari na kisha asikilize kauli zao achunguze ushahidi wao na hatimaye amaleze kila kitu.

Lakini suala hili kufika kwa mtu wa juu kiutawala na kwa haraka ya namna hii hata kabla Imam Hasan Al–Askari hajazikwa huku suala likitoka kwenye uwezo wa Mahakama ilihali ndiyo yenye jukumu hilo, na kisha utawala unalikabili kwa nguvu kama tuliyoifafanua mwanzo, hayo yote yanathibitisha kwa yakini

kuwa utawala ulikuwa ukiamini kwa yakini kabisa kuwa Mahdi tuliyeahidiwa ndiye mzunguko wa mwisho wa cheni toharifu ambayo haiwezi kukatika kwa kufariki Imam wa kumi na moja, hasa baada ya kauli ya (s.a.w.w.) "Hivyo viwili – Kitabu na Kizazi – hav– itoachana mpaka vitakaponifikia kwenye Hodhi." kuenea kwa watu wote.

Kwani kutokuzaliwa Mahdi au kutoendelea kuwa hai maana yake ni kutoweka kwa kizazi, na hii ni kauli isiyosemwa na yeyote yule anayejiita kiongozi wa waumini miongoni mwa wana wa Abbas, kwa sababu kauli hiyo ni kumkadhibisha Mtukufu Mtume wetu (s.a.w.w.) bali haisemwi na mwisilamu yeyote ila yule tu asiyejali ukadhibishaji huu au mwenye kuji– danganya kuwa anaawili Hadithi na kuyapeleka malengo ya Hadithi kwenye kitu ambacho hakijaletewa hoja yoyote ya wazi."[7]

5. Wanachuoni wa Sunni wamekiri kuwa Imam Mahdi (a.s.) ameshaz– aliwa.

Sayyid Thamir Al–Amidiy amezungumzia suala hili akasema: "Kauli za kukiri za Wanachuoni wa sharia, wafasiri, wanahistoria, watafiti, wafasihi na waandishi wa kisunni zimefikia zaidi ya mia moja, wote wakikiri wazi– wazi kuwa Imam Mahdi (a.s.) ameshazaliwa. Zaidi ya nusu yao wametam– ka waziwazi kuwa Imam Muhammad bin Hasan Al–Mahdi (a.l.f.s.) ndiye Imam tuliyeahidiwa kuwa atadhihiri mwishoni mwa zama.

Kauli hizi za kukiri zimepangwa kulingana na vifo vya wenye nazo, hivyo tumezikuta zimeungana kizama kiasi kwamba haishindikani mwenye tamko la sasa kuwepo zama za mwenye tamko lililopita, hivyo ni kuanzia zama za ghaibu ndogo mpaka leo hii, ishaallah tutataja kauli za baadhi yao ambazo tumezipata ndani ya vitabu vyao pindi zamu yao itakapofika, na kwa wengine tutaishia kutaja majina yao tu bila kugusia kauli zao hiyo ni kutokana na kushindikana kuzinukuu katika sura hii.

Kauli zao zimefikia ishirini na tisa huku ya mmoja kati yao ikiwemo ndani ya kitabu "Ilzamun–Naswibu" kwenye kurasa zaidi ya mia moja.[8] Je hali ingekuwaje laiti angesajili kauli zao wote? Zaidi ya hapo ni kuwa tutakayo itaja kwenye matamshi bila kuonyesha rejea yake kwenye pambizo ni dalili kuwa tumeichukua kutoka kwenye vitabu vya Shia Imamiya ambavyo vimetangulia kuzungumzia suala hili, na tutakazania kusajili namba ya juzuu, namba ya kurasa, sehemu na mwaka wa chapa.

Kitabu kikubwa mno katika mlango huu ni kitabu "Al–Mahdiyyu Al– Muntadhar Finahjil–Balagha" cha Sheikh Mahdiyyu Faqihi Iymaniy, ambaye humo ametaja wapokezi mia wawili na wawili miongoni mwa wapokezi wa kisuni ambao wamekiri hilo[9] huku akiishia kutaja majina yao na vitabu vyao kwa kuainisha juzuu zake pamoja na kurasa zake bila kugusia kauli zao.

Nyakati nyingine alilazimika kuainisha kwa umakini kiunganishi kati yake na wao, na yaliweza kumpita karibuni majina thelathini. Sana tumemtege– mea yeye na wala hatukurudia tena ili kutafuta chochote kilichompita kwani tayari kuna mwingine asiyekuwa mimi alisharudia na kukusanya kile kilichompita[10], akarudia kwa mzunguko katika dalili hii huku akiishia kukusanya na kupangilia kulingana na karne."[11]

Kisha akataja majina mia moja ishirini na nane ya waandishi miongoni mwa waandishi wa kisunni

ambao ndani ya baadhi ya vitabu vyao wamem- taja Imam Mahdi kwa kichwa cha habari: Imam wa kumi na wawili mion- goni mwa maimamu wa Ahlul-Bait (a.s.). Miongoni mwa waandishi hao wamo walioishi zama za kuzaliwa kwake na zama za ghaibu ndogo, ushahidi wa hawa una hadhi maarufu ya kihistoria.

Miongoni mwa hao ni:

1. Abubakri Ar-Riwayaniy, Muhammad bin Harun aliyefariki mwaka 307 A.H ndani ya kitabu chake "Al-Musnad".

2. Ahmad bin Ibrahim bin Ali Al-Kindiy, yeye ni kati ya wanafunzi wa Ibnu Jarir At-Tabari aliyefariki mwaka 310 A.H.

3. Muhammad bin Ahmad bin Abu Thalji, Abubakri Al-Baghdadiy aliye- fariki mwaka 322 A.H. ndani ya kitabu "Mawalidul-Aimah", hiki kimechapwa ndani ya kitabu "Al-Fusulul-Asharat Fil-Ghaybah" cha Sheikh Al-Mufid, pamoja na kitabu "Nawadiru Ar-Rawandiy kili- chochapwa Najaf tukufu mwaka 1370 A.H. Na miongoni mwa Wanachuoni wakubwa waliokuwa karibu na zama za kuzaliwa kwake ni Al-Khuwarazimiy aliyefariki mwaka 387 A.H. ndani ya kitabu chake "Mafatihul-Ulumi: 32 na 33" chapa ya Lidan mwaka 1895 A.D.

Hebu tujadiliane na wakanushaji

Kutokana na maelezo yaliyotangulia imebainika kuwa suala la Mahdi ni suala la kiitikadi kabla halijakuwa la kihistoria, na dalili ya kulithibitisha ni ya kiitikadi kabla haijakuwa ya kihistoria. Pia imebainika kuwa baadhi ya dalili za kihistoria zimelithibitisha na pia imebainika kuwa kadhia ya siri isiyoonekana kama ile ya Imam Mahdi kwa kawaida hulazimu kupatikana wakanushaji wa kadhia kama hiyo.

Hakika yule anayejificha mbali na macho ya watu kwa ajili ya kutimiza lengo lolote miongoni mwa malengo yake basi kwa kitendo hicho huwa amekusudia asionwe na mtu yeyote kiasi kwamba kama watu wataulizwa kuhusu yeye watasema: "Hatujamwona" hata kama walioulizwa ni watu wa karibu mno na yeye. Na tumesema kuwa ukanushaji wa watu kama hawa katika kadhia ya siri iliyofichikana hausihi kuwa dalili ya kutokuwe- po kwa kadhia hiyo.

Hiki ndio kitofautishi cha msingi walichoteleza wale wenye kukanusha kuzaliwa na kuwepo kwa Imam Mahdi (a.s.), kwani wao wamekuwa wak- itafuta ushahidi wa namna hii ndani ya historia na pale wanapopata cho- chote mfano wa hicho basi hukifanya dalili ya kutokuzaliwa na kutokuwe- po Imam Mahdi (a.s.), hivyo wao hushikilia mambo kama vile, kitendo cha Shia kutofautiana juu ya muda wa kuzaliwa na juu ya jina la Imam na ushahidi wa Jafar mwongo ami yake na Imam Mahdi aliyedai kuwa kaka yake amefariki bila kuacha mtoto.

Na mjadala wetu wa msingi na hawa ni kuwa, mfumo wa historia unaweza kutoa uamuzi kwenye masuala ya kimaada ambayo vipengele vyake vyote viko chini ya mtazamo wa wapokezi na

wanahistoria tu, mfano vita vya Siffin, vita vya Karbala na vinginevyo, lakini wenyewe hauwezi kuamua kwenye masuala yenye msingi wa ghaibu na itikadi yale yenye miale ya kimaada kwa wateule tu kiasi kwamba laiti watu wa kawaida wakiulizwa kuhusu suala hilo watalikanusha.

Basi inakuwaje mnafanya ukanushaji wa watu wa kawaida kuwa ni dalili ya kutokuwepo kadhia ambayo tangu mwanzo inaaminiwa kuwa si kadhia inayokubali kushuhudiwa kwa milango ya fahamu isipokuwa kwa wateule tu?

Ni wajibu kwa mtu anayetaka kujadili suala la Mahdi aanzie mwanzo wake ambao ni itikadi na wala asianzie mwisho wake ambao ni historia, kwa sababu kadhia ya siri iliyofichwa kwa lengo maalumu dhidi ya macho ya watu wa karibu haikosi tofauti kama zile za muda wa kuzaliwa Imam na tofauti juu ya jina la mama wa Imam, na pia ushahidi kama wa Jafar mwongo haudhuru kadhia hiyo.

Kwa sababu jibu la kawaida katika hali kama hii ni isemwe: Hakika tofau- ti juu ya mwaka wa kuzaliwa na jina la mama wa Imam ilikuwa ni hali ya kawaida inayotokana na juhudi za Imam Hasan Al-Askari katika kuficha vipengele vya kadhia, ufichaji kamili kabisa dhidi ya macho ya watu wa karibu, akiwa anazuia habari zisiufikie utawala wa ukoo wa Abbas.

Hivyo hata ushahidi wa Jafar mwongo kuwa kaka yake alikufa bila ya kuacha mtoto ulikuwa ni wa namna hii, kiasi kwamba Imam Hasan Al- Askari alitaka kuficha mazazi yake hata kwa kaka yake na bila kudhi- hirisha hilo mbele yake. Hata kama Imam angekuwa hana mtoto baada yake basi utaratibu huu wa Imam Hasan Al-Askari mbele ya kaka yake ungekuwa ni wa kimantiki hata kama kaka yake asingekuwa mwongo ambaye ufasiki wake umethibitishwa, sembuse katika hali hii ambayo Jafar mwongo ufasiki wake umethibitishwa?[12]

Sifa ya pili: Uimamu wa udogoni

Miongoni mwa sifa za lazima zinazoambatana na uwelewa wa wazo la Mahdi kwa mujibu wa upande wa Ahlul-Bait ni kuamini uimamu wa uto- toni wa Imam Mahdi (a.s.), sifa hii kuna kipindi tunaitazama kwa upande wa Uislamu, tukikusudia kutoa dalili na kuthibitisha huku tukijibu utata wowote wa kidini unaoweza kujengwa. Mwingine ni upande wa tukio lenyewe, tukikusudia kubainisha kuwa uimamu huu ni uimamu halisi wenye sifa zote zinazostahili, na wala si uimamu wa dhana au madai matupu.

Tunapoitazama kwa upande wa Uislamu tunakuta kwanza kuna dharura ya kufafanua je, wenyewe ni suala la kiitikadi au wenyewe ni suala la kisharia (kifiqihi)? Ikiwa suala ni la kiitakidi kama wanavyoamini Shia basi sisi tunaikuta Qur'an tukufu inathibitisha waziwazi unabii kwa mtoto, na unabii ni suala la kiitikadi. Mwenyezi Mungu anasema: "Ewe Yahya shika kitabu kwa nguvu, na tukampa hekima angali mtoto."[13]

Na kama ni suala la kisharia (kifiqihi) basi ni wazi kabisa kuwa sharia (fiqihi) ya kiisilamu imemzuia mtoto kujiendeshea muamala wowote, na aliyezuiliwa kujiendeshea muamala hana utawala juu ya nafsi yake,

basi ikiwa hivyo ndivyo itawezekanaje tena yeye awe mtawala wa mwingine? Hivyo uimamu wa mtoto si halali.

Waisilamu wametofautiana katika suala hili na hatimaye madhehebu ya madhehebu manne ikaufanya ukhalifa na uimamu kuwa miongoni mwa majukumu ya kisharia (kifiqihi) na vitendo vya mukalafina.

Kambi ya Ahlul–Bait yenyewe ikaamini kuwa ni suala la kiitikadi na ni miongoni mwa misingi ya dini ambayo ndio majukumu ya Mola mlezi wa ulimwengu na wala si miongoni mwa majukumu ya mukalafina na viten– do vya waja.

Hivyo madhehebu ya Ahlul–Bait inapoamini uimamu wa utotoni kwa baadhi ya maimamu akiwemo Imam Mahdi yenyewe huwa na uhakika katika hilo na wala hakuna utata wowote upande wa akida maadamu Qur'an tukufu inathibitisha waziwazi unabii wa utotoni kwa Yahya (a.s.), pia hakuna utata wowote upande wa sharia (fiqihi) maadamu suala hili kwa mtazamo wa Ahlul–Bait liko nje na wigo wa sharia (fiqihi) na liko kwenye wigo wa akida. Hukumu za sharia katika mlango wa kumzuia mtoto kujiendeshea mambo unawahusu mukalafina na haumuhusu Mwenyezi Mungu, kwa sababu sharia ni maamrisho ya Mwenyezi Mungu yanayoelekezwa kwa mukalafina.

Hivyo inabainika kuwa lengo letu katika kutoa ushahidi kupitia unabii wa Yayha (a.s.) ni kutaka kubainisha kuwa uimamu ni kama unabii yote maw– ili ni masuala ya kiakida, na kuwa suala la kiakida haliko chini ya vipimo vya kibinadamu, bali hua haliwi hata chini ya vipimo vya sharia ambayo imekuja ili kuratibu mwenendo wa mukalafina na hivyo haisihi kuioanisha na Mola mlezi wa walimwengu.

Hivyo unabii wa Yayha (a.s.) unatufidisha kuwa suala la kiakida linasima– ma kwa dalili na hoja, hivyo iwapo itathibiti hoja ya kiakida inay– outhibitisha uimamu wa mtoto mdogo basi ni lazima kuuamini kama tulivyoamini unabii wa mtoto mdogo pindi iliposimama hoja kuuthibitisha, na hapo haitokuwa na maana yoyote kauli ya mwenye kusema kuwa kuthibitisha kupitia unabii wa Yahya haiwezekani kwa sababu wenyewe umetamkwa waziwazi ndani ya Qur'an kinyume na suala la Mahdi.

Kuanzia hapa utaona hauna msingi wowote ukanushaji wa Ibnu Hajar Al– Haythami na mfano wake juu ya uimamu wa Imam Mahdi bali umeangu– ka, kwani yeye ameandika kwa njia isiyonasibu kuwa: "Kisha kina– chokubalika ndani ya sharia takatifu ni kuwa utawala wa mtoto mdogo hausihi, nawashangaa hawa wapumbavu walioghafilika imekuwaje wadai

kuwa uimamu wake ulianzia umri wa miaka mitano….."[14] Imeshakuwa wazi kuwa hili si miongoni mwa uamuzi wa sharia bali ni uamuzi wa fiqi– hi yao ambayo haisihi kutulazimisha sisi.

Tunapolitazama suala hili upande wa hali halisi ya kihistoria tunakuta kuwa Mahdi (a.s.) alichukua nafasi ya baba yake katika uimamu wa waisil– amu akiwa ni mtoto wa umri wa miaka mitano, hii inamaanisha kuwa alikuwa ni Imam aliyekamilika katika kila linalohusu uimamu, kuanzia uwezo wa kifikra hadi wa kiroho ikiwa ni mapema mno katika uhai wake mtukufu.

Sayyid Shahid As–Swadri anasema katika suala hili: “Uimamu wa mape– ma ni hali iliyotangulia kuwapata baadhi ya baba zake, kwani Imam Muhammad bin Ali Al–Jawad (a.s.) alichukua uimamu akiwa na umri wa miaka minane15 na Imam Ali bin Muhammad Al–Hadi alichukua uimamu akiwa mna umri wa miaka tisa16 na Imam Abu Muhammad Al–Hasan Al– Askari mzazi wa kiongozi anayengojewa alichukua uimamu akiwa na umri wa miaka ishirini.17

Hivyo inaonekana kuwa tukio la uimamu wa mapema lilishamiri kwa Imam Mahdi na Imam Al–Jawad, sisi tunaliita kuwa ni tukio la wazi kwa sababu kwa kule kuwatokea baadhi ya baba zake lilikuwa limetengeneza dalili ya kivitendo ya kimaada iliyoishi ndani ya jamii ya waisilamu na hivyo kipindi cha Imam wakawa wameijua na kuizowea, na hivyo hai– wezekani kuombwa dalili iliyo wazi na yenye nguvu kuliko uzoefu wa umma18 ili tushibitishe tukio miongoni mwa matukio.

Hilo tutalibainisha ndani ya nukta zifuatazo:

a. Uimamu wa Imam yeyote wa Ahlul–Bait haukuwa makao makuu ya ufalme na utekelezaji ambao unarithiwa kutoka kwa baba hadi kwa mtoto, ambao unapewa nguvu na utawala wa mtawala kama ilivyokuwa uimamu wa makhalifa wa kifatimiyya na ukhalifa wa makhalifa wa kiabbasia, bali sera zake pana za kiraia zilikuwa zikipendwa kupitia njia ya kiroho waliyokuwa nayo, ukinaishaji wa sera hizo kifikra kuwa wao ndio wanao– faa kwa uimamu huu ili kuongoza Uislamu, na uongozi wao uliyokuwa kwa misingi ya kiroho na kifikra.

b. Sera hizi za kiraia ziliasisiwa tangu mwanzo wa Uislamu na zikashamiri na kuenea zama za maimamu wawili Al–Baqir na As–Sadiq (a.s.) na hivyo madhehebu hii iliyolelewa na maimamu hawa wawili ndani ya sera hizi za kiraia ikawa imetengeneza mkondo mpana wa kifikra ndani ya ulimwengu wa kiisilamu, mkondo uliyojumuisha mamia ya Wanachuoni wa sharia, wanathaiolojia, wanatafsiri na Wanachuoni katika fani mbalimbali za maarifa ya kiisilamu na kibinaadamu yaliyokuwa maarufu zama hizo, mpaka Hasan bin Ali Al–Washa akasema: “Mimi niliingia msikiti wa Kufa humo nikawaona masheikh19 mia tisa kila mmoja akisema ametusimulia Jafar bin Muhammad.”

c. Hakika masharti waliyokuwa nayo madhehebu hii pamoja na sera za kiraia walizoziwakilisha ndani ya jamii ya kiisilamu yenyewe tu yalivyo yanauamini uimamu na kuweka mipaka katika kumwainisha Imam na kutambulisha uwezo wake katika jukumu la uimamu, ni masharti makali mno kwa sababu yenyewe yanaamini kuwa Imam hawi Imam ila anapokuwa ni mjuzi kuliko watu wote wa zama zake.20

d. Hakika madhehebu na sera zake za kiraia ilikuwa ikitoa muhanga mkub– wa katika kuimarisha akida yake kuhusu uimamu, kwa sababu kwa mtazamo wa ukhalifa wa zama hizo ulikuwa ukiiona madhehebu hiyo ni adui, kwa uchache ni upande wa kifikira, jambo lililopelekea utawala wa zama hizo kuwatokomeza na kuendelea kuwauwa, hivyo akauwawa aliyeuwawa, akafungwa aliyefungwa na mamia wakafia ndani ya giza la magereza, hii inamaanisha kuwa itikadi ya uimamu wa Ahlul–Bait ilikuwa ikiwakalifu gharama ghali,21 na mtu hakuwa na kishawishi chochote isipokuwa ile hisia ya kujikurubisha karibu mno na Mwenyezi Mungu mtukufu aliyonayo mwenye kuamini au kutarajia.

e. Hakika maimamu wenyewe ambao sera hizi za kiraia zilikuwa karibu nao kupitia uimamu hawakujitenga nazo na wala hawakutegemewa kujik- weza kama ilivyo kwa wafalme mbele ya raia wao na wala hawakuwa wamejificha labda wafichwe na utawala uliokuwa madarakani zama hizo kwa kuwafunga na kuwafukuza, hili tunalifahamu kupitia idadi kubwa ya wapokezi na wasimulizi wa Hadithi wa kila mmoja miongoni mwa maima- mu kumi na moja na pia kupitia barua kati ya Imam na watu wa zama zake, pia kupitia safari alizokuwa akisafiri Imam upande mmoja na wawakilishi wake sehemu mbalimbali za ulimwengu upande mwingine, na kupitia kile kitendo kilichozoeleka na wafuasi wao cha kwenda kuwajulia hali maima- mu wao na kuwazuru huko Madina tukufu pindi wanapokuja nyumba tukufu toka kila sehemu kwa ajili ya kutekeleza faradhi ya hija.22 Hayo yote yanalazimu kuendelea kuwa pamoja kwa kiwango cha wazi kati ya Imam na sera zake zilizoenea sehemu zote za ulimwengu wa kiisilamu katika matabaka mbalimbali ya Wanachuoni na wasiokuwa Wanachuoni.

f. Ukhalifa wa zama za maimamu ulikuwa ukiwatazama wao na uongozi wao wa kiroho na kiimamu kama chimbuko la hatari kubwa dhidi ya utawala wao na mikakati yao, kwa ajili hii ulitumia kila juhudi katika kuu- tokomeza uongozi huu, na katika kutimiza hilo wakalazimika kuwa na njia mbalimbali hasi, na kuna muda ulidhihirisha chuki na ujeuri pale unapo- lazimika kulinda nafasi yake, na hivyo viliendelea vitendo vya kuwaweka maimamu gerezani na kuwafukuza bila kujali hisia za machungu na kuk- erwa kwa waisilamu na watu wa viwango mbalimbali wenye kuwatawal- isha.

Tukichukua nukta hizi sita kwa uangalifu ambazo ni ukweli halisi wa kihistoria usiokuwa na shaka yoyote tunaweza kupata natija ifuatayo, nayo ni: Tukio la uimamu wa mapema lilikuwa ni tukio lililotokea kweli wala si ndoto miongoni mwa mambo ya ndoto, kwa sababu Imam ambaye anaji- tokeza mbele za watu ilihali akiwa mdogo kisha anajitangaza kuwa ni Imam wa kiroho na kifikra kwa waisilamu ni lazima awe katika uwezo wa wazi unaoonekana bali awe na elimu kubwa na maarifa, mtazamo wa juu, umakini katika sharia, tafsiri na akida.

Kwa sababu asingelikuwa hivyo basi asingeliweza kuwakinaisha raia hao juu ya uimamu wake, ilihali imeshatangulia kuwa maimamu walikuwa katika nafasi ambayo inawaruhusu raia kuwa nao pamoja na kuyamiliki maisha yao na kuchunguza shakhsia zao.

Hivi unaona inawezekana mtoto mdogo adai uimamu na ajisimike kama kiongozi wa Uislamu mbele ya macho na masikio ya umma kisha watu wote wamwamini na kutoa kila kilicho ghali na thamani kwa ajili ya kuutetea na kuundeleza bila ya watu hao kujilazimisha kuchunguza hali yake? Na bila ya kutetemeshwa na tukio hili la uimamu wa mapema ili kujua undani wa tukio na kumtathmini kijana huyu mdogo aliye Imam23**?**

Hebu tujalie kuwa watu hawakujishughulisha na kitendo cha kutaka kujua undani, je suala hili linaweza kuendelea miaka yote na miezi yote bila ya ukweli kugundulika na hasa ukizingatia kuwa kuna ushirikiano halisi wenye kuendelea kati ya mtoto ambaye ndiye Imam na watu wengine? Je akili inakubali kijana yule kwa akili yake na fikira yake awe ni Imam laki- ni hilo lisionekane ndani ya uhusiano wake wa muda mrefu?

Tukijalia kuwa sera za kiraia za uimamu wa Ahlul–Bait hazikutoa nafasi ya kugundua hali halisi ya mambo basi ni kwa nini ukhalifa uliokuwa madarakani ulinyamaza bila kufichua hali halisi kwa faida yake? Hivi uoni hivyo ingekuwa ni rahisi sana juu ya utawala uliyokuwepo madarakani laiti kweli Imam mtoto angekuwa ni mtoto kifikira na kielimu kama ilivyo kwa watoto wengine.

Hivi huoni njia ya kufanikiwa zaidi ingekuwa ni hii ya kutoa hali halisi ya mtoto huyu kwa wafuasi wake na wasiokuwa wafuasi wake, na kisha kuthibitisha kutokufaa kwake kwa uimamu na uongozi wa kiroho na kifiki– ra? Kwani hata kama ni vigumu kukinaisha kuwa mtu fulani mwenye miaka arubaini au hamsini aliyekusanya elimu kubwa zama zake hafai kuchukua uimamu lakini hakuna ugumu wowote katika kukinaisha kuwa mtoto wa kawaida hafai kuchukua uimamu kwa maana ile waijuayo Shia Imamiya[24], hiyo ni vyovyote vile atakavyokuwa mwerevu na mwenye kipaji. Njia hii ingekuwa ni nyepesi na rahisi mno kuliko njia hizo za utokomezaji na uuwaji zilizochukuliwa na utawala wa zama hizo.

Hakika tafsiri pekee ya kitendo hiki cha kunyamaza kwa ukhalifa wa zama hizo dhidi ya mchezo huu mwepesi[25] ni kuwa wenyewe ulijua fika kuwa uimamu wa mapema ni tukio dhahiri la kweli na wala si mbinu za kuund– wa. Ni kweli kabisa kuwa wenyewe uliujua fika ukweli huo kivitendo baada ya kuwa umejaribu kucheza mchezo huo mwepesi lakini ukashindwa. Historia inatusimulia majaribio ya namna hii na jinsi yalivyofeli, ilihali katu haijatusimulia jinsi tukio la uimamu wa mapema lilivyotetereka au jinsi mtoto aliye Imam alivyokumbana na kikwazo kilicho juu ya uwezo wake au kilichotetemesha na kuwafanya watu wakose imani naye.

Na hii ndio maana ya ile kauli tuliyosema kuwa uimamu wa mapema ni tukio la kweli lililotokea ndani ya maisha ya Ahlul–Bait (a.s.) na wala si ndoto tupu, pia tukio hili lililotokea lina mizizi na hali mbalimbali ndani ya utamaduni utokao mbinguni ambao umedumu ndani ya ujumbe na uongozi wote utumwao na Mola mlezi.

Yahya (a.s.) anatosha kuwa mfano halisi wa tukio hili la uimamu wa mapema wa Ahlul–Bait (a.s.) uliyomo ndani ya utamaduni huu wa Mola mlezi pale Mwenyezi Mungu aliposema: “Ewe Yahya! Shika kitabu kwa nguvu, na tukampa hekima angali mtoto.”[26] Basi itakapothibiti kuwa uimamu wa mapema ni tukio lilitokea na lipo kivitendo ndani ya maisha ya Ahlul–Bait hakutokuwa tena na kizuizi chochote kinachohusu uimamu wa Mahdi (a.s.) na ukhali wake baada ya baba yake akiwa angali mdogo.”[27]

Sifa ya tatu: Ghaiba inalazimu umri mrefu unaolingana na urefu wa zama.

Miongoni mwa mambo ya lazima na sifa za uelewa wa wazo la uwepo wa Mahdi kwa mujibu wa upande wa Ahlul–Bait (a.s.) ni kuamini ghaibu ya Imam (a.s.) dhidi ya macho na kuendelea kuwa katika hali hiyo mpaka Mwenyezi Mungu atakapomwidhinia kudhihirika. Ili tuthibitishe sifa hii basi tunaizungumzia ndani ya hatua wawili:

Ya kwanza: Hatua ya kuthibitisha uwezekano wa umri mrefu mpaka mwisho wa zama.

Hakika tatizo la msingi ambalo uwelewa wa uwepo wa Mahdi kwa mujibu wa Ahlul–Bait unakumbana nalo ni ile hali ya umri mrefu inayolazimu uwelewa huu, pamoja na urefu wa zama wenye kuendelea sanjari na umri wake. Tatizo hili limetatuliwa kwa majibu mengi nasi hapa tutatoa jibu la Sayyid Shahid alipoandika kuwa:

“Je, inawezekana mwanadamu akaishi karne nyingi kama inavyoonekana kwa huyu kiongozi anayengojewa atakayeubadili ulimwengu, ambaye hivi sasa umri wake umefikia zaidi ya miaka elfu moja mia moja na arubaini, yaani zaidi ya mara kumi na nne ya umri wa mwanadamu wa kawaida anayetimiza hatua za kawaida kuanzia utotoni mpaka ukongweni?

Neno uwezekano hapa linamaanisha moja ya maana tatu: Uwezekano wa kivitendo, uwezekano wa kielimu na uwezekano wa kimantiki au kifilosofi. Nisemapo uwezekano wa kivitendo, nakusudia kuwa kitu kiwe kinawezekana lakini ili kitimie kinamuhitaji mtu ima mimi au wewe au mwanadamu mwingine ili akitimize kivitendo. Mfano, kupiga mbizi baharini hadi kufika chini ya kina cha bahari, au kupanda mwezini ni vitu ambavyo vina uwezekano wa kivitendo unaoweza kutimia, na hivyo hivi sasa wapo wanaofanya vitendo hivyo na kuvitimiza kwa namna fulani.

Nisemapo uwezekano wa kielimu, nakusudia kuwa kuna vitu ambavyo havina uwezekano wa kivitendo unaowezwa kutimizwa na mimi au wewe wala kutimu kupitia vifaa vya kisasa, lakini elimu haina kauli wala haiashirii rai yake inayoweza kutafsiriwa kuwa inakanusha uwezekano wa kutokea na kutimia vitu hivyo kupitia vifaa maalumu. Mfano, ndani ya elimu hamna kauli inayokanusha kutokea kwa kitendo cha kupanda hadi

kwenye sayari ya Zuhura, bali nadharia ya sasa inaonyesha kuwa hilo linawezekana japokuwa hivi sasa haijakuwa rahisi kwangu au kwako kufanya hivyo. Kwa sababu hakuna tofauti ila ndogo kati ya kupanda hadi kwenye sayari ya Zuhura na kupanda hadi mwezini, na wala kupanda hadi kwenye sayari ya Zuhura si kingine bali ni kuushinda ugumu wa ziada utokanao na masafa ya mbali zaidi.

Hivyo kitendo cha kupanda hadi sayari ya Zuhura kinawezekana kielimu japokuwa hivi sasa kivitendo haiwezekani28, hiyo ni kinyume na kitendo cha kupanda hadi kufika kwenye jua huko mbinguni, jambo hilo hali– wezekani kielimu, yaani elimu haina matarajio ya kutokea hilo kwani uwezekano wa kutengeneza chombo chenye uwezo wa kuzuia joto la jua hausawiriki kielimu na kitafiti.

Nisemapo uwezekano wa kimantiki na kifilosofi, nakusudia kuwa akili haioni kizuizi kinachopelekea kuhukumu kuwa jambo fulani ni muhali na haliwezekani kabisa, hiyo ni kutokana na kanuni za uwezekano ina– zozidiriki. Kwa mfano, kugawa machungwa matatu kwa uwiano sawa ni kitendo kisichokuwa na uwezekano wa kimantiki, kwa sababu akili inajua kuwa tatu ni idadi tasa na wala si idadi shufwa hivyo haiwezekani kugawanyika kwa uwiano sawa, kwa sababu kugawanyika kwa uwiano sawa kutakuwa kunamaanisha yenyewe ni shufwa na hapo itakuwa ni tasa na shufwa wakati mmoja, na hali hii ni mpingano na mpingano ni muhali kimantiki.

Lakini mwanadamu kuingia ndani ya moto bila kuungua au kupanda hadi kwenye jua bila ya kuunguzwa

na joto la jua ni jambo lisilokuwa muhali kimantiki, kwani hamna mpingano katika kufikiria kuwa joto halitoki kwenye umbo lenye joto kali na kuingia kwenye umbo lenye joto dogo, bali ni kinyume na utafiti uliyothibiti sasa kuwa joto hutoka kwenye umbo lenye joto kali mpaka kwenye umbo lenye joto dogo hadi pale maumbo yote mawili yatakapolingana kwa joto. Na hivyo tunagundua kuwa uwezekano wa kimantiki una wigo mpana kuliko uwezekano wa kielimu na ule wa kielimu una wigo mpana kuliko wa kivitendo.

Hamna shaka kuwa kurefuka umri wa mwanadamu hadi maelfu ya miaka ni jambo linalowezekana kimantiki kwa sababu hilo si muhali kwa mtazamo wa kaikili, wala katika hali kama hii hakuna mpingano wowote kwa sababu uhai kama uhai haulazimu kifo cha haraka, na wala hakuna mjadala katika hilo.

Pia hamna shaka wala mjadala kuwa umri huu mrefu hauwezekani kivi- tendo kwa namna ile ya uwezekano wa kivitendo wa kuteremka mpaka chini ya kina cha bahari au kupanda hadi mwezini, hiyo ni kwa sababu elimu na vitendea kazi vyake na nyenzo zake zilizopo sasa, na ule uwezo wa uzoefu wa mwanadamu wa zama hizi, vyote haviwezi kurefusha umri wa mwanadamu hadi mamia ya miaka, kwa ajili hii tunawakuta watu wengi wenye kujali uhai na wenye uwezo wa kuandaa nyenzo za kielimu hawafanikiwi kufikia umri ila ule wa kiwango cha kawaida.

Ama kwa upande wa uwezekano wa kielimu ni kuwa mpaka leo hakuna rai inayokanusha hilo.29 Mada hii ina uhusiano na tafsiri ya kifasiolojia kuhusu hali ya uzee na ukongwe wa mwanadamu, je hali hii inatokana na kanuni ya maumbile inayolazimu nyama za mwili wa mwanaadamu na chembechembe zake kukauka kidogokidogo na kupungua uwezo wa kuen- delea katika utendaji mpaka kufikia kiwango cha kusimama katika muda maalumu hata kama tutautenga na sababu za nje?

Au ukaukaji huu na upungufu wa uwezo huu katika nyama na chem- bechembe za mwili hutokana na kule kupambana na sababu za nje kama vile bakteria au sumu inayoingia mwilini kupitia chakula anachokula au sababu nyingine yoyote?

Elimu inajiuliza yenyewe swali hili hivi sasa na ina uwezo wa kulijibu, swali hili lina jibu zaidi ya moja kwa mtazamo wa kielimu. Kwani iwapo tukichukua mtazamo wa kielimu unaotafsiri uzee na udhaifu wa ukongwe kuwa unatokana na mapambano dhidi ya sababu maalumu za nje, hii ita- maanisha kuwa kwa uwezekano wa kielimu ni kuwa iwapo nyama ambayo inatengeneza mwili wa mwanaadamu itatengwa mbali na sababu hizo maalumu basi ina uwezo wa kuendelea na uhai na kujiepusha na hali ya uzee na kuishinda kabisa.

Na kama tukitafsiri uzee kuwa unatokana na kanuni ya kimaumbile ya chembechembe hai na nyama yenye uhai binafsi, kwa maana kuwa yenyewe ina nguvu yenye ukomo maalumu inayopitia ukongwe na uzee na kuishia kifo. Basi nasema: Kama tukitafsiri kwa mtazamo huu haitomaan- isha kuwa kwa kanuni hii ya kimaumbile hakuna udhaifu. Bali yenyewe inaonyesha udhaifu upo, kwa sababu katika uhai wetu wa kawaida tunaku- ta uzee ni hali ya kifasiolojia isiyokuwa na wakati maalumu na hivyo huweza kuja mapema, na wasomi wanathibitisha hilo katika tafiti zao za kielimu.

Na pia inaweza kuchelewa kiasi kwamba akawa na miaka mingi ya kupin– dukia lakini akawa bado viungo vyake vina nguvu na wala havitokezi kwake viambata vya uzee, kama matabibu wanavyoeleza hilo.30 Bali wasomi wameweza kivitendo kutumia udhaifu kwa kanuni hiyo ya kimaumbile na hivyo wakajua umri wa baadhi ya wanyama kuwa ni zaidi ya mamia ya miaka ukilinganisha na umri wa kawaida, hiyo ni kutokana na kutengeneza mazingira na sababu zinazochelewesha utendaji wa kanuni ya uzee.

Kwa maelezo haya inathibiti kielimu kuwa kuchelewesha kanuni hii kwa kutengeneza mazingira na sababu maalumu ni jambo linalowezekana kie– limu japokuwa elimu haijafanikiwa kutimiza ucheleweshaji huu kivitendo kwa kiumbe maalumu kama mwanaadamu, hakuna kitofautishi ila ni kwa sababu ya tofauti ya kiwango cha ugumu kilichopo kati ya utimizaji huu kwa mwanadamu na kwa viumbe wengine.

Hii inamaanisha kuwa upande wa nadharia ya kielimu na kulingana na maelekezo ya mitazamo yake kamwe hakuna kinachokanusha uwezekano wa kurefuka umri wa mwanadamu, hiyo ni sawa tutafsiri uzee kuwa una– tokana na mapambano na vita dhidi ya sababu za nje au tutafsiri kuwa ni matokeo ya kanuni ya kimaumbile ya chembechembe hai zenyewe binafsi huelekea kwenye kutoweka.

Muhtasari wa hali hiyo ni kuwa urefu wa umri wa mwanaadamu na kuen– delea kwake kuishi karne nyingi ni jambo linalowezekana kimantiiki na kielimu, lakini lenyewe halijawezekana kivitendo isipokuwa mitazamo ya kielimu ipo mbioni kulitimiza hili kivitendo baada ya juhudi ndefu.

Kutokana na maelezo haya tunauzungumzia umri wa Mahdi (a.s.) na mshangao na maswali yanayouzunguka, tunasema: Baada ya kuthibiti kuwa umri huu unawezekana kimantiki na kielimu, na baada ya kuthibiti kuwa elimu ipo mbioni kidogo kidogo kuubadili uwezekano huu wa kinad– haria na kuugeuza kuwa wa kivitendo basi hakuna nafasi ya mshangao labda kushangaa jinsi gani Mahdi ameitangulia elimu yenyewe, na hivyo uwezekano wa kinadharia unabadilika na kuwa wa kivitendo kwa Mahdi mwenyewe kabla ya elimu kufikia kiwango cha uwezo huo wa kivitendo katika maendeleo yake kuhusu mabadiliko haya, hii ni sawa na mtu anayei–

tangulia elimu katika kugundua dawa ya kansa.

Na ikiwa suala ni vipi Uislamu umezitangulia harakati za elimu katika sekta hii ya mabadiliko? Basi jibu ni kuwa: Hiyo si sekta pekee ambayo Uislamu umezitangulia harakati za kielimu, kwani sisharia yote ya kiisila– mu imezitangulia harakati za elimu na maendeleo ya kimaumbile ya fikra za mwanadamu kabla ya karne nyingi?31

Kwani haijatoa changamoto kwa kutoa kanuni mbalimbali zinazohitaji utekelezaji ambao bado uwezo wa mwanadamu haujaufikia katika harakati zake binafsi ila baada ya miaka mingi?

Hivi haujaleta sheria ambazo ziko katika kilele cha hekima ambazo mwanadamu hajaweza kutambua siri zake na hekima yake ila baada ya muda fulani? Hivi ujumbe wa Mola haujafichua siri za ulimwengu

ambazo hazikuweza kugonga ndani ya mawazo ya mwanadamu, kisha baadae ndipo elimu ikathibitisha na kuunga mkono?

Ikiwa kweli tunayaamini haya yote basi ni kwa nini tunakanusha kitendo cha huyu aliyeutuma ujumbe huu kuwa ameitangulia elimu kupitia umri wa Mahdi?[32] Mimi hapa sijazungumzia ila hali ya utanguliaji ambayo sisi tunaweza kuidiriki moja kwa moja na hapo tunaweza kuongezea hali ya utanguliaji ambayo inazungumziwa na ujumbe wa Mola wenyewe.

Mfano wa hali hiyo ni: Wenyewe unatupa habari kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipelekwa usiku kutoka msikiti mtukufu hadi msikiti wa mbali, safari hii[33] ikiwa tutataka kuifahamu kupitia kanuni za kawaida za kiulimwengu basi yenyewe inaonyesha jinsi ya kutumia kanuni za kawai- da za kiulimwengu kwa namna ambayo elimu haikufanikiwa kutimiza matumizi hayo ila baada ya mamia ya miaka.[34] Hivyo ujuzi huu wa Mola ambao ulimwezesha Mtukufu Mtume kusafiri kwa haraka mno kabla ya elimu kufanikiwa kitimiza hilo ndio uliomwezesha Khalifa wake wa mwisho awe na umri huu mrefu kabla ya elimu kufanikiwa kutimiza hilo.

Ndio, umri huu mrefu ambao Mwenyezi Mungu amemtunuku mwokozi anayengojewa unaonekana ni kitu kigeni ndani ya mipaka iliyozoeleka na hata leo katika maisha ya kawaida ya watu na hata ndani ya maendeleo ya kisasa yaliyotimizwa kwa uzoefu wa wasomi. Lakini je, jukumu gumu la mabadiliko aliloandaliwa huyu mwokozi nalo sigeni ndani ya mipaka ya kawaida ya maisha ya watu ukilinganisha na maendeleo mbalimbali yaliy- owapitia katika historia ya maisha?

Hivi si kakabidhiwa mabadiliko ya ulimwengu na kurejesha hali yake ya kiustaarabu kama ilivyokuwa mwanzo kwa msingi wa haki na uadilifu?

Kwa nini basi tunashangaa pindi jukumu hili kubwa linapokuwa na baad- hi ya hali ngeni zilizoko nje ya mazoea yetu kama vile urefu wa umri wa mwokozi anayengojewa? Kwani ugeni wa hali hizi na kuwa kwake nje ya mazoea hata kama utakuwa ni mkubwa wa kiasi gani bado haujaushinda ugeni wa jukumu lenyewe kubwa ambalo ni lazima huyu tuliyeahidiwa alitekeleze.

Ikiwa tunaridhika na jukumu hilo la kipekee[35] la kihistoria japokuwa ndani ya historia ya mwanadamu halina mfano wake uliotangulia basi ni kwa nini haturidhii umri huo mrefu ambao ndani ya maisha yetu ya kawaida hatu- japata umri mfano wake? Na wala sijui je, ni bahati au la, kitendo cha watu wawili tu kusimama na kumaliza ustaarabu mbovu wa mwanadamu kwa kujenga ustaarabu mpya, huku kila mmoja kati yao akiwa na umri mrefu unaouzidi mara elfu umri wetu wa kawaida ?

Mmoja kati ya hao wawili tayari alishamaliza jukumu lake katika historia iliyopita ya mwanadamu, naye ni Nabii Nuh ambaye Qur'an Tukufu imemwelezea[36] kuwa aliishi ndani ya jamii yake miaka elfu moja kasoro hamsini, na kwa kupitia mafuriko akafanikiwa kuutengeneza ulimwengu upya.

Mwingine ni yeye atakayetekeleza jukumu lake huko mbele kwenye mus- takabali wa maisha ya mwanadamu, naye ni Mahdi (a.s.) ambaye mpaka sasa ameishi ndani ya jamii yake zaidi ya miaka elfu

moja, na siku aliyokadiriwa ataujenga ulimwengu upya.

Basi ni kwa nini tunakubali umri wa Nuh ambaye ulikaribia miaka elfu moja kwa kadirio la chini lakini hatukubali umri wa Mahdi (a.s.)?37

Mpaka sasa tumeshajua kuwa umri mrefu ni jambo linalowezekana kie- limu, lakini hebu tujalie kuwa ni jambo lisilowezekana kielimu na kuwa kanuni ya uzee na ukongwe ni jambo lisilowezekana kwa mwanadamu wa sasa na wala hata baada ya juhudi ndefu haiwezekani kuushinda na kubadili kanuni zake na masharti yake, hali hiyo inamaanisha nini?

Inamaanisha kuwa kurefuka kwa umri wa mwanaadamu kama Nuh na Mahdi (a.s.) kwa kuishi karne nyingi ni kinyume na kanuni za kawaida za Ama kuhusu uyakinifu wa nassi ni kuwa Hadithi za Mahdi zimefika kiwango cha uwingi usiopingika "*tawaatur*" na hali hiyo huwajibisha uyakinifu na elimu hivyo hakuna tofauti kati ya makundi mawili. Rejea kitabu At-Taju Al-Jamiu Lil-Usul 5:341 na 360. Uwingi usiyopingika "*Tawaturi*" umepokewa kutoka kwa Shawkaniy, na hatimaye Wanachuoni wa makundi yote mawili wamefikia kusema kuwa atakayepinga kuhusu Mahdi basi amempinga Mtukufu Mtume Muhammad. Hawajasema hivyo ila ni kwa ajili ya kuthibiti hali ya uwingi usiyopingika "tawa- turi" wa Hadithi hizo, na kuwa suala hilo ni katika dharura za kidini na atakayezikanusha basi ni kafiri kwa kauli ya wanazuoni wote. Rejea Al-Ishaah Liashratisaah cha Al-Barazanjiy anapomzungumzia Mahdi. Maelezo ya uwingi usiyopingika "tawaturi" tumeyanukuu kwenye utangulizi.

kiulimwengu ambazo zimethibitishwa na elimu, utafiti na majaribio ya kisasa, na kwa ajili hiyo hali hiyo inakuwa ni muujiza ambao umesitisha kanuni ya kiulimwengu katika hali maalumu ili kuhifadhi uhai wa mtu ambaye amekabidhiwa jukumu la kuhifadhi ujumbe wa Mola.

Huu si muujiza pekee wa namna yake au mgeni katika itikadi ya mwisila- mu anayeamini Qur'an na Sunna,38 kwani kanuni ya uzee na ukongwe si nzito zaidi kuliko kanuni ya joto kuhama toka umbo lenye joto kali hadi kwenye umbo lenye joto hafifu mpaka litakapokuwa na uwiano sawa, kwani tayari Mwenyezi Mungu alishasitisha kanuni hii ili kuokoa maisha ya Nabii Ibrahim (a.s.) pindi njia pekee ya kumwokoa ilipokuwa ni kusi- tisha kanuni hiyo.

Moto ukaambiwa pindi alipowekwa ndani ya moto: "Tukasema: Ewe moto, kuwa baridi na salama kwa Ibrahim."39 Basi akatoka ndani ya moto huo kama alivyoingia akiwa salama bila kupatwa na madhara yoyote. Na kanuni mbalimbali nyingi za kiulimwengu ambazo zilisitishwa ili kuwaokoa manabii na hoja wa Mwenyezi Mungu juu ya ardhi.

Bahari ilipasuliwa kwa ajili ya Musa40 (a.s.), warumi wakafananishiwa Isa41 pindi walipotaka kumshika na hawakuwa wamemshika, Mtume Muhammad (s) akatoka nyumbani kwake akiwa amezingirwa na vijana wa kikurayshi ambao walibaki saa nyingi wakisubiri kumshambulia, basi Mwenyezi Mungu akamsitiri dhidi ya macho yao ilihali akitembea katikati yao.42

Hali zote hizi zinaonyesha kanuni za kifizikia zilivyositishwa ili kum- wokoa mtu ambaye hekima ya Mola

ilihitaji kumwokoa, basi na kanuni ya uzee na ukongwe iwe miongoni mwa kanuni hizo.

Na tunaweza kutoa uwelea jumuishi kutoka ndani ya hali hiyo kuwa kila uhifadhi wa maisha ya hoja wa Mwenyezi Mungu unapolazimu kusitisha kanuni za kifizikia basi kurefuka kwa maisha ya mtu huyo kunakuwa ni dharura ili kutimiza jukumu lake aliloandaliwa kwalo, kwa sababu msaada wa Mola uliingilia kati kusitisha kanuni hiyo ili kutimiza jukumu hilo, kinyume na pale mtu anapokuwa tayari keshatimiza jukumu lake aliloan– daliwa kwalo na Mola, yeye hupokea mwito wake na kufariki au hufa kishahidi kulingana na taratibu za kanuni ya kifizikia .

Kwa kawaida huwa tunakutana na swali lifuatalo kutokana na uwelewa huu jumuishi: Inawezekanaje kanuni kusitishwa? Na inakuwaje unakatika uhusiano wa kutoachana (dharura au lazima) uliyopo katika hali ya kifizikia? Huoni hali hii inapingana na elimu iliyogundua kanuni hiyo ya kifizikia na kuainisha uhusiano huu wa kutoachana (dharura au lazima) kwa misingi ya majaribio na utafiti?

Jibu: Hakika elimu yenyewe binafsi imejibu swali hili kwa kuondoa fikira ya kuwepo hali ya kutoachana katika kanuni za kifizikia. Ufafanuzi juu ya hilo ni kuwa: Hakika elimu huzigundua kanuni za kifizikia kwa msingi wa utafiti wa majaribio na utaratibu maalumu, hivyo pindi inapozalisha utokeaji wa tukio la kiulimwengu baada ya tukio lingine basi uzalishaji huu huthibitishwa kwa kanuni ya kifizikia, nayo ni kila linapopatikana tukio la mwanzo baada yake hupatikana tukio la pili.

Isipokuwa ni kuwa elimu haioni kuwa ndani ya kanuni hii ya kifizikia mna hali ya kutoachana kati ya matukio mawili kupitia uhusiano wa tukio hili na lile, kwa sababu kutoachana ni hali ya ghaibu ambayo majaribio na utafiti wa kielimu haviwezi kuithibitisha, na kwa ajili hii mantiki ya elimu ya sasa inasisitiza kuwa kanuni ya kifizikia haizungumzii uhusiano usioachana bali huzungumzia mkutano wenye kuendelea kati ya matukio mawili.43 Hivyo muujiza unapokuja hutenganisha tukio moja dhidi ya lingine na kwenda kinyume na kanuni ya kifizikia na hali hiyo si kukatisha uhusiano usioachana wa matukio mawili.

Ukweli ni kuwa muujiza kwa uwelewa wake wa kidini kwa mujibu wa mantiki ya elimu ya kisasa umekuwa ni uwelewa wa kiwango kikubwa mno kuliko ulivyokuwa zama zile za nadharia ya kilasikia juu ya uhusiano wa sababu na visababishwa. Kwani kwa mujibu wa nadharia ya kale ilikuwa ikiona kuwa kila moja kati ya matukio mawili limezalisha hali ya moja kukutana na lingine, hivyo uhusiano wao ni ule wa dharura. Dharura hapa maana yake ni muhali tukio moja kuachana na tukio lingine.

Lakini ndani ya mantiki ya elimu ya sasa uhusiano huu umegeuka na kuwa kanuni ya mkutano au ya mfuatano unaozalika44 kati ya matukio mawili bila ya kuwepo dharura hiyo ya ghaibu. Hivyo muujiza unakuwa ni hali iliyotoka nje ya kanuni hii ya mkutano au mfuatano bila ya kugongana na dharura au kupelekea hali ya muhali.

Ama kwa misingi ya utafiti wa kimantiki45 sisi tunakubaliana na mtazamo wa elimu ya sasa kuwa utafiti huo hauthibitishi kuwa kuna uhusiano wa dharura kati ya matukio mawili, lakini sisi tunaona wenyewe unaonyesha kuwa kuna tafsiri shirikishi ya uzalikaji wa mkutano au mfuatano kati ya matukio mawili kwa

namna ya kuendelea. Tafsiri hii shirikishi kama ambavyo inawezekana kuitengeneza kwa misingi ya dharura ya asili pia vilevile inawezekana kuitengeneza kwa misingi ya hekima iliyopelekea Mnadhimu wa ulimwengu kufunganisha matukio maalumu na matukio mengine maalumu kwa namna yenye kuendelea, na hekima hiihii mara nyingine inalazimu kuvua matukio hayo toka kwenye kanuni na hivyo kupatikana muujiza."46

Hivyo dalili inabainika wazi kielimu na kimantiki kuwa umri mrefu ni jambo linalowezekana na wala haulazimu dosari ya kielimu wala ya kifal- safa, na kwa maelezo haya tunakamilisha hatua ya mwanzo ya utafiti kati- ka sifa ya ghaiba.

Pili: Hatua ya kuthibitisha kutokea hilo kivitendo kwa Imam Mahdi (a.s.): Uchambuzi katika hatua hii utakamilika kwa njia wawili: Ya kiakida na ya kihistoria.

Njia ya kiakida

Tunaweza kuiunda kwa fafanuzi tatu:

a. Sifa hii ni miongoni mwa vitu vya lazima vya asili ya uelewa wa wazo la Mahdi kwa Ahlul-Bait hivyo kuthibiti uwelewa huu uthibitikaji utokanao na dalili yakinifu, na kule kubainika ubatilifu wa uwelewa usiokuwa huu vinatuongoza kwa namna ya kawaida kuamini ghaiba ya Imam wa kumi na wawili (a.s.). Maadamu maimamu ni kumi na wawili tu na wao ni wenye kuainishwa na Mwenyezi Mungu na watu hawana ruhusa

ya kuwateua basi hatuwezi kusawiri chochote ila kule kuendelea kwa uhai wa Imam wa kumi na wawili na msafara wake katika safari ya wanadamu na baada ya hapo kudhihiri zama za mwisho.

Na ni hali ya kawaida kuwa mwanadamu anayeandaliwa kwa lengo kama hili na kupangiwa maisha marefu kama haya asifanikiwe kuishi maisha hayo kwa sura ya dhahiri, na ni lazima ayaishi kwa sura ya siri mbali na macho ya watu ila iwapo tutasema Imam Mahdi (a.s.) alikufa kifo cha kawaida kama watu wengine kisha atarudi tena kuishi zama atakazodhihiri. Lakini kauli hii inalazimisha hoja ya Mwenyezi Mungu kukatika ndani ya kipindi tenganishi kati ya kufa kwake na kudhihiri kwake, na hali hiyo inapingana na Hadithi ya vizito viwili ambayo inaonyesha Kitabu haki- toachana na Kizazi na kuwa havitoachana hata muda mchache mpaka pale Kiyama kitakaposimama na kuingia kwenye Hodhi. Na italazimu kuamini kurejea Imam Mahdi kwenye uhai baada ya kifo chake, na hii ni kauli isiyosemwa na mwisilamu yeyote.

b. Riwaya zinaonyesha Imam Mahdi ana sifa ya ghaiba, na baadhi ya vyan- zo vya kisunni mfano wa kitabu Yanabiul-Mawaddah na Faraidus- Samtwayni vimeeleza hilo. Ndani ya kitabu Yanabiul-Mawaddah amenukuu kutoka kwenye kitabu Faraidus-Samtwayni kutoka kwa Al- Baqir (a.s.) kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake Ali (a.s.) amese- ma: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: "Mahdi ni kutoka kwenye kizazi changu, atakuwa na ghaiba na atakapodhihiri ataijaza ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa ujeuri na dhulma."47

Pia humo mna nyingine kutoka kwa Said bin Jubayri kutoka kwa Ibnu Abbas (r.a.) amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: “Hakika Ali ni wasii wangu na Al-Qaimu mwenye kungojewa Mahdi ambaye ataijaza ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa dhu- luma na jeuri atatoka kwenye kizazi chake. Naapa kwa Yule aliyenituma kwa haki niwe mbashiri na muonyaji hakika wale watakaothibiti katika imani ya kuamini uimamu wake zama za ghaiba yake ni watukufu mno kuliko madini ya yakuti chekundu.”

Akasimama Jabir bin Abdullah akasema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)! Al-Qaimu kutoka kwenye kizazi chako ana ghaibu? Akasema: “Ndio, naapa kwa Mola wangu Mlezi ili Mwenyezi Mungu awachambue wale walioamini na awaangamize makafiri.” Kisha akasema: “Ewe Jabir! Jambo hili ni jambo la Mwenyezi Mungu na siri miongoni mwa siri za Mwenyezi Mungu, basi jiepushe na shaka kwani hakika kushakia jambo la Mwenyezi Mungu ni ukafiri.”

Pia ndani ya kurasa zilizotajwa imepokewa kutoka kwa Hasan bin Khalid amesema: Ali bin Musa Ridhaa amesema: “Hakika wa nne toka kizazi changu ni mwana wa bibi wa watumwa, kupitia yeye Mwenyezi Mungu atatoharisha ardhi dhidi ya kila ujeuri na dhulma na yeye ndiye ambaye watu watashakia kuzaliwa kwake na ndiye mwenye ghaibu, basi atakapodhihiri ardhi itang’aa kwa nuru ya Mola wake Mlezi.”[48]

Pia mna: Kutoka kwa Ahmad bin Ziyad kutoka kwa Daabal bin Ali Al- Khazaiy katika Hadithi waliyoipokea kuhusu Ridhaa (a.s.) na alivyosoma shairi mpaka akasema: “Hakika Imam baada yangu ni mwanangu Muhammad na baada ya Muhammad ni mwanae Ali na baada ya Ali ni mwanae Hasan na baada ya Hasan ni mwanae Hoja Al- Qaimu naye ndiye mwenye kungonjewa ndani ya ghaibu yake na mwenye kutiiwa atakapodhihiri, ataijaza ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa jeuri na dhuluma. Ama ni lini atadhihiri? Ni kuwa habari kuhusu wakati amenisimulia baba yangu kutoka kwa baba zake kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: “Mfano wake ni sawa na Kiyama hakitowaijia ila ghafla.”[49]

Na mna: Kutoka kwenye kitabu Ghayatul-Marami kutoka kwenye kitabu Faraidus-Samtwayni kutoka kwa Jabir bin Abdullah, ameivusha: “Mahdi ni kutoka kwenye kizazi changu jina lake ni jina langu na kuniya yake ni kuniya yangu, ndiye mtu afananaye na mimi sana tabia na maumbile, atakuwa na ghaibu na mataifa yatakuwa na mbabaiko mpaka viumbe vipotee dhidi ya dini zao, hapo ndipo atadhi- hiri kama vimondo vyenye kuruka na kuijaza ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa dhuluma na ujeuri.”

Na mna: Kutoka kwenye kitabu Faraidus-Samtwayni kwenye ukurasa uliotajwa, kutoka kwa Al-Baqir kutoka kwa baba zake kutoka kwa Ali bin Abu Talib (a.s.)- ameivusha: “Mahdi ni kutoka kwenye kizazi changu, atakuwa na ghaibu ambayo ndani yake mataifa yatapotea – akaendelea mpaka akasema- na ataijaza ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa dhuluma na ujeuri.”[50]

Na mna: Kutoka kwa Abu Jafar Muhammad Al-Baqir amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema:

“Ni uzuri ulioje kwa atakayemdiriki Qaimu wa Ahlul–Bait wangu naye huku akimfuata wakati wa ghaibu yake kabla ya kusimama kwake, huku akiwapenda vipenzi vyake na akiwafanyia uadui maadui zake, basi huyo ni mion– goni mwa marafiki zangu na wenye mapenzi kwangu, na ndiye mbora kwangu siku ya Kiyama katika umma wangu.”

Na mna: Kutoka kwa Abu Basira kutoka kwa As–Sadiq Jafar bin Muhammad kutoka kwa baba zake kutoka kwa kiongozi wa waumini (a.s.) amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema: “Mahdi ni kutoka kwenye kizazi changu jina lake ni jina langu na kuniya yake ni kuniya yangu, ndiye mtu afananaye na mimi sana tabia na maumbile, atakuwa na ghaibu na mataifa yatakuwa na mbabaiko mpaka viumbe vipotee dhidi ya dini zao, hapo ndipo atadhihiri kama vimondo vyenye kuruka na kuijaza ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa dhuluma na ujeuri.”

Kutoka kwake mfano wa hiyo isipokuwa alisema: “Hapo ndipo ataku– ja kama vimondo vyenye kuruka atakuja na akiba ya manabii (a.s.).”51

Na katika ukurasa wa 494 mna: Kutoka kwake kutoka kwa Jabir bin Yazid Al–Jaafiy amesema: Nilimsikia Jabir bin Abdullah Al–Ansar akisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) aliniambia: “Ewe Jabir! Mawasii wangu na maimamu wa waisilamu baada yangu wa kwanza wao ni Ali kisha Hasan kisha Husein kisha Ali bin Husein kisha Muhammad bin Ali maarufu kwa jina la Al–Baqir na utamdiriki ewe Jabir, basi utakapokutana naye mpe salamu kutoka kwangu.

Kisha ni Jafar bin Muhammad kisha Musa bin Jafar kisha Ali bin Musa kisha Muhammad bin Ali kisha Ali bin Muhammad kisha Hasan bin Ali kisha Al–Qaimu. Jina lake ni jina langu, kuniya yake ni kuniya yangu mwana wa Hasan bin Ali, huyo ndiye ambaye Mwenyezi Mungu atafungua Mashariki ya ardhi na Magharibi yake mikononi mwake. Huyo ndiye ambaye atakuwa ghaibu dhidi ya vipenzi vyake, hatothibiti kwenye imani ya kuamini uimamu wake ila ambaye Mwenyezi Mungu ameutahini moyo wake kwa ajili ya imani.”

Hakika Mahdi tuliyeahidiwa akiwa si Imam mtakasifu na akawa ni mtu wa kawaida kama waisilamu wa kawaida basi hakutokuwa na munasaba wowote kati yake na kudhihiri na Masih (a.s.) kwa pamoja, ilihali yeye ni miongoni mwa manabii watano watukufu mno ili ampe nguvu Mahdi na kuwalingania wakristo waamini unabii wa Mtukufu Nabii (s.a.w.w.), hivyo ni lazima Mahdi tuliyeahidiwa awe Imam mtakasifu.

Na kwa kuwa uimamu wenye utakaso si jambo lililopo chini ya madai bali ni jambo linalohitaji uainishaji kutoka kwa Mola na nasi ya Mtume inay– oonyesha hilo, na kwa kuwa hilo halijatokea kwa wasiokuwa maimamu kumi na wawili (a.s.) hata katika kiwango cha madai tu achia mbali dalili na hoja, na kwa kuwa vifo vya maimamu kumi na mmoja waliotangulia vimethibiti na miili yao imezikwa maeneo maalumu na amebakia Imam wa kumi na wawili pekee ndiye hakijajulikana kifo chake mpaka leo basi ni lazima tuamini kuwa uhai wa Imam huyu unaendelea kuanzia pale alipoza– liwa mpaka atakapodhihiri zama za mwisho ili afae kupewa nguvu na Masihi (a.s.).

Sayyid Samiy Al–Badriy amezungumzia hilo kwa kusema: “Hakika kudhi– hiri kwa Isa kutahitaji

mjumuisho wa kielimu na kiuongozi kutoka kwa Mahdi tuliyeahidiwa kwa kuzingatia yeye (Isa) atasimama kama shahidi wake na wa ujumbe ambao wito wake utaenezwa (na Mahdi) na atakuwa mfuasi wake. Mahdi kwa mtazamo wa kisunni hatokuwa na uwezo wa kumjumuisha Masihi (a.s.) bali yeye si mwenye uwezo wa kuyajumuisha makundi ya kiisilamu.

Hatokuwa na uwezo wa kumjumuisha Masihi kwa sababu Masihi ni Nabii na Mtume mtakasifu na mwenye kupewa nguvu kwa miujiza ya Mola, na mtu wa mfano huo hawezi kujumuishwa na mwanadamu asiyepewa nguvu na miujiza, wala utakaso na elimu timilifu. Na hatokuwa na uwezo wa kuu- jumuisha umma wa kiisilamu bila ya nguvu ya muujiza wa Mola na utaka- so na elimu timilifu."52

Njia ya kihistoria

Tunaweza kuiunda kwa fafanuzi tatu:

Hakika historia imethibitisha kuzaliwa kwa Imam Mahdi (a.s.) na wala haijathibitisha kufariki kwake, jambo linaloonyesha kuwa uhai wake unaen- delea, na kwa kuwa uwepo wake hatuoni na wala hatumwoni mtu yeyote aitwaye Mahdi mwana wa Imam Hasan Al-Askari basi ni lazima atakuwa na uhai wa siri usioonekana kwa watu.

Historia imethibitisha kuwa Imam Mahdi ameonekana kwa macho mara kwa mara zama za ghaibu yake, na vimeandikwa vitabu mbalimbali juu ya hilo mfano wa kitabu Tabsiratul-Waliy Fimanr-Raa Al-Qaim Al-Mahdiy cha Sayyid Hashim Al-Bahraniy. Sheikh Abu Talib At-Tajlil At-Tabriziy ndani ya kitabu chake amewataja watu mia wawili sitini na sita53 waliomwona Imam Mahdi zama za ghaibu yake ndogo na akawa ametaja visa vyao na akatenga sura maalumu ya waliomwona Imam zama za ghaibu yake kubwa.

Akataja vitabu ishirini ambavyo ndani yake waandishi wake wameta- ja visa na habari za kihistoria kuhusu hilo, sisi hapa tutataja kisa ali- chokitoa Sayyid Sadrud-Dini As-Sadr ndani ya kitabu chake Al-Mahdi akinukuu kutoka kwa Sheikh Abdul-Wahabi As-Shaaraniy ndani ya kitabu chake Tabaqatul-Irfai kuhusu hali ya Sheikh Hasan Al-Araqiy amesema: "Nilikwenda kwake pamoja na bwana wangu Abul Abbas Al-Harithiy akasema: Unaniidhinia nikusimulie simulizi yangu kuanzia mwazo wangu mpaka muda huu kama vile ulikuwa rafiki yangu tangu udogoni mwangu?

Nikamwambia: Ndio, akasema: Nilikuwa kijana kutoka Damascus, nilikuwa fundi na siku ya ijumaa tulikuwa tukijikusanya kwa ajili ya upuuzi, michezo na pombe, basi siku moja nikafikiwa na tahadhari kutoka kwa Mwenyezi Mungu, je umeumbwa kwa ajili ya hili? Basi nikaacha waliyokuwa nayo na nikawakimbia wakanifuata nyuma laki- ni hawakunikuta. Nikaingia kasri la ukoo wa Umayya nikamkuta mtu mmoja amekaa juu ya kiti akizungumzia kuhusu Mahdi (a.s.) basi nikatamani nikutane naye.

Nikawa sisujudi sijida yoyote ila humuomba Mwenyezi Mungu aniku- tanishe naye, basi usiku baada ya Swala ya magharibi nilipokuwa nikiswali Swala ya Sunna ghafla nikamwona mtu nyuma yangu na akagusa bega langu na kuniambia: "Mwenyezi Mungu amejibu dua yako ewe mwanangu! Unataka nini

mimi ndiye Mahdi.” Nikamwambia: Utakwenda na mimi nyumbani kwangu? Akasema: “Ndiyo” basi akaenda na mimi na kusema: “Niachie sehemu ya faragha nijitenge peke yangu.” Basi nikamtengea sehemu ya faragha na akawa amekaa kwangu siku saba mchana na usiku.”54

Sheikh Ali bin Isa Al–Urbaliy amesema ndani ya kitabu Kashful– Ghummah: “Watu wananukuu visa na habari kuhusu mambo yasiyokuwa ya kawaida ya Imam Mahdi (a.s.) ambayo ufafanuzi wake ni mrefu, mimi hapa nitakutajia visa viwili tu vya karibu na zama zetu ambavyo nimesimuliwa na kundi la ndugu zetu waaminifu.

Cha kwanza: Katika mji wa Al–Hilah kati ya mto Furati na mto Dijlah kulikuwa na mwanaume aitwaye Ismail bin Hasan, akasema: Ndugu yangu Ismail ametusimulia kuwa juu ya paja lake la kushoto kulizuka kipele chenye ukubwa wa shiko la mwanadamu basi matabibu wakashindwa kutibu ndipo akaja Baghdad, matabibu walipomwona wakasema: Hauna tiba. Basi akaelekea Samrau na kuwazuru maimamu wawili Ali Al–Hadi na Hasan Al–Askari (a.s.), akashuka na kuingia nyumba ya chini ya ardhi, akamwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu na kutaka msaada kupitia Imam Mahdi (a.s.) kisha akaenda Dijlah akaoga na kuvaa nguo zake.

Basi akawaona wapanda farasi wanne wakitokea mlango wa uzio wa mji mmoja wao ni mzee aliyebeba mkuki mkononi na mwingine akiwa na upinde wenye rangi, mwenye mkuki alikuwa kuliani mwa njia na kushotini mwa njia kulikuwa na vijana wawili na yule kijana mwenye upinde alikuwa katikati ya njia. Basi mwenye upinde akamwambia: Wewe kesho utaenda kwenye familia yako. Akamwambia: Ndiyo. Basi mwenye upinde akasema: “Njoo kwangu ili nione kinachokuuma.” Basi akaenda kwake na ndipo akanyoosha mkono wake na kumkamua upele kwa mkono wake, akahisi maumivu na baadae akatulia.

Mzee mwenye mkuki akasema: “Umefaulu ewe Ismail, huyu ni Imam.” Kisha wakeendelea kwenda ilihali naye akiwa pamoja nao, Imam akasema: “Rejea.” Akajibu: “Kamwe sitokuacha.” Imam akase– ma: “Masilahi yako yako kwenye kurejea kwako.” Akasema: “Kamwe sitokuacha.” Mzee akasema: “Ewe Ismail! Hauoni aibu! Imamu anakwambia mara mbili rejea nawe unampinga!” Basi Imam akasima– ma na kutangulia mbele baadhi ya hatua, kisha akamgeukia na kumwambia: “Ewe Ismail! Utakapofika Baghdad ni lazima Abu Jafar atakutafuta, yaani Khalifa Al–Mustansir billah basi utakapofika kwake na akakupa kitu chochote usipokee, umwambie mtoto wetu Ridhaa akuandikie ujumbe kwa Ali bin Awdhu hakika mimi nitamsihi akupe unachokitaka.”

Kisha akaondoka pamoja na maswahaba zake, basi akaendelea kuwaona mpaka walipotoweka, kisha akaketi juu ya ardhi saa nzima akihuzunika na kulia kwa kutengana nao, kisha akaja Samrau basi watu wakamzunguka na kumwambia: “Tunaona uso wako umebadili– ka umepatwa na nini?” Akasema: “Je mliwajua wapanda farasi waliotoka mjini na kuelekea ufukweni mwa mto?” Wakasema: “Ndiyo, wao ni viongozi na wamiliki wa kondoo,” basi akawaambia: “Hapana, wao ni Imam na maswahaba zake, kijana mwenye upinde ndiye Imam, baraka za mkono wake zimeondoa maradhi yangu.”

Wakasema: “Tuonyeshe.” basi akafunua paja lake na hawakuona athari yoyote, ndipo wakachana nguo

yake na kumwingiza hazina na wakawazuia watu wasiende ili watu wasisongamane kwake, kisha mpelelezi kutoka upande wa Khalifa akaja hazina na kumuuliza kuhusu habari hii na kuhusu jina lake, nasaba yake, mji wake na kuhusu kwenda kwake Baghdad mwanzo wa wiki hii kisha akamwacha.

Ismail akakesha ndani ya hazina akaswali Swala ya asubuhi na akato- ka pamoja na watu mpaka wakafika mbali na Samrau na ndipo watu wakamwaga na kurejea, basi akaendelea peke yake mpaka akafika sehemu fulani akawaona watu wamesongamana kwenye jengo la kale wakiuliza kuhusu mtu aliyewasili kwao, jina lake, nasaba yake na sehemu aliyotokea. Basi walipokutana naye na wakamtambua kupitia alama zilizotajwa walichana nguo yake na kuichukua kwa ajili ya kupata baraka kwani mpelelezi wa alikuwa ameshawaandikia Baghdad na kuwajulisha hali.

Waziri alikuwa keshamwomba As-Said Radhiyu Dini amjulishe kuhusu usahihi wa habari basi Radhiyu Dini ambaye alikuwa miongo- ni mwa marafiki wa Ismail akatoka, na yeye ndiye aliyekuwa mwenye- ji wake kabla ya kwenda Samrau, basi Radhiyu Dini na kundi lake walipomuona wakateremka kutoka kwenye wanyama wao na kuwaonyesha paja lake na hawakuona chochote, ghafla Radhiyu Dini akazimia saa nzima, kisha akamshika mkono na kumwingiza kwa waziri huku akilia na kusema:

“Huyu ni ndugu yangu na mtu wa karibu mno na moyo wangu.” Ndipo waziri akamuuliza kuhusu kisa, naye akasimulia na hatimaye akawahudhurisha matabibu walioona ugonjwa wake, akawauliza mlimuona lini, wakasema kabla ya siku kumi, basi ndipo waziri akawafunulia paja la Ismail wakakuta hakuna athari yoyote, wakase- ma: “Hii ni kazi ya Masihi (a.s.),” waziri akasema: “Sisi tunamjua ni nani aliyemtibu hivyo.”

Kisha waziri akampeleka mbele ya Khalifa naye akamuuliza kuhusu

kisa, basi akamsimulia yaliyotokea na ndipo akampa dinari elfu moja. Akamwambia: “Sina ujasiri wa kuchukua hata punje moja.” Khalifa akamwambia: “Unamwogopa nani?” Akasema: “Yule aliyefanya hivi, kwani aliniambia: Usichukue chochote kutoka kwa Abu Jafar.” Khalifa akalia.

Kisha Ali bin Isa akasema: “Nilikuwa nikiwasimulia kisa hiki jamaa waliokuwa kwangu na Shamsud-Dini mwanae alikuwa kwangu ilihali mimi simjui, akasema: Mimi ni mwanae kutoka kwenye mgongo wake. Nikasema: Je uliliona paja la baba yako likiwa na jeraha? Akasema: “Mimi nilikuwa mtoto mdogo pindi paja lake lilipojeruhika, lakini nilikisikia kisa kutoka kwa baba yangu, mama yangu, karaba zangu na jirani zangu, na nililiona paja lake baada ya kuwa limepona likiwa halina athari yoyote na eneo hilo likiwa limeota vinyweleo.”

Na pia akasema: “Nilimuuliza Sayyid Swafiyud-Dini Muhammad bin Muhammad na Najmud-Dini Haydar Ibnu Al-Aysar, wakaniambia kisa hiki ni sahihi na kuwa wao wawili walimwona Ismail kipindi cha ugonjwa wake na baada ya kupona kwake, na mwanae akanisimulia kuwa baba yake alikwenda Samrau mara arubaini baada ya kupona kwake, akiwa anatamani umrudie tena wakati ule aliomwona.

Cha pili: Alinisimulia Sayyid Baqiy bin At’watu Al-Alawi Al-Hasaniy kuwa baba yake At’watu alikuwa

aamini kuwepo kwa Imam Muhammad Al–Mahdi (a.s.) na akisema: “Iwapo Imam ataniijia na kuniponya maradhi haya basi ndipo nitaamini kauli yao.” Alikuwa akikariri kauli hii, basi ndipo siku moja tukiwa tumekusanyika wakati wa Isha ghafla baba yetu akatuita nasi tukaenda haraka, akasema: “Mfuateni Imam ametoka kwangu sasa hivi.” Tukatoka na wala hatukumwona mtu. Tukarudi kwake naye akatuambia: “Mtu aliingia kwangu na kuniambia: “Ewe At’watu!” Nikasema: “Labayka.” Akasema: “Mimi ndiye Mahdi nimekuja kwako kukuponya ugonjwa wako.” Kisha akanyoosha mkono wake wenye baraka akakamua tako langu na kuondoka basi likawa kama kamba iliyofumuliwa.” Ali bin Isa amesema: “Nilimuuliza kisa hiki mwingine asiyekuwa mwanae akakikubali.”55

Kuanzia hapa Wanachuoni wa kisunni wameamini uhai wake na kuen– delea kwake kuishi au ndio matokeo ya maneno yao. Sayyid Sadrud– Dini As–Sadri amewataja baadhi yao akasema: “Miongoni mwao ni Sheikh Muhyid–Dini Ibnul Arabiy ndani ya kitabu Al–Futuhati kwa mujibu wa riwaya ya Sheikh Abdul–Wahab As–Shaaraniy ndani ya kitabu chake Al–Yawaqitu Wal–Jawahir amenukuu kutoka kwenye kitabu Is’afur–Raghibina, kwani kuwepo Imam Mahdi bin Hasan Al– Askari bila kitenganishi cha wakati kama alivyotamka wazi hilo, pia kuwepo kifo cha Imam Hasan Al–Askari mwaka mia wawili na sitini vinalazimu uhai wa Mahdi na kuendelea kuishi mpaka atakapodhihiri, au kusema atakufa kisha Mwenyezi Mungu atamfufua tena kwa uwezo wake. Na wala sidhani Sheikh Muhyid–Dini anaridhia kunasibishwa na dhana hii ya mwisho.

Na miongoni mwao ni Sheikh Abdul–Wahabi As–Shaaraniy ndani ya kitabu chake Al–Yawaqitu Wal–Jawahir kama ilivyo ndani ya kitabu Is’afur–Raghibina, amesema: “Mahdi bin Imam Hasan Al–Askari amezaliwa usiku wa nusu ya Shaabani mwaka mia wawili hamsini na tano na bado yupo mpaka atakapokutana na Isa bin Maryam. Hivyo ndivyo alivyonipa habari Sheikh Hasan Al–Araqiy kuhusu Imam Al– Mahdi pindi alipokiri na bwana wangu Ali Al–Khawasu56 akamwafiki.”

Miongoni mwao ni Sheikh Abu Abdullah Muhammad bin Yusuf bin Muhammad Al–Kunjiy ndani ya kitabu chake Al–Bayan Fiakhbar Sahibuz–Zaman kama kilivyonukuu kitabu Is’afur–Raghibina, amesema: “Na miongoni mwa dalili za kuthibitisha kuwa Mahdi yu hai mwenye kuendelea na uhai baada ya ghaibu yake mpaka sasa, na kuwa hakuna kizuizi katika kuendelea kwake ni kule kuendelea kwa Isa bin Maryam, Al–Hidhri na Ilyasa miongoni mwa mawalii wa Mwenyezi Mungu, na kuendelea kwa chongo Dajjal na Ibilisi mlaanifu miongoni mwa maadui wa Mwenyezi Mungu, hawa wote imethibiti kuwa bado wanaendelea kuishi kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.”57

Miongoni mwao ni Sheikh Al–Arif Al–Fadhil Al–Khawajih Muhammad Barisa ndani ya kitabu chake Faslul–Khitabi kama ilivyo ndani ya kitabu Yanabiul–Mawaddah, baada ya kuelezea kuzaliwa kwa Mahdi anayengojewa, na kuwa Mwenyezi Mungu amempa hekima na ubainifu wa maneno akiwa mtoto mchanga kama alivyomneemesha Yaya na Isa (a.s.) kwa hilo, akasema: “Mwenyezi Mungu amerefusha umri wake kama alivyorefusha umri wa Al–Hidhri (a.s.)”.58

Miongoni mwao ni Sheikh Sadrud–Dini Al–Qawnawiyu katika baadhi ya wasii wake kwa wanafunzi wake pindi alipokuwa akifariki kama ilivyo ndani ya kitabu Yanabiul–Mawaddah, amesema: “Hakika vitabu vya

tiba, hekima na falsafa vilivyo vyangu viuzeni na thamani yake wapeni sadaka mafakiri. Ama vitabu vya tafsiri, Hadithi na utawa vihi- fadhini jumba la vitabu, na someni tamko la upweke () mara elfu sabi- ni kila usiku na mnifikishie salamu kwa Mahdi (a.s.)."[59]

Nasema: Huenda mtu akasema kusema kwake huko hakuonyeshi uwepo wa Mahdi wala uhai wake, kwani huenda alisema hayo kwa kule kutaraji kuwa watadiriki kudhihiri kwake, lakini maana ya mwan- zo ndio inayofahamika.

Miongoni mwao ni Sheikh Saidud-Dini Al-Humawiy kama ilivyo ndani ya kitabu Yanabiul-Mawaddah, imenukuliwa kutoka kwenye kitabu cha Sheikh Azizi bin Muhammad An-Nasafiy pindi anapozungumzia utaratibu wa mawalii: "Hakika Mwenyezi Mungu alichagua mawalii kumi na wawili ndani ya umma huu kutoka Ahlul- Bait akawafanya makhalifa wa Nabii Wake mtukufu (s.a.w.w.)." mpaka akasema: "Ama Walii wa mwisho ambaye ndiye Khalifa wa mwisho wa Nabii, ambaye ni walii, naibu wa kumi na wawili na hitimisho la mawalii ni Mahdi mwenye zama hizi."[60]

Miongoni mwao ni Sheikh Shihabud-Dini Al-Hindi maarufu kwa jina la mfalme wa Wanachuoni ndani ya kitabu chake Hidayatus-Suadai kama ilivyo ndani ya kitabu Ad-Durar Al-Musawiyah, amesema anapozungumzia maimamu kumi na wawili: "Wa tisa kutoka katika kizazi cha Husein ni Imam Hoja wa Mwenyezi Mungu Al-Qaimu na yeye ni ghaibu na ana umri mrefu kama walivyo waumini Isa, Ilyasa na Al-Hidhri. Na katika makafiri ni kama Dajjal na As-Samiriy."

Miongoni mwao ni zaidi ya mmoja kati ya waheshimiwa na wanafasi- hi, kwani linalodhihiri kutoka kwenye mashairi yao ya kiarabu na kia- jemi yaliyotajwa ndani ya kitabu Yanabiul-Mawaddah na vinginevyo katika vitabu vya fadhila ni kuwa wao wanaamini uhai wa Mahdi mwenye kungojewa na kuwa yeye yu hai anaruzukiwa pale wanapom- sifu kuwa ana utawala, uimamu, ukhalifa na unaibu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kuwa yeye ndiye kiunganishi katika rehema za Mola."[61]

Katika ufafanuzi wa tatu tutategemea ule aliouandika Sayyid As-Shahid Muhammad Baqir As-Sadri (r.a.) ameandika: "Hakika ghaibu ni uzoefu walioupata baadhi ya watu muda unaokaribia miaka sabini, nao ni muda wa ghaibu ndogo, ili kufafanua hilo tunaanza kukupa fikira fupi kuhusu ghaibu ndogo.[62]

Hakika ghaibu ndogo huelezea kipindi cha mwanzo cha uimamu wa kiongozi mwenye kungojewa (a.s.), Imam huyu alipangiwa kuwa asionekane kwa watu wote tangu atakapochukua uimamu na aendelee kuwa mbali na matukio kwa jina lake japokuwa yupo karibu nayo kwa moyo wake na akili yake.

Ilionekana kuwa iwapo ghaibu hii ikija ghafla basi italeta tatizo kubwa kwa raia juu ya uimamu ndani ya umma wa kiisilamu kwa sababu raia hawa walikuwa wamezoea kuwasiliana moja kwa moja na Imam ndani ya kila zama, wakiamiliana naye na kurejea kwake katika utatuzi wa matatizo mbalimbali, hivyo iwapo Imam ghafla akiwa mbali na macho ya wafuasi wake na wakahisi mahusiano yao ya kiroho na kifikra yamekatika, basi ghaibu[63] hii itasababisha hisia za ghafla zenye mtik- isiko mkali unaoweza kung'oa jamii nzima na kuifarakisha, hivyo ikawa ni lazima kuandaa mazingira ya ghaibu hii ili raia hawa waun- gane nayo hatua kwa hatua na kuwiana nayo kidogo kidogo kwa kufu- ata misingi yake.

Maandalizi haya yalikuwa ni ghaibu ndogo ambayo Imam humo aliji- ficha dhidi ya mazingira ya watu wote isipokuwa daima alikuwa na mawasiliano na wafuasi wake kwa njia ya mawakili wake na manaibu wake na waaminifu miongoni mwa maswahaba zake ambao wanatengeneza kiungo kati yake na watu wanaoamini njia yake ya uimamu.[64]

Kituo hiki cha unaibu wa Imam zama hizi za ghaiba ndogo kilikuwa chini ya manaibu wanne ambao raia wote wamekongamana juu ya uchamungu wao, udhibiti wao na usafi wao walioishi nao. Na wao ni kama ifuatavyo:

● Uthman bin Said Al-Amri Muhammad bin Uthman Al-Amri Abul Qasim Husein bin Ruh

● Abul Hasan Ali bin Muhammad As-Sumriy

Hawa wanne[65] walifanya jukumu hili la unaibu kwa utaratibu huo uliota- jwa, kila alipofariki mmoja mwingine aliyefuata alichukua nafasi yake kwa kuainishwa na Imam Mahdi (a.s.).

Naibu alikuwa akiwasiliana na wafuasi na kupeleka maswali yao kwa Imam na kumpelekea matatizo yao na huku akibeba majibu yake kwao kwa mdomo na mara nyingine kwa maandishi.[66] Hivyo jamuhuri iliyokuwa haimuoni Imam ikawa imepata pole na kifuta machozi kwa njia ya barua hizi na mawasiliano haya yasiyokuwa ya moja kwa moja. Saini zote na barua zote zilizokuwa zikitoka kwa Imam Mahdi (a.s.) zilikuwa za hati moja ya namna moja[67] muda wote wa manaibu wote wanne ambao ulidumu kipindi cha miaka sabini.

As-Sumriy ndiye aliyekuwa naibu wa mwisho, hivyo alitangaza kumalizika kipindi cha ghaibu ndogo ambacho kilijitofautisha kwa kuwa na manaibu maalumu na hapo ikaanza ghaibu kubwa ambayo haina watu maalumu walioainishwa kwa ajili ya ukiungo kati ya Imam kiongozi na wafuasi wake.

Mabadiliko ya kutoka kwenye ghaibu ndogo hadi ghaibu kubwa yameelezea jinsi ghaibu ndogo ilivyofanikiwa kutimiza malengo yake na jukumu lake kukamilika kwa sababu kitendo hiki cha hatua kwa hatua kiliwazuia wafuasi dhidi ya hisia za ghafla zenye mtikisiko mkali wa kutokwa na Imam kwa sababu ya ghaibu na hivyo ikafaniki- wa kuandaa mazingira ya wafuasi kulingana na ghaibu na kuwazoesha kidogokidogo ili waipokee fikira ya unaibu usio maalumu wa Imam.

Na kwa ajili hii unaibu ulibadilika kutoka kwa watu maalumu waliotangazwa kwa nasi[68] mpaka kuwa ni mfumo wa watu wote,[69] nao ndio mfumo wa Mujtahid mwadilifu mjuzi wa mambo ya dunia na dini, hiyo ni kutokana na kubadilika ghaibu ndogo na kuwa ghaibu kubwa.

Na sasa unaweza kuchukua msimamo kutokana na maelezo yaliyotan- gulia ili uweze kutambua kwa uwazi kabisa kuwa Mahdi ni ukweli mtupu walioishi nao baadhi ya watu, na manaibu na mabalozi wakau- tambulisha muda wa miaka sabini kupitia muamala wao na watu wengine.

Muda wote huu hakuna mtu yeyote aliyeona kwao mchezo mchafu katika maneno, au ujanja fulani katika hilo au dosari zozote katika nukuu, sasa je unadhani uongo unaweza kudumu miaka sabini na

watu wanne wakautumia kwa namna moja tena kwa kufuatana mmoja baada ya mwingine na wote wakiwa wameafikiana juu yake? Na isitoshe waendelee kuutumia kana kwamba ni kadhia wanayoishi nayo wao wenyewe na kuiona kwa macho yao bila kutokea kitu chochote kina- chozua shaka, na bila ya kuwa na uhusiano maalumu wa pekee kati ya wanne unaotoa fursa ya kula njama ya kukubaliana, na huku kutokana na mwenendo wao wanapata sifa ya watu kuwaamini wao wenyewe na kadhia yenyewe wanayodai kuwa wanaiona na kuishi nayo?!

Kuna usemi: Njia ya mwongo ni fupi, na hata mantiki ya maisha inathibitisha hilo kuwa ni muhali kivitendo kwa mujibu wa hesabu za matarajio uongo kudumu kwa namna hii na kwa muda wote huu na ndani ya mahusiano kama hayo ya kuchukua na kutoa, kisha upate kuaminiwa na wote wanaouzunguka.

Hivyo tunatambua kuwa hali ya ghaibu ndogo tunaweza kuichukulia kama uzoefu wa kivitendo ili kuthibitisha hali halisi ya maudhui husi- ka na kumkubali Imam kiongozi kuanzia kuzaliwa kwake, uhai wake, ghaibu yake70 na tangazo lake kuu kuhusu ghaibu kubwa ambayo kwa mujibu wake amefichwa mbali na mazingira ya watu na wala hajajifichua kwa yeyote.71”72

---

1. Usulul-Kafiy 1: 327, kitabu cha hoja, mlango wa kielelezo na maelezo kwa mwenye nyumba.
2. Usulul-Kafiy 1: 327, kitabu cha hoja, mlango wa jina la aliyemwona (a.s.).
3. Kamalud-Dini 2: 424, mlango wa 42.
4. Man’huwa Al-Mahdiy cha A Abu Talib Tajlil At-Tabrizi: 460 – 506.
5. Kamalud-Dini 2: 442, na imepokewa kutoka kwake ndani ya kitabu Biharul- An’war 52: 30, mlango wa 26.
6. Al-Irshad cha Sheikh Al-Mufid 2: 336.
7. Difau Anil-Kulayniy 1: 567 – 568, cha Hasan Hashim Thamir Al-Amidiy.
8. Ilzamun-Naswibu Fiithbatil-Hujatil-Ghaib cha Sheikh Ali Al-Yazdi Al-Hairiy 1: 321 – 440.
9. Al-Mahdiyyu Al-Muntadhar Finahjil-Balagha cha Sheikh Mahdiyyu Faqihi Iymaniy: 16 – 30.
10. Al-Imam At-Thani Ashar cha Sayyid Muhammad Said Al-Musawiy: 27 – 70. Muhakiki wa kitabu hiki pambizoni mwa kitabu amekusanya wapokezi thelathini wa kisunni waliompita mwandishi. Angalia pambizoni mwa kitabu husika: 72 – 89. Al-Mahdiyyu Al-Maw’udu Al-Muntadhar Indaahlis-Sunah Wal-Imamiyah cha Sheikh Najmud-Dini Al-Askari 1: 220 – 226.
11. Difau Anil-Kafiy 1:568.
12. Tazama Usulul-Kafiy 1: 421, kitabu cha Hoja, mlango wa mazazi ya Abu Muhammad Hasan bin Ali (a.s.). Kamalud-Dini 1: 40 kwenye utangulizi wa mwandishi. Al-Irshad 2: 321. Iilamul-Waraa Biaalamil-Huda cha Al-Fadhlu bin Hasan At-Tabari: 357. Tazama Kamald-Dini 2: 375, mlango wa 43 aliyemwona Al-Qaimu (a.s.).
13. Sura Maryam: 12.
14. As-Swawaiq Al-Muhriqah: 256, Darul-Kutubi Al-Ilmiyah.
15. Al-Fusulul-Muhimmah cha Ibnu As-Swabagh Al-Malikiy: 253. Al-Irshad cha Sheikh Al-Mufid 2: 274 na ufuatao.
16. At-Tatimah Fitawarikhil-Aimah cha Sayyid Tajud-Din Al-Amiliy mwanazuoni wa karne ya kumi na moja hijiriya, kilisambazwa na taasisi ya Al- Biithah ya huko Qum takatifu. Pia rejea As-Swawaiq Al-Muhriqah cha Ibnu Hajar: 312 – 313, pale anapotaja baadhi ya karama za Imam na mwenendo wake.
17. At-Tatimah Fitawarikhil-Aimah cha Sayyid Tajud-Din Al-Amiliy mwanazuoni wa karne ya kumi na moja hijiriya, kilisambazwa na taasisi ya Al-Biithah ya huko Qum takatifu. Pia rejea As-Swawaiq Al-Muhriqah cha Ibnu Hajar: 312 – 313,

pale anapotaja baadhi ya karama za Imam na mwenendo wake.
18. Al–Irshad cha Sheikh Al–Mufid 2: 281 na ufuatao. As–Swawaiq Al–Muhriqah: 312 – 313. Ameleta kisa cha mazungumzo yaliyotokea baina ya Imam Al–Jawad na Yahya bin Aktham zama za Al–Maamun, na kuonyesha jinsi gani Imam (a.s.) alivyoweza kuthibitisha ujuzi wake wa kielimu na uwezo wake wa kumfumba mtu mdomo, ilihali Imam akiwa badi na umri mdogo.
19. Rejea Al–Majalis As–Saniyyah cha Sayyid Al–Amin Al–Amiliy 2: 468, kisa hiki ni mashuhuri kimenukuliwa na Sunni na Shia. Rejea Sahahul–Akhbar cha Muhammad Sirajd–Dini Ar–Rifaiy: 44, amenukuu kutoka kwenye kitabu Imam As– Sadiq Wal–Madhahib Al–Arbaah cha Asad Haydar 1: 55. Amesema Ibnu Hajar ndani ya kitabu chake As–Swawaiq Al–Muhriqah kuwa: "Jafar As–Swadiq, watu walinikuu kutoka kwake elimu ambazo zilibebwa misafara na misafara na sauti yake ikaenea miji yote. Maimamu wakubwa kama vile Yahya bin Said, Ibnu Jariji, Malik Sufiyani wawili, Abu Hanifa, Shaabah na Ayubu As–Sakhtiyaniy wote wamepokea kutoka kwake...."
20. Sula la Imam kuwa mjuzi kuliko watu wote wa zama zake ni suala linalokubaliwa na Shia imamiya wote, rejea kitabu Al–Babu Al–Hadi Ashara cha Al–Allamah Al–Hiliy: 44, kuna mitihani mingi waliyofanyiwa maimamu ili kuthibitisha dai hili na hatimaye walifaulu. Rejea As–Swawaiq Al–Muhriqah cha Ibnu Hajar: 312, yeye katika suala hili kanukuu kwa upana zaidi katika kisa cha Yahya bin Aktham na Imam Al–Jawad (a.s.).
21. Hakika imani ya uimamu wa maimamu uliwagharimu wafuasi wao gharama ghali, na hili ni suala lililothibiti ndani ya historia na wala hamna njia ya kulikanusha, na lililopo huthibitisha lisilokuwepo. Rejea kitabu Muqatilu At– Talibina cha Abul Farji Al–Asbahaniy.
22. Maimamu waliwausia hilo wafuasi wao kama riwaya nyingi zisemavyo. Rejea kitabu Usulul–Kafiy 1: 392, kitabu cha hija, mlango wa "wajibu wa watu pindi wanapomaliza kutekeleza ibada zao ni kuja kwa Imam na kumuuliza maswala mbalimbali juu ya dini yao na kumtambulisha mapenzi yao na utawal– ishaji wao kwake."
23. Isharatu Ilal–Imam Al–Mahdi.
24. Yaani ni lazima awe mbora kuliko watu wote na mjuzi kuliko watu wote kama inavyoaminiwa na Shia Imamiya.
25. Anakusudia kuwa kule kushindwa kumjaribu Imam mbele za watu ili kudhi– hirisha hali yake halisi.
26. Sura Maryam: 12.
27. Bahthu Hawlal–Mahdi cha Sayyid As–Shahid: 93 – 99, uhakiki wa Dk. Abdul Jabarah Shararah. Baadhi ya mashia wapenzi wa karibu walimwona Imam Mahdi na wakawasiliana naye na wakapokea kutoka kwake kama ilivyokuwa kwa njia ya mabalozi wanne. Rejea kitabu Tabsiratul–Waliy Fiman'raa Al–Qaim Al–Mahdi cha Al–Bahraniy. Pia rejea Al–Irshad cha Sheikh Al–Mufid: 345. Rejea kwa undani zaidi kitabu Ad–Difau Anil–Kafiy cha Sayyid Thamir Al–Amidi 1: 535 na ufuatao.
28. Chunguza kwa makini, anachodai ni kuwa inawezekana kielimu lakini haija– tokea kivitendo, ukweli ni kuwa majaribio mengi ya anga na kufika kwenye sayari na viambata vingine vya ardhi ni mambo yaliyotimia mwishoni mwa karne ya ishirini.
29. Ndio, hakuna kigezo cha kielimu kinachokataa nadharia hii, bali ni kuwa wasomi wa tiba hivi sasa wanajishughulisha sana kutaka kurefusha umri wa mwanadamu na mpaka sasa kuna majaribio mengi yamefanywa katika hili. Kitendo hicho ni dalili tosha yenye nguvu ithibitishayo uwezekano wa kielimu.
30. Jaribio hili linasisitizwa sana na matabibu na masomo ya tiba na wao wana ushahidi mbalimbali katika suala hili, na huenda suala hili ndilo lilolowasukuma kufanya majaribio ya kurefusha umri wa kawaida wa mwanadamu, na kama inavyozoeleka kuwa jaribio la kwanza huwa ni kuwafanyia wanyama kwani ni rahisi kwao, na hakuna kizuizi kinachozuia kufanya jaribio hilo kwa mwanadamu.
31. Maswali haya anayoyatoa Sayyid Shahid yanalenga kuimarisha ukweli muhimu nao ni kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anapombashiri Mahdi na hali isiyokuwa ya kawaida kwa wanadamu basi ndani ya utabiri huo anatoa habari za maelezo ambayo tayari yameshatangulia yaliyotimia kwa uwezekano wa kiviten– do baada ya kusisitiza uwezekano wa kielimu. Yaani kitendo cha mwanadamu kubakia muda mrefu usiokuwa wa kawaida tayari kimeshaelezwa na Qur'an na Hadithi tukufu sehemu nyingi katika masuala ya kifizikia, ulimwengu na uhai. Rejea kitabu Al–Qur'an Wal–Ilmi Al–Hadith cha Dk. Abdur–Razaq Nawfal.
32. Anaashiria kuwa hii ni aina pia ya muujiza nao ni kipawa maalumu kutoka kwa Mola, na jambo hili mwisilamu hawezi kulikanusha baada ya Kitabu kituku– fu kuzungumzia jambo kama hilo na hasa Qur'an kama ilivyozungumzia umri wa Nabii Nuhu na mambo mengine ya aghaibu. Zaidi ya hapo masunni wengi watawa na wanairfani wanaamini kuwa karama na

miujiza huwatokea mawalii, wachamungu na watu wakaribu na Mola. Rejea At–Taju Al–Jamiu Lil–Usul 5: 228, kitabu cha utawa.

33. Anaashiria kauli ya Mwenyezi Mungu: “Utukufu ni wake ambaye alimpeleka mja wake usiku kutoka Msikiti mtukufu mpaka Msikiti wa mbali…” Sura Al–Israi.

34. Anaashiria hali ya hewa angani na urefu wa masafa tokea ardhini na kuyaka– ta kwa muda wa masaa mengi au siku nyingi. Mambo haya yamedhihiri zama zetu hizi mwishoni mwa karne ya ishirini.

35. Anaashiria jukumu la mabadiliko aliloandaliwa Imam Mahdi (a.s.) katika kiwango cha ubinadamu kama isemavyo haditihi tukufu: “Ataijaza ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa dhuluma na ujeuri.” Na jukumu hili wameafikiana kwalo Wanachuoni wote wa kiisilamu. Ama tofauti zilizopo ni kwenye baadhi tu ya vipengele visivyokuwa vya asili, na kuanzia hapa swali alilolitoa Sayyid Shahid limekuwa ni la kimantiki sana.

36. Aya tukufu: “Na akakaa nao miaka elfu kasoro miaka hamsini..” Sura Ankabuti: 14.

37. Swali linaelekezwa kwa waisilamu wanaoamini Qur’an na Hadithi tukufu. Wanachuoni wa kisunni wamepokea umri mrefu zaidi ya huo kwa asiyekuwa Nuhu. Rejea kitabu Tahdhibul–Asmai Wallughati cha An–Nawawi 1: 176, wala haifai mtu kujenga hoja kuwa hilo la Nuh limeelezwa na Qur’an kwa uyakinifu na pia linamuhusu Nabii aliyetumwa Nuhu (a.s.), ama hapa kwa Mahdi hatuna nassi yakinifu wala jambo linalohusiana na Mtume.

Jibu: Kwanza, hakika jukumu ni moja nalo ni kuondoa dhuluma na ufisadi, kama ambavyo jukumu alikabidhiwa Nabii vilevile hapa jukumu amekabidhiwa yule mteule wa Mola mtukufu kama riwaya sahihi zisemavyo. Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: “Hata kama dunia haitobakiwa ila na siku moja basi ni lazima Mwenyezi Mungu atairefusha siku hiyo mpaka amlete mtu kutoka watu wa nyum– ba yangu atakayeijaza ardhi usawa na uadilifu….” At–Taju Al–Jamiu Lil–Usul 5:343.

38. Yaani suala hilo linakuwa muujiza, nalo limezungumzwa na Qur’an na Sunna sahihi. Muujiza ni ukweli ulioambatana na wito wa manabii na dai lao la kuwa mabalozi wa Mola, nalo ni jambo asiloweza mwisilamu kulikanusha au kulitilia shaka, bali hata asiyekuwa mwisilamu hushirikiana na mwisilamu katika kuamini miujiza.

39. Sura Anbiyai: 69.

40. Anaashiria kauli ya Mwenyezi Mungu: “Mara tulimpelekea Wahyi Musa: Piga bahari kwa fimbo yako. Mara ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mwamba mkubwa.” Sura Shuaraa: 63.

41. Anaashiria kauli ya Mwenyezi Mungu: “Na wala hawakumuua wala hawakumsulubu, lakini alifananishwa kwao…”. Sura Nisaa: 157.

42. Rejea Sirat Ibnu Hisham 2: 483, amenukuu tukio hili.

43. Amefafanua kauli hii kunako suala hii ndani ya kitabu chake Falsafatuna: 295 na 299 rejea huko.

44. Rejea kitabu Falsafatuna: 282 na ufuatao

45. Rejea ufafanuzi wa nadharia hii ndani ya kitabu Al–Ususu Al–Mantiqiya Lil– Istiqrai cha Sayyid Shahid As–Sadri (q.s.), humo Imam kafanikiwa kufichua umuhimu na hatari kwa mujibu wa nadharia ya maarifa kwa ujumla.

46. Ni uchambuzi uliotokana na uchambuzi wa kitabu Bahthu Hawlal–Mahdiy cha Sayyid Shahid As–Sadri (q.s.): 65 – 80, uhakiki na maelezo ya Dk. Abdul Jabbar Shararah.

47. Yanabiul–Mawaddah 3: 296, mlango wa sabini na nane.

48. Yanabiul–Mawaddah 3: 297, mlango wa sabini na nane.

49. Yanabiul–Mawaddah 3: 310, mlango wa 80

50. Yanabiul–Mawaddah 3: 386, mlango wa 94

51. Yanabiul–Mawaddah 3: 397

52. Shubhat Warudud, mzunguko wa nne: 32.

53. Man’huwal–Mahdiy: 460.

54. Al–Mahdiy: 149 cha Sadrud–Din As–Sadri.

55. Yanabiul–Mawaddah 3: 315 – 317.

56. Is’afur–Raghibina: 157.

57. Is’afur–Raghibina: 227.

58. Yanabiul–Mawaddah 3: 352, mlango wa themanini na saba.

59. Yanabiul–Mawaddah 3: 352, mlango wa themanini na saba.

60. Yanabiul-Mawaddah 3: 352, mlango wa themanini na saba.
61. Al-Mahdiy: 146 – 148.
62. Rejea kitabu Al-Ghaybatu As-Sughra cha Sayyid Muhammad As-Sadri, amechambua kwa upana zaidi.
63. Anaashiria ghaibu kubwa.
64. Rejea Tabsiratul-Waliy Fimanraa Al-Qaim Al-Mahdiy cha Sayyid Hashim Al-Bahraniy. Difau Anil-Kafiy cha Sayyid Thamir Al-Amidiy 1: 568 na ufuatao.
65. Rejea wasifu wa hawa wanne ndani ya kitabu Al-Ghaybatu As-Sughra cha Sayyid Muhammad As-Sadri, sehemu ya tatu: 395, kimesambazwa na Darutaaruf Lilmatbuati Bayrut 1980.
66. Tahriri hizi hujulikana kwa jina la 'Tawqiati", nazo ni majibu ya maandishi na ya mdomo ambayo yalinukuliwa kutoka kwa Imam Mahdi (a.s.). Rejea kitabu Al- Ihtijaj cha Tabarasiy 2: 523 na ufuatao.
67. Kilichomakinika kwa wanafasihi wa sasa na wazamani ni kuwa "Mfumo ndio mtu mwenyewe" kauli hii ni sahihi. Kuanzia hapa ndio maana tumeona na kusikia kuwa wanafasihi wengi na wanamashairi kwa kusoma tu msitari wa shairi au nathari hutambua kuwa ni la nani au ni la fulani, si kwa chochote ila ni kwa sababu mfumo ndio mtu mwenyewe. Na kuwa kila mwandishi ana alama na chapa maalumu katika maandishi yake ambayo kwayo unaweza kumtofautisha na mwingine, ukiachia mbali kuwa hati ya mtukufu (a.s.) inatofautiana na hati nyingine.
68. Anaashiria manaibu wanne waliotajwa.
69. Kiistilahi unaitwa "Marejeo makuu ya kidini" na hapa zinaonekana sifa ambazo Shahid anaona ni lazima mtu awe nazo ili afae kuwa marejeo makuu ya kidini.
70. Imam Mahdi kukutana na wafuasi wake kwa njia ya manaibu wake na mawakala wake au kwa njia nyinginezo mbalimbali ni ukweli wa kihistoria ambao hauna njia ya kukanushwa, ukiachia mbali dalili nyingine nyingi zina- zotegemea utoaji habari wa yule ambaye ni lazima kumsadikisha. Kisha suala hili ni muktadha wa Hadithi mutawatiri kama vile Hadithi isemayo: "Atakayefariki huku hamjui Imam wa zama zake basi amekufa kifo cha kijahiliya." Na nyingine- zo, nazo zinakubalika na makundi mengi ya kiisilamu, hizo zote zinabatilisha shaka za wenye kushakia uwepo wa Imam Mahdi na kuendelea kwake kuishi. Rejea kitabu Al-Ghaybatu As-Sughra cha Sayyid Muhammad As-Sadri: 566.
71. Kuna Tawqii tukufu ya Imam Mahdi (a.s.) inayoonyesha kuwa hatoweza kuonekana waziwazi baada ya ghaibu kubwa, suala hili Shia Imamia wote wamekongamana juu ya hilo. Rejea kitabu Munaqashatul-Mas'alah Fil- Ghaybatus-Sughra cha Sayyid Muhammad As-Sadri: 639 na ufuatao.
72. Bahthu Hawlal-Mahdi: 108 – 111, uhakiki na maelezo ya Dk. Abdul Jabbar Shararah.

Sura Ya Tatu

Umuhimu wa uwelewa wa wazo la Mahdi kiakida katika madhehebu ya Ahlul-Bait

Akida yoyote sawa iwe ya kidunia ambayo chanzo chake huwa ni mwanadamu mwenyewe au iwe ya kimola ambayo chanzo chake ni Mwenyezi Mungu mtukufu ni lazima iwe na maana ya kibinadamu, hivyo ikiwa ni ya kidunia basi huwa imetokana na mazingira ya mwanadamu na huwa inaonyesha kuelimika kwake na shauku yake ya kutaka kufikia maisha bora zaidi.

Na kama ni ya kutoka kwa Mola basi yenyewe huonyesha rehema za Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu na jinsi anavyompenda na kuwa na pupa ya kutaka kumfikisha kwenye ufukwe wa

mafanikio. Hili ndilo analoliamini kwa yakini muumini katika msingi wa akida ya kiisilamu, hiyo ni sawa maana hii ya kibindamu iwe wazi kwake kwa ufafanuzi au vipengele vyake viwe bado ni muhtasari vikiwa vimeji- ficha ndani.

Mwanadamu huamiliana na akida mara kiakili kwa hoja na dalili na mara nyingine kimaada kulingana na jinsi akida hizi zinavyomtimizia malengo yake na kumfanikishia na kutatua matatizo ya mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Akida hizi vyovyote vile zitakavyokuwa wazi na timilifu kihoja na kidalili lakini bado kutoeleweka kwake kwa upande wa mwanadamu huzifanya zishakiwe na kutiliwa wasiwasi, au kwa uchache huwa ni nukta isiyo na msuku- mo na isiyokuwa na mwangaza ndani ya nafsi ya mwanadamu.

Akida ya kiisilamu ni kama akida nyingine za kutoka kwa Mola hatu- taraji kuwa zitafafanua malengo yake ya kibinadamu kwa undani zaidi

kwa sababu ufafanuzi wa ndani zaidi hupelekea kutilia umuhimu upande wa maada katika utu wa mwanadamu na hivyo kupingana na msingi wa akida unaoonekana waziwazi upande wa kiakili huku uki- tilia umuhimu upande wa kiroho katika utu wa mwanadamu, hivyo kwa kawaida inapasa akida hii ikomee kubainisha malengo yake ya kibinadamu kwa kiwango cha chini na kwa muhtasari, kama kauli ya Mwenyezi Mungu: “Nasi hatukukutuma ila uwe rehema kwa walimwengu.”1

Lakini wakati huohuo mwanadamu muumini kwa kuzama kiakili na kimazingatio ndani ya matokeo anaweza kufanikiwa kupata hekima inayotarajiwa na malengo ya kibinadamu ya ndani zaidi yanayotaraji- wa kwenye nyanja mbalimbali za kiakida na kisharia toka ndani ya Uislamu.

Sisi tumechambua suala la wazo la Mahdi upande wa dalili na hoja, na imetubainikia kuwa uwelewa wa wazo la Mahdi kwa madhehebu ya Ahlul-Bait ukilinganisha na uwelewa wa wazo la Mahdi kwa madhe- hebu ya madhehebu manne kwa upande wa dalili na hoja basi hulifik- isha suala hili kwenye kiwango chake cha ukamilifu na utimilifu.

Ukamilifu wake upande wa kiakida na dalili unatulazimisha na kutupelekea kuamini ukamilifu wake katika yale unayompa mwanadamu. Tofauti ambayo inapelekea mara nyingi kushakia na kuzua utata kuhusu uwelewa wa wazo la Mahdi kwa upande wa Ahlul-Bait ina- tokana na hawa kutokutazama upande wa dalili na hoja, kiasi kwamba wanatilia umuhimu upande wa kibinadamu ambao unawafanya waji- ulize: Ni faida ipi inayotokana na kuamini uwelewa wa wazo la Mahdi wenye maana zisizo za kawaida kama vile ghaiba, umri mrefu na uimamu wa mapema?

Wanaposhindwa kufikia jibu lenye kutosheleza na huku upande wa kibinadamu wa uwelewa huu ukiendelea kuzingirwa na giza na utata hupelekea kutoutambua uwelewa huo. Na kule kushindwa kwao kusawiri uelewa huu huwapelekea kukanusha uelewa huu na kuushutumu kuwa ni upenzi wa kupindukia na kitu kisicho na uwepo, na sehemu yake huleta uwelewa mwingine mbadala kuhusu wazo la Mahdi usiokuwa na vipengele hivi na wala usiohitaji ghaibu kubwa.

Wanafanya hivyo bila kujua kuwa kwa kitendo chao hiki wao wame- toka kwenye ukamilifu na kuingia kwenye upungufu na kuwa kupinga kwao vipengele hivi vya ughaibu ni kupinga johari yenye thamani ya uwelewa wa wazo la Mahdi ndani ya Uislamu, ukiachia mbali kule kupingana kwake na upande wa mantiki ambao katika mlango wa akida unalazimisha kufuata dalili na hoja popote vitakapoelekea, na wala si kuvipinga kwa kufuata hatinafsi, malengo na itikadi binafsi.

Laiti wangetuliza akili ndani ya uwelewa wa Ahlul-Bait kuhusu Mahdi (a.s.) wangeukuta upande wa kibinadamu ni kamilifu kuliko uwelewa wa madhehebu ya Sunni kuhusu wazo hilo.

Sayyid As-Shahid Muhammad Baqir As-Sadri amechukua jukumu la kubainisha upande huu ubainifu mzuri akaandika akisema:2 “Hivi sasa tunazungumzia swali la pili, nalo linasema: Kwa nini mwenyezi Mungu amjali sana mwanadamu huyu, hadi kanuni za kifizikia zisi- tishwe ili kurefusha umri wake? Kwa nini uongozi wa siku hiyo tuliyoahidiwa asiachiwe mtu atakayekuzwa na mustakabali na kuwivishwa na misukosuko ya siku hiyo tuliyoahidiwa na hatimaye abarizi uwanjani na kutekeleza jukumu lake linalongojewa. Kwa lugha nyingine ni kuwa ni ipi faida ya ghaibu hii ndefu na ni upi uhalali wake?

Watu wengi wanauliza swali hili huku wakiwa hawataki kusikia upande wa nguvu za kimola, basi sisi tunaamini kuwa maimamu kumi na wawili ni kundi la kipekee3 haiwezekani kumbadili yeyote mion- goni mwao, isipokuwa hawa wenye kuuliza wanataka ufafanuzi wa kijamii juu ya suala hili kwa mujibu wa mambo ya kimaada kwa ajili ya kazi hii ya mabadiliko makubwa na mahitaji ya uwelewa wa siku tuliyoahidiwa.

Kwa msingi huu tunasitisha kwa muda sifa tunazoamini kuwa hawa maimamu watakasifu wanazo4, na hapa tunatoa swali lifuatalo: Bila shaka sisi tunaelekea kwenye mabadiliko tunayotaraji siku tuliyoahidi- wa kwa namna ambayo unaeleweka kulingana na mwenendo wa maisha na uzoefu wake, sasa je umri huu mrefu wa kiongozi wake aliyetunzwa tunaweza kuuchukulia kuwa ni sababu miongoni mwa sababu za kufanikisha mabadiliko hayo? Na inawezekana kwake kuyatimiza na kuyaongoza kwa kiwango kukibwa zaidi?

Hilo tunalijibu kwa kukubali, hiyo ni kutokana na sababu mbalimbali, miongoni mwazo ni hizi zifuatazo: Mabadiliko makubwa yanahitaji mazingira ya kisaikolojia ya pekee ya kiongozi mwenye kufanya mabadiliko hayo, mazingira yaliyojaa utambuzi juu ya ushindi na hisia juu ya vilimwengu ambavyo kaandaliwa ili avitokomeze na kuvibadili kiustaarabu na kuvifanya ulimwengu mpya.

Kwa kadiri ambavyo moyo wa kiongozi utakavyojaa utambuzi juu ya uduni wa ustaarabu anaopambana nao na akawa na hisia za wazi kuwa wenyewe ni nukta tupu juu ya msitari mrefu wa ustaarabu wa mwanadamu ndivyo atakavyokuwa na uwezo mkubwa upande wa kisaikolojia5 katika kupambana nao na kusimama imara mbele yake na kuendeleza mabadiliko mpaka ushindi upatikane.

Ni wazi kuwa ukubwa huu wa utambuzi unaohitajika wa kisaikolojia hunasibiana na ukubwa wa mabadiliko yenyewe na ule ukubwa wa jamii na ustaarabu anaotaka kuuteketeza, hivyo kila mapambano ya jamii yanapokuwa makubwa na ustaarabu imara na mzito ndivyo unavyohitaji asilimia kubwa zaidi ya

utambuzi huu wa kisaikolojia.

Na kwa kuwa ujumbe wa siku tuliyoahidiwa ni wa kuubadili ulimwen− gu uliojaa dhuluma na ujeuri mabadiliko yaliyojumuisha kila ustaarabu wa thamani na miundo yake mbalimbali basi kwa kawaida ni lazima ujumbe umtafute mtu mwenye utambuzi mkubwa wa kisaikolojia
kuliko huo ulimwengu wote, mtu ambaye si katika vizazi vya ulimwengu huo ambavyo vimekulia ndani ya ustaarabu huo ambao anataka kuutokomeza na kuubadili kwa ustaarabu wa uadilifu na haki. Kwa sababu anayekulia ndani ya ustaarabu imara uliyojaa dunia kwa utawala wake na thamani yake na fikra zake huwa anaishi akiwa na uoga ndani ya nafsi yake mbele ya ustaarabu huo kwa sababu yeye kazaliwa ukiwa umesimama, akakuwa ukiwa imara na akafumbuwa macho yake juu ya dunia bila kukuta chochote ila nyanja mbalimbali za ustaarabu huo.

Hali hiyo ni kinyume na mtu aliyekulia ndani ya historia, ameishi duni− ani kabla ya ustaarabu huo kuiona hiyo nuru, ameona ustaarabu wa namna mbalimbali ulio mkubwa uliotawala ulimwengu mmoja baada ya mwingine kisha ukatoweka,6 ameona hayo kwa macho yake na wala si kwa kusoma ndani ya vitabu vya historia.

Kisha akaona ustaarabu ambao unakadiriwa kuwa ndio sehemu ya mwisho ya kisa hiki cha mwanadamu kabla ya siku iliyoahidiwa, ameuona ukiwa bado punje ndogo iliyongumu kuonekana, kisha akau− tazama ukiwa tayari umeshachukua nafasi yake ndani ya jamii ya mwanadamu ukisubiri fursa ili uchipue na kudhihiri

Kisha akaishi nao zama moja ukiwa umeshaanza kuchipua na kutam− baa huku mara ukianguka na mara nyingine ukufanikiwa kwa taufiki. Kisha akauongoza huku ukistawi, ukijikita na kumiliki nguvu yote ya ulimwengu kwa ukamilifu kidogokidogo, hakika mwanadamu kama huyu aliyeishi ndani ya hatua zote hizi kwa akili na uangalifu kamili

huitazama nguvu hii anayotaka kuitokomeza kwa mtazamo wa msa− fara wa historia hiyo ndefu ambayo ameishi nayo na akaishuhudia na si kwa mtazamo wa yaliyomo ndani ya vitabu vya historia tu.

Haitazami kama nguvu ya mwisho na wala haitazami kama John Jack Rusuw7 alivyokuwa akiutazama ufalme wa Ufaransa, imepokewa kuwa kitendo tu cha kuiwaza Ufaransa kilikuwa kikimtetemesha hata bila kuangalia ufalme, japokuwa alikuwa miongoni mwa wanaharakati wa kifikra na kifalasafa waliokuwa wakililia uboreshaji wa mazingira ya kisiasa zama hizo; hiyo ni kwa sababu huyu Rusuw alikulia ndani ya ufalme na akavuta pumzi yake muda wote wa uhai wake.

Ama mwanadamu huyu aliyebobea ndani ya historia yeye ana haiba ya historia, nguvu ya historia na utambuzi zaidi kuwa jamii na ustaarabu unaomzunguka ni matokeo ya siku moja miongoni mwa siku za histo− ria, kuna sababu zilizoandaliwa ndipo ukapatikana, na kuna sababu zitaandaliwa utatoweka na hivyo hautobakiwa na chochote kama ambavyo juzi na majuzi haukuwa na chochote, na kuwa vyovyote utakavyorefuka umri wa kihistoria wa ustaarabu mbalimbali na jamii mbalimbali lakini wenyewe si chochote ila ni siku chache ndani ya umri mrefu wa historia.

Je, umesoma sura ya vijana wa pangoni? Na je, umesoma kuhusu vijana hao waliomwamini Mola wao Mlezi na Mwenyezi Mungu akawazidishia uongofu?8 Wakakumbana na utawala wa ushirikina uliokuwa ukitawala zama hizo usiohurumia wala kusita kunyonga mbegu yoyote miongoni mwa mbegu za Tawhidi na yenye kujiepushana umoja wa shirki, basi nafsi zao zikaumia na wakapatwa na hali ya kukata tamaa huku madirisha ya matarajio yakifungika mbele ya macho yao, ndipo wakakiwawilia pangoni wakitafuta ufumbuzi wa matatizo yao kutoka kwa Mwenyezi Mungu baada ya ujanja wote kuwaishia huku kitendo cha batili kuendelea kutawala, kudhulumu, kuigandamiza haki na kumteketeza kila aliye na haki ndani ya moyo wake kikizidi kuwauma.

Je, unajua Mwenyezi Mungu aliwafanyia nini? Yeye aliwalaza ndani ya pango hilo miaka mia tatu na miaka tisa9 kisha akawaamsha kuto- ka kwenye usingizi wao huo na kuwapeleka kwenye mapambano ya maisha baada ya kuwa tayari umeshadondoka ule utawala uliowatisha kwa nguvu zake na kuwadhulumu, na historia ikawa haimtishi mtu wala haimtingishi aliyetulia, yote hayo ni ili vijana hawa washuhudie kudondoka kwa batili hiyo ambayo ilikuwa ikionekana kubwa juu yao kuanzia uwezo wake, nguvu yake na kuendelea kwake, na watazame mwisho wake kwa macho yao na ionekane ndogo ndani ya nafsi zao.

Na ikiwa kupitia tukio hilo la kipekee ambalo lilirefusha maisha yao miaka mia tatu mtazamo huu wa wazi ulitimia kwa vijana wa pangoni kwa kila ukubwa na uimara wa kisaikolojia basi ni jambo hilohilo lita- timia kwa kiongozi anayengojewa kupitia umri wake mrefu ambao utamwezesha kuona nguvu hizo zikiwa bado ndogo, mti mrefu ukiwa bado mbegu, na zama nyingi zikiwa bado roho.10

Zaidi ya hapo ni kuwa uzoefu unaoutoa msafara wa ustaarabu huo wenye kufuatana na mapambano ya moja kwa moja ya harakati zake na maendeleo yake una athari kubwa katika kuandaa fikira na kuimar- isha ujuzi wa kiutawala kwa ajili ya siku tuliyoahidiwa, kwa sababu unamweka mwanadamu aliyeandaliwa mbele ya utendaji mwingi wa wengine wenye kila aina ya nukta ya udhifu na uimara, makosa na usahihi na unampa mtu huyu uwezo mkubwa mno katika kutathmini mambo ya kijamii kwa ujuzi kamili juu ya sababu zake na mazingira yake yote ya kihistoria.

Kisha mabadiliko yanayomsubiri kiongozi anayengojewa yanasimama kwa msingi wa ujumbe maalumu nao ni ujumbe wa Uislamu, na kwa kawaida hali hii inahitaji kiongozi wa karibu na vyanzo vya mwanzo vya Uislamu. Ambaye utu wake umejengeka kikamilifu kwa sura ya kujitegemea na ya kipekee iliyojitenga na athari za ustaarabu ambao amekadiriwa kuupiga vita siku hiyo tuliyoahidiwa.

Hali hiyo ni kinyume na mtu ambaye anazaliwa na kukulia ndani ya ustaarabu huu na fikira zake na hisia zake vinafunguka ndani ya mazingira yake, hakika aghlabu hanasuki kutoka kwenye ustaarabu huo na malengo yake hata kama akiongoza mapambano ya mabadiliko dhidi ya ustaarabu huo.

Ili kiongozi aliyehifadhiwa asalimike na ustaarabu huo ambao kaan- daliwa kuubadilisha ni lazima utu wake uwe umejengeka kikamilifu katika kipindi cha ustaarabu uliotangulia ulio karibu mno na roho ya jamii yote na atoke upande wa asili mpaka kwenye hali ya ustaarabu ambao siku tuliyoahidiwa inaelekea

kuutimiza chini ya uongozi wake."[11]

Kisha mheshimwa (r.a.) baada ya hapo akatoa swali jingine linalohu- siana na upande wa kibinadamu kuhusu akida ya Mahdi, nalo ni: Kwa nini kiongozi wa kiulimwengu hajadhihirika muda wote huu? Na ikiwa tayari ameshajiandaa kwa ajili ya kazi ya kijamii basi ni kitu gani kili- chomzuia kudhihiri kwenye uwanja wa maisha zama za ghaibu ndogo au baada yake badala ya kuigeuza na kuwa ghaibu kubwa?

Jibu ni kuwa: a. Hakika Mtume (s.a.w.w.) kivitendo alikuwa chini ya hali ya kujitenga kikamilifu dhidi ya ustaarabu wa kijahiliya, kama ilivyopokewa ndani ya sira ya Mtume kuwa alikuwa akijipwekesha akienda pango la Hira akikaa huko. Na pia manabii walikuwa wakijiepusha na mazingira ya jamii zao na hivyo kujitenga, na hilo limeashiriwa na kauli ya Mwenyezi Mungu: "Basi alipojitenga nao na wanayoyaabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu, tukampa Isihaka na Yakubu, na kila mmoja tukamfanya Nabii." Sura Maryam: 49.

b. Hakika Nabii Mtume hupewa wahyi na hupewa nguvu moja kwa moja na Mola na hufikia kazi na hatua anazozichukua hatua kwa hatua, na Imam hapewi wahyi na wala hafikii vitu moja kwa moja kutoka kwa Mola. Ndiyo, yuko chini ya uan- galizi wa Mola hivyo yeye anahitaji maandalizi maalumu, wakati ambao anakuwa karibu na mwenye mahusiano na ustaarabu wa kiisilamu akitegemea baba zake katika asili, elimu na maarifa ni wakati huohuo anakuwa mjuzi juu ya mambo ya wanadamu na ustaarabu, anajua jinsi gani unakua, sababu za kujengeka kwake na kupata nguvu yake, na ni jinsi gani unashuka, sababu za kudhoofika na kuporomo- ka. Hivyo anategemea ujuzi, uwezo na uwelewa wa mambo yote, hali hii ni bila kusahau imani yetu kuwa Imam ana uwezo wa asili wa elimu ambayo Mwenyezi Mungu humtunuku na kupewa nguvu na Mola

Kwani zama hizo mazingira ya kikazi kijamii na kimabadiliko yalikuwa mepesi na rahisi, na mawasiliano yake na watu ya kivitendo kupitia utaratibu wa ghaibu ndogo ulikuwa unampa fursa ya kuku- sanya nguvu zake na kuanza kwa nguvu zote, pia nguvu iliyokuwa ikitawala zama hizo ilifikia kiwango cha chini kuliko nguvu na uwezo ambao amefikia mwanadamu baada ya hapo kupitia maendeleo ya kiteknolojia na kiviwanda.[12]

Jibu: "Kila kazi ya mabadiliko ya kijamii kufaulu kwake kuna uhu- siono na masharti na mazingira ya kadhia husika, malengo yake haya- timii ila baada ya masharti na mazingira hayo kutimia. Mabadiliko ya kijamii ambayo yanafanywa na Mola aridhini yana sifa ya pekee kwa sababu yenyewe upande wake wa kimola hayana uhusiano na mazin- gira ya kadhia husika,[13] kwa sababu ujumbe unaotegemewa na mabadiliko hapa ni wa kimola, lakini upande wa utekelezaji unatege- mea mazingira ya kadhia husika na hivyo kufaulu kwake na wakati wake vina uhusiano na mazingira hayo.

Kwa ajili hiyo Mola alisubiri zipite karne tano za ujahiliya ndipo akateremsha ujumbe wake wa mwisho mikononi mwa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kwa sababu mahusiano ya mazingira ya kadhia husika ya utekelezaji yalikuwa yakilazimu kuchelewesha ujumbe huo japokuwa ulimwengu ulikuwa na haja nao tokea muda mrefu kabla ya hapo.

Mazingira ya kadhia husika ambayo yana mchango katika kutekeleza kazi ya mabadiliko baadhi yake hutengeneza hali munasibu na anga kuu kwa ajili ya mabadiliko yanayolengwa, na baadhi yake huten- geneza baadhi ya vipengele ambavyo harakati za mabadiliko zinavihi- taji kupitia kona zake zote.

Kwa mfano kazi ya mabadiliko aliyoyaongoza Lenin huko Urusi na kufaulu ilikuwa na uhusiano na sababu kama vile vita vikuu vya kwan- za vya dunia na kuporomoka kwa utawala wa Kaysari, na hili lilisaidia kupatikana mazingira munasibu ya kazi hii ya mabadiliko. Pia ilikuwa na uhusiano na sababu nyingine ndogo ndogo kama vile kusalimika kwa Lenin mwenyewe katika safari yake ya uficho kuingia Urusi na kuongoza mapinduzi, kwani angepatwa na tukio lolote ambalo lingemzuia basi inatarajiwa kabisa kuwa mapinduzi hayo yangekosa nguvu zake na kutokudhihiri mapema.

Sera ya Mwenyezi Mungu isiyokuwa na mabadiliko katika kazi ya mabadiliko ya kimola imeendelea kuhitaji mazingira ya kadhia husika upande wa utekelezaji, mazingira ambayo hutimiza hali munasibu na anga kuu ili kufanikisha kazi ya mabadiliko, na kuanzia hapa ndipo Uislamu haukuja ila baada muda fulani wa mitume na baada ya kumalizika uchungu ulioendelea muda wa karne nyingi.

Japokuwa nguvu ya Mwenyezi Mungu ilikuwa na uwezo wa kudhalil- isha kila lililo tatizo na gumu mbele ya ujumbe wa Mola, na kuten- geneza hali munasibu kimuujiza lakini hakutaka kutumia njia hii, kwa sababu mtihani, balaa na matatizo ambayo kupitia kwayo mwanadamu hukamilika yanalazimu kazi ya mabadiliko iwe katika hali ya kawaida na ya kikadhia husika kwa upande huu.

Hili halimzuii Mwenyezi Mungu baadhi ya nyakati kuingilia baadhi ya yale yanayohusu vipengele ambavyo huwa si hali munasibu, bali baad- hi ya nyakati harakati uhitajia hilo ndani ya hali hiyo munasibu, na miongoni mwa mahitajio hayo ni msaada na nguvu za ghaibu ambazo Mwenyezi Mungu huwatunuku mawalii wake ndani ya saa ngumu na hivyo kupitia msaada huo uuhami ujumbe.

Ghafla moto unakuwa baridi na salama juu ya Ibrahim,14 mkono wa myahudi ambao uliinua upanga juu ya kichwa cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) unapooza na kukosa nguzu za kufanya kazi,15 ghafla kimbunga kikali kinang'oa mahema ya makafiri na mushirikina ambao waliuzingira mji wa Madina siku ya vita vya Handaki na kutia woga ndani ya nafsi zao,16 isipokuwa haya yote hayavuki vipengele. Kwani kutoa msaada katika saa ngumu baada ya anga kuwa munasibu na hali kulingana na kazi ya mabadiliko kwa ujumla, kunaweza kukawa kwa sura ya kawaida na kwa kulingana na mazingira ya kadhia husika.

Inajulikana kuwa Mahdi hakuwa amejiandaa kwa ajili ya kazi ya jamii fulani wala kwa ajili ya kazi ya mabadiliko inayokomea eneo fulani la ulimwengu na kuacha eneo jingine, kwa sababu ujumbe wake ambao umehifadhiwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili yake ni mabadiliko kamili ya ulimwengu na kuwatoa wanadamu toka kwenye giza la ujeuri mpaka kwenye nuru ya uadilifu.17

Kazi hii ya mabadiliko makubwa utekelezaji wake hauhitajii kupatikana tu ujumbe na kiongozi msuluhishi kwani ingekuwa hivyo masharti yake yote yangetimia tangu zama za utume, bali ni kuwa unahitaji vilevile hali munasibu ya kiulimwengu na anga kuu la kimataifa ambalo litatimiza mazingira ya kadhia

husika kwa ajili ya kazi ya mabadiliko ya kiulimwengu.

Hivyo upande wa binadamu inachukuliwa kuwa kile kitendo cha wanadamu kutambua ustaarabu kwa undani ni sababu ya msingi wa kutengeneza mazingira munasibu ili kupokea ujumbe mpya wa uadili- fu, utambuzi huu wa ndani hujengeka na kuimarika kupitia mazoea ya ustaarabu wa namna mbalimbali ambao humo mwanadamu hutoa ustaarabu mpya huku akiwa mzito kutokana na yale yakuachwa aliyo- jengeka kwayo, huku akijua fika haja yake inahitaji msaada na akiita- mbua nguvu ya ghaibu kwa maumbile yake.

Upande wa kimaada ni kuwa huenda masharti ya maisha ya kimaada ya kisasa yakawa na nguvu mno katika kutimiza ujumbe ulimwenguni kote kuliko maisha ya zamani katika kipindi cha ghaibu ndogo, hiyo nikutokana na ukaribu wa masafa, uwezo mkubwa katika kuamiliana na mataifa mbalimbali ya aridhini na kupatikana vifaa na nyenzo ambazo makao makuu inazihitaji ili kupanua uelewa wa mataifa ya ulimwengu na kuyaelimisha kwa msingi wa ujumbe mpya.

Ama kuhusu kile kilichogusiwa katika swali kuwa kila muda wa kud- hihiri kwake unavyozidi kurefuka ndivyo nguvu za kijeshi na vifaa vitakavyopambana na kiongozi siku hiyo tuliyoahidiwa vinavyozidi kukua, kweli hili ni sahihi, lakini ukuaji wa nguvu kimaada zitasaidia nini ikiwa kisaikolojia ndani ya nafsi umeshashindwa, huku nguvu ya kiroho kwa mwanadamu ambaye ndiye anamiliki nguvu hizo na vifaa hivyo imeshasambaratika? Ni mara ngapi ndani ya historia jamii ya ustaarabu wenye nguvu imesambaratika mwanzo tu wa vita kwa sababu tu kabla ya vita hivyo ilikuwa imeshasambaratika kisaikolojia huku ikiwa haijiamini na wala haina matumaini na muundo wake na imekosa imani na hali yake halisi?"18

Pia tunaweza kuzungumzia faida ya kiakida ya wazo la Mahdi kwa mwanadamu katika uwelewa wa Ahlul-Bait (a.s.) kwa upande mwingine. Hivyo tunasema: Itikadi ya kuamini wazo la Mahdi aliyem- bali na macho lakini aliye hai na mwenye kuingilia baadhi ya matukio kwa ajili ya masilahi ya kundi lenye kuamini huku akiwa ana sifa zote za uimamu kuanzia utakaso, nasi ya Mtukufu Mtume na ukamilifu wa kielimu na kivitendo kwa kawaida ni lazima ieneze ndani ya jamii hali ya uimamu huu na nguvu zake za kimaana na kiroho za hali ya juu.

Na ni lazima imshibishe mwanadamu hisia nzuri kwa kule kuendelea kuwepo mahusiano kati ya ardhi na mbingu na mbingu kuendelea kuitunza ardhi na kubadili hali hiyo na kuwa maana zenye kuonekana kivitendo zenye msukumo mkubwa ndani ya nafsi baada ya awali ndani ya misingi yake ya kiakida kuwa ni maana za akilini.

Na ni lazima iimarishe utawala wa Tawhidi ndani ya uwanja wa kijamii na kisiasa na kuufanya ni utawala ulio karibu na hisia ya mwanadamu kwa kutambua kuwa Mahdi aliye ghaibu si mwanadamu wa kawaida bali yeye ni Imam wa kumi na wawili aliyeteuliwa na Mola ili ashughulikie nafasi ya uimamu mpaka mwisho wa historia.

Sahihi watu hawamwoni moja kwa moja kwa milango ya fahamu laki- ni kule kuamini kuwa yeye ni

ukweli wa kimaada kunapunguza hamasa ya milango yetu ya fahamu kutaka kumdiriki, inaifanya nafsi iwe katika hali ya kuamiliana kiroho na kiutii na njia ya uimamu uliy- oteuliwa na Mola na uliyo mtakasifu kwa kuzingatia kuwa wenyewe ni maelezo na mwendelezo wa utawala wa Tawhid aridhini.

Muamala huu unazidi zaidi pale Mahdi mtakasifu aliye ghaibu anapo- tolewa maelezo ya kisiasa yaliyo barizi kupitia msingi wa unaibu maalumu ndani ya kipindi cha ghaibu ndogo na msingi wa unaibu wa wote wa Wanachuoni wa sharia ndani ya kipindi cha ghaibu kubwa ambao ni uongozi wa kisiasa wa kisharia wa jamii ya kiisilamu ambao unahifadhi nafasi ya juu ya uimamu kama msimamizi na mwangalizi anayefatilia uzoefu wa kisiasa na kijamii na kuunusuru na kama chem- chemu inayounywesha sharia pale inapoukuta unaafikiana na Uislamu.

Kutokana na mjumuiko wa ubainifu huu inaonekana wazi maana ya ukamilifu inayotolewa na uwelewa wa wazo la Mahdi kwa Ahlul-Bait (a.s.) wa faida za kibinadamu nazo ni faida zinazooana kikamilifu na asili ya wazo la Mahdi, kwani Mahdi mtakasifu aliye ghaibu ni mwenye harakati na mwenye kuleta athari za utii katika hali halisi ya mwanadamu.

Wakati Mahdi ndani ya uwelewa wa masunni hana athari yoyote kati- ka hali halisi ya mwanadamu, naye si chochote zaidi ya habari za mus- takabali. Kana kwamba Mahdi wa Ahlul-Bait (a.s.) anachukua jukumu la kutimiza unayoahidi kupitia msukumo wa hali halisi ya mwanadamu na muamala wa utii pamoja naye.

Suala hili lenyewe ni jambo bora linalofafanua maana ya utii ya uwele- wa wa kungojea, kwani kungojea faraja si kunyamaza na kushindwa bali ni roho ya utii yenye msukumo kuelekea mabadiliko ya Mahdi yanayohitajika.

Matokeo ya uchambuzi

Mwisho wa uchambuzi tunaweza kufupisha matokeo ya uchambuzi kwa nukta zifuatazo:

Hakika dini ni mabadiliko kamili ya uhalisia wa binadamu na Uislamu ni mabadiliko kamili zaidi juu ya uhalisia wa dini na Ushia ni maelezo kamil- ifu zaidi juu ya uhalisia wa Uislamu na hatimaye Mahdi wa Ahlul-Bait (a.s.) ndiye maelezo kamilifu zaidi kuhusu asili ya wazo la Mahdi ambaye waisilamu wote wamekongamana katika kumwamini.

Asili ya tofauti kati ya Mahdi wa Ahlul-Bait na Mahdi wa Wanachuoni wa kisunni inatokana na uimamu, kwani Mahdi kwa madhehebu ya Ahlul-Bait (a.s.) ndiye Imam wa kumi na wawili (a.s.) wakati kwa upande wa madhe- hebu ya kissuni ni suala la mustakabali lisilokuwa na kitu.

Kwa kuwa suala la Mahdi kwa Ahlul-Bait ni suala la Imam wa kumi na wawili ambaye hakuna tena baada yake Imam basi kuanzia hapa uwelewa wa wazo la Mahdi kwao (a.s.) limekuwa na sifa tatu muhimu: Kuzaliwa Imam kwa siri kulikofichwa, uimamu wa utotoni na ghaibu yake inayolaz-

imu umri mrefu unaolingana na zama. Sifa hizi tatu zimethibiti kwa kuthibiti asili ya uimamu wa maimamu kumi na wawili watakasifu ambao ndio umezaa wazo la Mahdi, ukiachia mbali dalili za wazi ambazo tumes- hazitaja moja baada ya nyingine.

Hakika sifa hizi tatu si tu kwamba zimethibiti kwa dalili za kiakida, kiak- ili na kimaumbile zilizokamilika na si tu kwamba hazihitajii utata wa kiak- ili na kidini, bali vilevile zenyewe ndizo zinazotoa maana ya ukamilifu ya uwelewa wa wazo la Mahdi, na kuufanya uwe ni uwelewa wenye thamani ya kiakida na faida za juu kwa mwanadamu na kufaa zaidi ndani ya jamii, huku ukikamilika na kuoana na faida za msingi wa dini ndani ya maisha ya mwanadamu.

Na mwisho wa dua yetu ni kumshukuru Allah Mlezi wa walimwengu.

---

1. Sura Anbiyai: 107.
2. Bahthu Hawlal-Mahdi: 83 – 89, uhakiki na maelezo ya Dk. Abdul Jabbar Shararah.
3. Anaashiria imani ya Shia Imamiya inayotegemea dalili za kiakili na za nukuu, na hasa Hadithi mutawatiri ya vizito viwili: "Mimi nimewaachieni viwili ambavyo laiti mkishikamana navyo kamwe hamtopotea baada yangu: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu watu wa nyumba yangu." Rejea kitabu Sahih Muslim 4: 1873. Rejea As-Sawaiq Al-Muhriqah cha Ibnu Hajar: 89, amesema: "Kisha tambua kuwa Hadithi ya kushikamana navyo ina njia nyingi za upokezi, imepokewa kutoka kwa maswahaba zaidi ya ishirini." Na pia anaashiria kauli ya (s.a.w.w.): "Havitoachana mpaka vitakaponikuta kwenye Hodhi..." na kauli yake (s.a.w.w.): "Makhalifa baada yangu ni kumi na wawili wote ni kutoka kwa maku- rayshi." Zote hizo zinatengeneza maana hii.
4. Mtukufu Mtume mara nyingi sana amezungumzia sifa zao, mizunguko yao, jukumu lao na kazi yao na kuwa wao ni wabebaji wa sharia, meli za uongofu, amani ya umma na kinga yake dhidi ya upotovu, kama ilivyoelekeza hilo Hadithi ya vizito viwili na Hadithi ya hivyo viwili havitoachana. Zote wawili zinasisitiza utakaso wao, kwani akili haikubali kuwa wao wasiwe watakasifu kisha wao ni kinga kwa umma dhidi ya upotovu na wasiachane na Qur'ani takasifu. Rejea kitabu Usulul-Amma Lil-Fiqhi Al-Muqarin cha Allamah Muhammad Taqiyu Al- Hakim, uchambuzi wa hoja ya Sunna, Uk 169 na unaofuatia
5. Kiongozi wa kihistoria awe ameandaliwa kisaikolojia maandalizi yanayona- sibiana na jukumu husika. Na laiti tukirudi ndani ya Qur'an tukufu tuitaikuta inazungumzia suala hili ndani ya historia ya manabii kwa sura ya wazi zaidi. Na hasa katika yale yanayomuhusu Nabii Nuhu (a.s.) nalo ni jambo linalozindua na kuvutia, na huenda hilo likatokana na kule kushabihiana katika jukumu walilok- abidhiwa, kama alivyonabihi Shahid As-Sadri. Rejea kitabu Maal-Anbiyai cha Afif Abdul-Fatah Tabarah.
6. Maana hii tunaweza kuiona kwenye muungano wa kisovieti jinsi ulivyokua na kustawi mpaka ukawa nguvu ya pili ulimwenguni, wenyewe na Marekani vik- agombania ustaarabu na nguvu ya kisiasa, wote kwa pamoja wakapanda angani na hatimaye tukashuhudia usambaratikaji wa muungano wa kisovieti na misingi yake kuachana kwa kasi ya ajabu. Hilo lina athari kiasi gani? Hilo lina mafunzo kiasi gani? Hilo ni dalili ya kina kiasi gani?
7. John Jack Rusuw (1712 – 1778 A.D.) mwandishi na mfilosofia wa kifaransa, baadhi ya wanafikra wanamchukulia kama mtu mwenye mchango mkubwa katika fasihi ya kifaransa ya kisasa na filosofia mpya. Maandishi yake na makala zake viliandaa mapinduzi ya kifaransa, na kitabu chake maarufu ni Al-Aqdu Al- Ijtimaiy. Rejea kitabu Mawsuatul-Mawridu cha Muniru Al-Baalabakiy 8: 169.
8. Anaashiria Aya ya Qur'an: "Hakika wao ni vijana waliomwamini Mola wao Mlezi, nasi tukawazidishia katika mwongozo." Sura Al-Kahfi: 13. Rejea tafsri ya Ayah ii ndani ya kitabu Al-Kashaf cha Az-Zamakhshar 2: 706, kilichosambazwa na Darul-Kitabi Al-Arabi – Beirut.
9. Anaashiria Aya: "Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu na wakazidisha tisa." Sura Al-Kahfi: 25.
10. Hayo yote yana mchango katika kumlea na kumwandaa maandalizi maalu- mu ikiwemo kummlikisha mtazamo wa kina

kamilifu, ukiachia mbali kile kitendo cha yeye mwenyewe binafsi kushuhudia kufeli kwa hao waliobobea kwenye dunia na kuwatisha watu. Ushahidi huu unamwezesha mara nyingi katika kutekeleza jukumu lake la kiulimwengu katika mabadiliko, yaani kuijaza dunia uadilifu kama utakavyokuwa umejaa dhuluma. Haya yote ni bila kujali uwezo wake wa dhati na msaada maalumu wa Mola.

11. Wala haifai mtu yeyote kuzua utata kuwa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) japokuwa ujumbe wake ulikuwa ni wa kiulimwengu na jukumu lake kubwa la mabadiliko isipokuwa yeye aliishi ndani ya mazingira ya ustaarabu wa kijahiliya na wala haukumuathiri, na ndio hali ya manabii waliomtangulia, sasa ni upi ubora wa rai hii?

12. Bahthu Hawlal-Mahdi cha Shahid Muhammad Baqir As-Sadri, rejea ya 89, uhakiki na maelezo ya Dk. Abdul Jabbar Shararah, chapa ya kituo cha Ghadir kwa ajili ya masomo ya kiisilamu.

13. Pamoja na umuhimu huu ambao Shahid As-Sadri ameuandika kuhusu mazingira ya kadhia husika na pia kuhusu mchango wake katika kuivisha na kuandaa mapinduzi mbalimbali ila ni kuwa Shahid As-Sadri anatoa mtazamo mpya katika kufahamu kazi ya mabadiliko ya kijamii yanayoletwa na Mola kupi- tia ujumbe Wake kuwa, upande wake wa kiujumbe yana uhusiano wake maalumu lakini upande wa utekelezaji yanategemea mazingira ya kadhia husika na hivyo yanahusiana nayo kiwakati na kiufaulu. Tunaposema mazingira ya kadhia husika tunamaanisha kuwa ni hali ya kisiasa na hali ya kijamii ya umma na hali halisi ya dola za wakati huo na kiwango cha nguvu za umma katika uwezo wake binafsi na maandalizi yake ya kisaikolojia.

14. Anaashiria kauli ya Mwenyezi Mungu: " Wakasema: Mchomeni na muiokoe miungu yenu ikiwa nyinyi ni wenye kutenda.* Tukasema: Ewe moto! Uwe baridi na salama juu ya Ibrahim.* Na wakamtakia ubaya lakini tukawafanya kuwa wenye kupata hasara." Sura Anbiyau: 68 – 70.

15. Rejea riwaya hii katika tafsiri ya Ibnu Kathir 2: 33 na rejea Al-Bihar cha Al- Majlisiy 18: 47 na 52 na 60 na 75, mlango wa miujiza ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

16. Tarikh At-Tabar 2: 244, matukio ya mwaka wa tano hijiriya.

17. Kama ilivyo nassi ya Hadithi ya Mtukufu Mtume: "Hata kama dunia haito- bakiwa ila na siku moja tu basi Mwenyezi Mungu atairefusha siku hiyo mpaka amlete mtu kutoka kizazi changu au kutoka watu wa nyumba yangu ili aijaze ardhi usawa na uadilifu kama itakavyokuwa imejaa dhuluma na ujeuri." Rejea kitabu At-Taju Al-Jamiu Lil-Usul 5: 343, amesema: "Ameipokea Abu Dawdi na Tirmidhiy".

18. Tumeshuhudia mwanzoni mwa miaka ya tisini mfano halisi wa kauli hii aliy- oitoa Shahid As-Sadri kutokana na ujuzi wake wa kina juu ya jamii ya mwanadamu, kwani muungano wa kisovieti umeporomoka haraka sana na kwa namna ambayo iliwashangaza wote, nao ulikuwa ni moja kati ya nguvu wawili zilizokuwa zikiutisha ulimwengu.

Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Juzuu ya Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)

8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al–Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo

47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as–Salaatu Khayrun Mina –'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume – Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume – Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume – Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l–Balaghah – Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l–Balaghah – Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu – Sehemu ya Tatu
67. Tujifunze Misingi Ya Dini
68. Sala ni Nguzo ya Dini
69. Mikesha Ya Peshawar
70. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
71. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
72. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
73. Liqaa–u–llaah
74. Muhammad (s) Mtume wa Allah
75. Amani na Jihadi Katika Uislamu
76. Uislamu Ulienea Vipi?
77. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
78. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
79. Raja'a
80. Shahidi kwa ajili ya Ubinadamu
81. Al – Badau
82. Raja'a
83. Kuanzia ndoa hadi kuwa wazazi
84. Historia na sera ya Viongozi wema.
85. Visa vya Kweli

86. Mtoto mwema
87. Maarifa ya Kiislamu

Back Cover

Kwa Waislamu, imani ya kuja kwa Mahdi (Muhudi) karibu ya mwisho wa dunia ni imani ambayo ina asili katika dini. Waislamu wote bila kujali tofauti za madhehebu zao wanakubaliana juu ya imani hii kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.) alisema: “Hata iwe imebakia siku moja tu kwa dunia hii kufikia mwisho wake Allah atairefusha siku hiyo ili kumwezesha Imam huyo kutawala na kuujaza ulimwengu huu uadilifu, amani na utulivu wakati ambapo ulikuwa umejaa ufisadi na dhulma.”

Kitu cha kuvutia ni kwamba imani hii haiko kwa Waislamu tu bali hata katika dini nyingine wana imani kama hii kwamba atatokea mtu wakati wa mwisho ambaye ataondoa dhulma na ufisadi na kuujaza ulimwengu huu uadilifu, amani na utulivu.

“Hakika ulimwengu unalingojea suluhisho litakaloukusanya chini ya ben- dera moja na tamko moja.” (Bertrand Russell)

“Hakika haiko mbali siku ambayo ulimwengu wote utatawaliwa na amani na usafi na watu kuwa katika hali ya kupendana na undugu.” (Albert Einstein)

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com [13]
Tovuti: www.ibn-tv.com [14]
Katika mtandao: www.alitrah.info [15]

Source URL: https://www.al-islam.org/sw/imam-mahdi-katika-usunni-na-ushia

Links
[1] https://www.al-islam.org/sw/user/login?destination=node/23324%23comment-form
[2] https://www.al-islam.org/sw/user/register?destination=node/23324%23comment-form
[3] https://www.al-islam.org/sw/person/sayyid-sadiq-al-husaini-al-shirazi
[4] https://www.al-islam.org/sw/organization/al-itrah-foundation-0
[5] https://www.al-islam.org/sw/person/abdul-karim-juma
[6] https://www.al-islam.org/sw/library/imam-al-mahdi

[7] https://www.al-islam.org/sw/tags/sunna

[8] https://www.al-islam.org/sw/tags/historia

[9] https://www.al-islam.org/sw/tags/imani

[10] https://www.al-islam.org/sw/person/imam-al-mahdi

[11] https://www.al-islam.org/sw/person/ahlul-bayt-0

[12] https://www.al-islam.org/sw/person/mtume-muhammad-saw

[13] mailto:alitrah@raha.com

[14] http://www.ibn-tv.com

[15] http://www.alitrah.info